28 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 28 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):

Taarifa ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. AMINA GOOD SAID K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Amina, Mjumbe wa Kamati hiyo.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza Maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 450

Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kisutu – Bagamoyo

MHE. SUBIRA K. MGALU aliuliza:-

Je, lini ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kisutu itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kisutu ina jumla ya wakazi 7,714. Wananchi wa Kata hii wanapata huduma za Afya katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambayo ipo umbali wa kilometa tisa kutoka Makao Makuu ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya katika Kata za kimkakati. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2026/2027 Serikali imeitengea Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo jumla ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kisutu pamoja na kukamilisha miradi viporo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya kwenye Kata za kimkakati ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza, ninaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuahidi na kutekeleza na kwa bajeti ya 2026/2027 kutenga shilingi milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kisutu. Kwa niaba ya wananchi wa Kisutu na wa Jimbo la Bagomoyo tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu madogo ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hospitali yetu ya Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo inatoa huduma za rufaa, na kwa kuwa zaidi ya 80% ya rufaa hizo inatokana na majeruhi wa ajali mbalimbali kutokana na mji wetu kupitiwa na barabara kubwa inayoenda mikoa ya kaskazini, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya upasuaji pamoja na kuleta mtaalamu wa upasuaji wa mifupa ili kuwasaidia wananchi wanaopata ajali na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Tumbi na Hospitali ya Muhimbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya mitungi ya gesi katika Halmashauri yetu ya Bagamoyo kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa na mitungi hiyo imekuwa ikiagizwa *Tanzania Oxygen Company Limited,* Dar es Salaam na kuipelekea hospitali yetu kupata gharama nyingi, na wastani wa matumizi ya mitungi imefika mitungi 36, 40 mpaka 45 kwa wiki, na kutokana na maono ya Serikali kwamba kutakuwa na shughuli mbalimbali katika miradi ya kimkakati, na maana yake mji wetu utakuwa na watu wengi watakaohitaji huduma hizo? je, Serikali haioni iko haja ya kutujengea jengo *(oxygen plant)* katika Hospitali ya Halmashauri ya Bagamoyo?Je, Serikali iko tayari kuanza tafakuri ya mpango huo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, kwa kufuatilia na ametoa shukurani hapa, amekiri kuhusu Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi. Hospitali zetu za wilaya siyo zote ambazo zinafanya hizi huduma za upasuaji wa mifupa, hizi huduma za kibingwa. Kwa hiyo, niendelee kumwambia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Bagamoyo, tuendelee kutumia hospitali zetu za rufaa zile ambazo ni Tumbi na Bagomoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ina mpango mkakati madhubuti kabisa wa kuhakikisha tutajenga *emergency wards* ambazo zitakuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia wagonjwa hawa, majeruhi wetu katika barabara zote *trunk road,* na tumeshaanza kazi hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kufanya tathmini na kuona ni namna gani tunajenga *theatre* za upasuaji katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu *oxygen*, tunakiri kwamba mitambo hii ya *oxygen plant,* kufanya *installation* yake ni gharama kubwa. Mpaka muda huu hospitali yetu hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge inapata huduma kupitia Mfumo wa *Medical Gas Manifold,* kwa wagonjwa wanaohitaji. Pia,

wanaendelea kupata *supply* ya mitungi ya *oxygen* kutoka hospitali zote za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wananchi wetu pale wanaendelea kupata huduma hii ya *oxygen* na tutaendelea kufuatilia kuona umuhimu wa kujenga *plant* hii maeneo ya karibu zaidi na kuweza ku-*supply* katika hospitali hizi. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Manolo iliyoko katika Halmashauri ya Lushoto ndiyo kata yenye wakazi wengi kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Kata hii iko katika vipaumbele vya kujengewa kituo cha afya. Sasa, ninatamani kujua, ni lini Serikali itapeleka fedha ili ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Manolo uweze kuanza? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulingana na Sensa ya Watu na Makazi, kata hii ndiyo ina idadi kubwa ya watu na Serikali tumeshaelekeza mwaka 2025/2026 tulitenga bajeti kuanza ujenzi wa kituo cha afya katika kata hii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa kata hii kwamba tunakwenda kujenga kituo cha afya katika eneo hili ili liweze kuhudumia wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali langu. Kwanza, kabisa ninaipongeza Serikali, imejenga hospitali kubwa na nzuri sana kwenye Wilaya ya Mlele na Jimbo la Katavi, lakini hospitali ile ina upungufu. Tumekuwa na changamoto kubwa ya kuhamisha wagonjwa kuwatoa wodi moja kuwapeleka wodi nyingine kwa

maana ya kwamba *walkways* hazipo, imepelekea kipindi cha mvua wagonjwa kubebwa mgongoni. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kupeleka fedha ili kujenga zile njia *(walkways)* za kuhamisha wagonjwa kutoka wodi moja kuwapeleka wodi nyingine ili kuondoa upungufu uliopo katika Hospitali ya Wilaya ya Mlele?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Thomas Maganga, kwa kufuatilia na hitaji hili la *walkway*. Tulishatoa maelekezo na niseme tu na nimhakikishie yeye pamoja na wananchi kwamba hospitali zetu zote za wilaya tumeshazitengea bajeti mwaka huu wa fedha 2026/2027 ili kuhakikisha miundombinu wezeshi inayohitajika tunakwenda kuikamilisha kwa wakati ili wananchi wetu waendelee ku-*enjoy* tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kituo cha afya cha Bunda Mjini, Naibu Waziri anakijua, kiko pale kimkakati, kinatoa huduma kwa takribani kata zaidi ya nne (Balili, Kabarimu, Bunda Mjini, Nyasura pamoja na Bunda Stoo). Kata zote pale zinategemea kile kituo na kina hudumia watu wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu wa *OPD,* wodi ya wanawake, wodi ya wanaume na wodi ya watoto, zaidi ya shilingi milioni 650 zinahitajika. Ni lini sasa mtakamilisha ili wananchi waweze kupata huduma ya afya inayostahiki kwenye Jimbo la Bunda Mjini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu

Spika, tumeshafanya utaratibu wa bajeti katika kupeleka fedha katika kituo hiki cha afya cha Bunda Mjini ili kiweze kuhudumia mama zetu katika eneo hilo hasa katika eneo la kujifungua. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Ester Bulaya na nimwelekeze Mkurugenzi kwamba fedha zikiingia kwanza ampe taarifa Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuona namna gani Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inavyowajali wananchi na kupeleka fedha za kwenda kukamilisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Isack Copriano, swali la nyongeza.

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza na mimi swali dogo la nyongeza. Kata yangu ya Mfereji sasa ni vipindi viwili imekuwa ikiwekwa kwenye bajeti kwa ajili ujenzi wa kituo cha afya. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya kwenye Kata ya Mfereji ambayo iko pembezoni mwa Wilaya ya Monduli?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Isack kwa kuuliza swali la nyongeza. Pia Mheshimiwa Isack tulikuwa naye kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maeneo hayo na tuliweza kuzungumza na tukapokea kero za wananchi moja kwa moja. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kutenga fedha na kujenga kituo hiki cha afya ili kiweze kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 451

Ujenzi wa Barabara ya Madukani - Mateneni Moshi Vijijini

MHE. MORRIS J. MAKOI aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Rau Madukani - Mamboleo - Materuni kilometa 7.8 kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Rau Madukani - Mamboleo - Materuni inayoanzia katika eneo la Rau Madukani kwenda Materuni inahudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* yenye urefu wa jumla ya kilometa 9.99.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kujenga barabara hii ya Rau Madukani - Mamboleo - Materuni kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 kwa awamu tatu kwa kiwango cha lami ambapo mpaka sasa tumejenga jumla ya kilometa 2.91 zimeshakamilika kwa jumla ya shilingi bilioni 1.11.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* iliendelea kutenga bajeti katika barabara hii kwa lengo la kuendelea kuijenga kwa kiwango cha lami kwa mchanganuo ufuatao. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 229.86 kujenga kilometa 0.235 tabaka la lami ambapo utekelezaji wake unaendelea na mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 164.03 kujenga kilometa 0.15 tabaka la lami ambapo utekelezaji wake upo kwenye hatua ya ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, swali la nyongeza.

MHE. MORRIS J. MAKOI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza. Hii barabara anayozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni barabara inayoenda kwenye maanguko makubwa ya maji ya *Materuni Water Falls,* ambayo kupitia Halmashauri ya Moshi yanaiingizia Serikali zaidi ya shilingi milioni 20 kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wamekuwa wanapata sintofahamu kwa sababu barabara inaingiza fedha, inaleta watalii, lakini bado Serikali haijaweka umuhimu mkubwa. Sasa je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha lile eneo lililobaki kuelekea kwenye maanguko ya maji linafanyiwa matengenezo ya kawaida kuwa na mitaro na kadhalika ili liweze kupitika wakati Serikali ikiendelea na mpango wa lami kidogo kidogo kama inavyoonekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili. Kwa vile barabara hii inasaidiana na barabara inayokwenda Shimbwe kuanzia Mamboleo; na Serikali pia imeweka fedha kwa mfumo huo wa kujenga kipande, kipande, je, Naibu Waziri ana kauli gani juu ya kuhakikisha barabara hizi mbili kwa ajili ya watu wa Shimbwe na watu Materuni *Water Falls* zinapitika wakati wote wa masika na kiangazi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Makoi kwa kufuatilia miundombinu ya barabara katika jimbo lake. Kwa niaba ya Waziri

wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Meneja wa *TARURA* kufanya tathmini ya mitaro yote ya barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, kwani bila kujenga mitaro, barabara zetu zinakuwa hatarini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukijenga mitaro bora italea barabara zetu hata kama ni zile za changarawe ili ziweze kupitika masika na kiangazi. Kwa hiyo, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* Wilaya, afanye tathmini na awasilishe andiko Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ili tuone namna gani ya kuanza kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshatoa maelekezo haya kwa Mameneja wote wa mikoa na wa kanda ili kuhakikisha kwamba tunazipitia barabara zetu zenye changamoto hasa kipindi cha mvua ili tuone namna gani ya kuziboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, niendelee kumwelekeza Meneja afanye andiko na awasilishe barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ili tuone namna gani ya kuanza kutenga bajeti na kujenga kwa awamu ili wananchi wetu waendelee kupita katika mazingira bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mvua nyingi sana kunyesha kwenye maeneo mengi nchini hasa kwenye Mkoa wa Katavi, Jimbo la Tanganyika barabara nyingi zimeharibika ikiwemo barabara ya Ikola - Isengule ambapo daraja limekatika. Ni lini Serikali itaenda kurejesha miundombinu ikiwemo hiyo barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari tumeshatoa maelekezo ya jumla na tayari tumeshatenga bajeti ya kuanza kurudishia miundombinu

iliyoharibiwa na mvua, ambapo ni maeneo mengi nchini yaliathirika na mvua. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso pamoja na wananchi wa jimbo lake kwamba tutaendelea kutenga bajeti ili kuhakikisha miundombinu hiyo tunairejesha iendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko mwishoni mwa mvua za masika, kwa hiyo, tunataenda kurekebisha barabara hizi ili zisisombwe tena na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Kakoso na wananchi wake kwamba tutaendelea kujenga barabara hiyo na kuitengea bajeti ili kuweza kurekebisha miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fagason Nkingwa, swali la nyongeza.

MHE. FAGASON A. NKINGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niulize swali dogo la nyongeza. Jimbo langu la Mbogwe katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 – 2030 imeahidi kujenga kiwango cha lami kilometa 102, lakini zipo barabara, Barabara ya Ivung'wa – Ushirika – Shibutwe ambayo ni mbovu sasa mpaka sasa hivi. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Aron Nkingwa Fagasoni, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe ambaye tunapakana katika majimbo aliyoyataja, na barabara aliyoitaja ikitoka kwake inaingia Jimbo la Busanda. Kwa hiyo, ninaifahamu vizuri na tumeitumia sana kipindi cha kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Fagasoni kuwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyoahidi

tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kuhakikisha barabara hizi tunazirekebisha na tunaweka mawasiliano katika majimbo haya ili sasa anapoanza kuja kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wake aje kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Aron na wananchi wa Jimbo la Mbogwe ninawahakikishia kwamba, tutaendelea kutoa ushirikiano wa dhati *TARURA* kuendelea kurekebisha barabara hii, na tayari wameshawasilisha andiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbwilo Kapunda, swali la nyongeza.

MHE. BAZILIO K. MBWILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Barabara pekee inayounganisha vijiji ndani ya Kata ya Swaila kuanzia Kasu – Swaila yenyewe – Majengo – Ndyele – Itindi hadi Centre Makufi ni moja ya barabara zilizoathirika sana na hii mvua ambayo imemalizia. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kuzirekebisha barabara hizi ambavyo kama nilivyosema ndiyo barabara pekee inayoviunganisha vijiji hivi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunakiri kama nilivyojibu awali kwamba, kweli barabara zetu ziliathirika sana na mvua iliyoendelea kunyesha kwa kiwango kikubwa, lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninamwelekeza tu Meneja wa *TARURA* Wilaya, kwanza aipitie barabara hii na kama alivyoisema Mheshimiwa Mbunge ni muhimu na inatumika na maeneo mengi katika jimbo lake. Kwa hiyo, Meneja wa *TARURA* Wilaya aende akafanye tathmini na atuwasilishie andiko rasmi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tuitengee bajeti ya dharura kwenda kurekebisha barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Kata ya Vingunguti kuna barabara inayotoka Vingunguti kwenda Kijiwe Samli yenye ukubwa wa kilometa 0.55. Ni barabara mbovu kwa muda mrefu na Serikali imekuwa ikiahidi kuijenga, kitendo ambacho kinasababisha wananchi kushindwa kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kufahamu leo, nini kauli ya Serikali kuhusiana na lini hii barabara itajengwa ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia miundombinu hii katika Jimbo lake la Segerea. Pili, Mheshimiwa Kaiza amepokea ugeni mwingi, nami nilikwenda katika jimbo lake, nimepita barabara hiyo aliyoitaja kwa ajili ya kukagua na kuweka msisitizo katika maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwelekeza tu Mkurugenzi pamoja na Meneja wa *TARURA* Wilaya atuletee andiko la barabara hii na *commitment* kwamba lini tunakwenda kuijenga. Nami nitakaa na Mheshimiwa Kaiza, nimhakikishie ya kwamba barabara hiyo inakwenda kujengwa na tunaitekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Isaya Moses Mngurumi, Mbunge wa Kongwa sasa aulize swali lake.

Na. 452

Hitaji la Madawati – Kongwa

MHE. JESCA Y. MBOGO K.n.y. MHE. ISAYA M. MNGURUMI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza na kusambaza madawati katika shule za Jimbo la Kongwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Isaya Moses Mngurumi, Mbunge wa Jimbo la Kongwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina jumla ya shule za msingi 133 na sekondari 45, ambapo mahitaji ya madawati kwa shule za msingi ni 26,820 na yaliyopo ni madawati 20,621 na upungufu ni madawati 6,199, sawa na 23.1%. Mahitaji ya seti za viti na meza kwa shule za sekondari ni 19,167 na zilizopo 18,524 na upungufu 643 sawa na asilimia tatu nukta nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango wa kuhakikisha kuwa madawati yatatosheleza mahitaji ya shule za Jimbo la Kongwa. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Halmashauri ya Kongwa kupitia mapato ya ndani imetoa shilingi milioni 28.92 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 445 na seti za viti na meza 54. Aidha, mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 33.25 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 475 na seti 320 za viti na meza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na kuhakikisha kuwa ujenzi wa madarasa mapya unaambatana na ununuzi wa madawati 15 au seti 40 za viti na meza kwa kila darasa linalojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa ninaomba utaje jina lako.

MHE. JESCA Y. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaitwa Mheshimiwa Jesca Mbogo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther...

MHE. JESCA Y. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Jesca Mbogo.

NAIBU SPIKA: Jesca! Mheshimiwa Jesca Swali la nyongeza.

MHE. JESCA Y. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025, iliahidi kujenga vyumba 200 vya madarasa. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza agizo hilo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshazielekeza halmashauri zetu zote 184 pamoja na Jimbo la Kongwa kufanya tathmini ya maoteo na kuhakikisha kwamba zile fedha za mapato ya ndani tunazielekeza kwenye kujenga madarasa na kuyakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi tunaendelea kutekeleza katika kujenga madarasa hayo ili watoto wetu waweze kupata sehemu salama na tulivu ya kujifunzia. Hii inaendana na ile sera ya elimu ambayo tunakwenda kubadilisha kabisa mfumo wetu kuelekea kwenye madarasa 10 elimu ya lazima. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha tunakamilisha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba mwakani kama nchi tunategemea kuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanaojiunga kidato cha kwanza kutokana na mabadiliko ya mitaala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa ambao tunatoa malighafi nyingi za utengenezaji wa madawati, na kutokana na kwamba Njombe utazalisha kwa bei nafuu na ya chini, na kuweza kusambaza kwenye sehemu kubwa ya nchi yetu, na kwa kuwa, kutakuwa na uhitaji mkubwa wa madawati, ni upi mkakati wa Serikali kutumia viwanda vilivyoko ndani ya Mkoa wa Njombe na Ndani ya Mkoa wa Iringa, na hususan *VETA* zilizoko huko ili kuzalisha madawati mengi yatakayoweza kusabazwa nchi nzima, kusaidia nchi yetu kuwa na madawati? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyoeleza na nimefanya ziara katika jimbo lake, nilifika mpaka kule Makete nimeona kabisa uwekezaji mkubwa wa viwanda vilivyoko kule ndani, na swali hili ameleta kimkakati. Huyu ni mchumi, kwa hiyo, anataka aone namna gani viwanda vile vinachagizwa kulingana na fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Sanga, tutakaa mimi na yeye pamoja ili kuweza kuielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuona namna gani bora ya kupata madawati, rasilimali zile kuzisambaza nchi nzima ili kuweza kuweka ustaarabu kwa watoto wetu katika kujisomea wakiwa wamekaa kwenye viti vya kisasa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado tunayo nafasi ya mimi na Mheshimiwa Sanga kukaa kuona namna gani tunaweza kuelekeza nguvu katika maeneo hayo aliyoyataja ili kuhakikisha

kwamba fedha inarudi kwa wananchi na kuchagiza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Jimbo la Same Mashariki ambalo lina shule za msingi 89, karibu zote zina matatizo ya madawati, na nikiangalia Halmashauri ya Wilaya ya Same haina mpango wowote wa kutafuta madawati kwa ajili ya shule za msingi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mara ya tano ninauliza hili swali humu ndani, leo Mheshimiwa Waziri, ananipa jibu gani la uhakika kabisa kuhusu madawati katika shule za msingi, Jimbo la Same Mashariki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ipo tayari kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu, tunaweka madawati katika madarasa yote na katika shule ambazo amezitaja. Kwa hiyo, tutaketi mimi na Mheshimiwa Mbunge ili tuone nilivyowaelekeza wataalamu wetu katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhakikisha kwamba tunaangalia idadi sawa kabisa ya madawati kuendana na wanafunzi wetu ili kupata maeneo salama ya kujifunzia na kuweza kupata elimu bora kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la madawati linaonekana ni tatizo la nchi nzima

hasa kwenye shule za msingi, na bahati nzuri tumejaaliwa misitu na kuna muda Serikali inatoa vibali kwa ajili ya uvunaji wa mbao, je, ni kwa nini Serikali isitoe vibali vya kuvuna mbao na halmashauri zikatengeneza madawati ya kutosha? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, amelileta kama ushauri na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumepokea kama swali dogo la nyongeza, na kama ushauri, ili kuona namna gani tunakwenda kuboresha na kuhakikisha halmashauri zetu zote zinapata madawati katika shule zetu na tuweze kuondokana na adha ya madawati nchini. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Chilombe, swali la nyongeza.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Jimbo la Tunduru Kusini lina upungufu wa madawati 2,516 na hali ya kwenye jimbo lile ni mbaya, kwani wanafunzi wengi wanakaa chini. Nini kauli ya Serikali ya kuhakikisha angalau inapunguza changamoto ile angalau kwa nusu? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumekuwa tukielekeza Wakurugenzi, Wakuu wetu wa Wilaya kupitia wadau mbalimbali katika maeneo yetu ya halmashauri kuendelea ku-*mobilize resources* ili kuona namna gani tunaweza kukamilisha madawati katika majengo yote ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuchakata taarifa, kuangalia uhitaji, na kuelekeza halmashauri zetu nchini kuendelea kutenga fedha. Pia kama alivyotoka kuuliza Mheshimiwa Dkt.

Mnzava, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI itaendelea kuona namna gani itatenga bajeti kuzisaidia halmashauri zile zenye mapato madogo, na kuona namna gani tunaboresha na kuweka madawati katika madarasa yetu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Kunti Majala. *(Makofi)*

MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Kwa niaba ya Mheshimiwa Silivestry Koka, ninaomba sasa swali lake la msingi liweze kupata majibu ya Serikali.

NAIBU SPIKA: Taja swali Mheshimiwa. Ni Swali Na. 453, ninaomba ulitaje.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba swali langu Na. 453, lipatiwe majibu. Ninakushukuru.

Na. 453

Upanuzi wa Barabara ya Kibaha – Chalinze

MHE. KUNTI Y. MAJALA K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Je, lini Serikal itaendeleza mradi wa upanuzi wa Barabara ya Dar es salaam – Morogoro kipande cha Kibaha hadi Chalinze kuwa njia nane?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali kwa sasa ni kujenga barabara mpya ya *expressway* ya kuanzia Kibaha – Chalinze – Morogoro, yenye urefu wa kilometa 163.8 kwa utaratibu wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)*. Kwa sasa, taratibu za kumpata mwekezaji mpya wa ujenzi wa barabara hiyo zinaendelea baada ya majadiliano na mwekezaji wa awali kushindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali Barabara ya sasa ya Kibaha – Chalinze ili kuhakikisha kuwa inaendelea kupitika vizuri katika majira yote ya mwaka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili. Suala zima la majadiliano baina ya ninyi Wizara ya Ujenzi na hawa wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi kwa maana ya *TPA* yameendelea kuchukua muda mrefu na majadiliano hayo ni kuhusiana na hii barabara ya Chalinze pamoja na barabara ya kutoka Tanga – Kibirashi – Handeni mpaka kwetu Chemba – Kwamtoro – Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa majadiliano haya yataenda kukamilika na hatimaye ujenzi wa barabara hizi ziweze kuanza kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Serikali ilituahidi kutujengea barabara ya kutoka Zamahelo ambayo inapita Babayu inakwenda Makorongo mpaka Donsee. Ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *PPP* hasa kwa suala la miundombinu, ni utaratibu ambao ni mpya na hasa kwa miundombinu hii ya barabara. Ndiyo maana Serikali imekuwa iko makini sana kuhakikisha kwamba tunaingia mikataba ambayo itakuwa na tija kwa Serikali. Ndiyo maana pale ambapo tunaona hatujakubaliana na mwekezaji, tunaamua kuachana naye kwa sababu wawekezaji wako wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuhakikishia, kwa barabara hii ya Kibaha – Chalinze – Morogoro, watu ambao sasa hivi tuko nao tunajadiliana nao ni hawa watu wa *NSSF*, na kwa barabara ile ya Handeni – Kiberashi – Chemba – Kwamtoro, tayari yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, ambapo alielekeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia *TANROADS* na *TPA* wafanye makubaliano ya kuijenga hiyo barabara. Upande wa *technical* kwa maana ya *TANROADS* kwa barabara hiyo tulishakamilisha na wako sasa hivi kuona namna gani watafanya kuijenga kwa kusaidiana na wenzetu wa Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatuwezi tukasema *exactly* ni lini kwa sababu inategemea na *parameters* mbalimbali. Mpaka tukubaliane ndipo tutaanza. Ni matumaini yetu kwamba tutafanya haraka kwa sababu tunaona uhitaji mkubwa kwa barabara zote hizi mbili, ya Kibaha – Chalinze – Morogoro, lakini Handeni – Kiberashi – Chemba – Kwamtoro.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere samahani, ninaomba ukae kidogo.

Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la pili la nyongeza hujalijibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, labda kama sikumsikia vizuri.

NAIBU SPIKA: Swali linasemaje?

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Swali langu la pili lilikuwa linasema, Serikali ilituahidi kutujengea barabara ya kutoka Zamahelo – Babayu – Makorongo – Donsee, ambayo tunakuja kuunganisha na Barabara ya Kibirashi. Ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuliahidi na hiyo barabara hapo Donsee ndiyo mahali ambapo inakutana na ile barabara kubwa ambapo tulifanya usanifu wa awali. Bado hatujafanya *detail design* kwa maana ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tukishakamilisha usanifu wa kina, sasa tutakuwa tuna uwezo wa kupata gharama ya hiyo barabara na kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi iliyopita nimekaa na viongozi wa Wizara kuhusu barabara ya Bukama – Kurusanga – Mihingo na Barabara ya Mugeta – Mihingo – Siwamsimba. Barabara zote hizo zimekatika na hazipitiki. Lini sasa wataenda kukarabati barabara hizo kwa dharura? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Getere arudie hilo swali hasa majina ya hizo barabara alizozitaja. Sijamsikia vizuri.

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Getere, kaa mbali kidogo na kisemeo.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Bukama – Mbeengo na Barabara ya Mugeta – Siwamsimba

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri ninadhani umesikia, majibu sasa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara hizo sasa hivi tunaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Baada ya kuzikamilisha, tutakuwa na uwezo sasa wa kuanza kuzijenga kwa kiwango cha lami baada ya gharama kufahamika.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, swali la nyongeza.

MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Likuyufusi – Mkenda ndiyo barabara pekee ambayo inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Nchi ya Msumbiji, lakini barabara hiyo bado haijajengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro kwamba Barabara ya Likuyufusi – Mkenda ambayo inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Nchi yetu ya *Mozambique* ambayo ina kilometa kama takribani 112 ni kweli hatujaijenga kwa kiwango cha lami. Hata hivyo atakubaliana na mimi kwamba tumeshaanza mpango wa kuijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi tumeshapata mkandarasi, na anachosubiri ni kulipwa fedha ya awali za kuanzia Likuyufusi hadi eneo linaloitwa Muhukuru kilometa 60. Ndiyo barabara ambazo zilikuwa zimekwama, na tumesema kwamba hicho ndiyo kitakuwa kipaumbele chetu kuanza hizo kilometa 60 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi yupo tayari, anachosubiri ni kulipwa malipo ya awali, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante.

Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, sasa aulize swali lake.

Na. 454

Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Utegi Hadi Shirati - Rorya

MHE. JAFARI W. CHEGE aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Utegi hadi Shirati kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Utegi – Shirati – Kirongwe yenye urefu wa kilometa 56.81 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza Mika – Utegi – Shirati kilometa 40.06 na ya pili ni Shirati – Kirongwe kilometa 16.75. Kwa sehemu ya Mika – Utegi, hadi sasa jumla ya kilometa 13.06 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, taratibu za manunuzi kwa sehemu iliyobaki ya Utegi – Shirati kilometa 27 zinaendelea kwa ajili ya kumpata Mkandarasi anayekidhi vigezo baada ya zabuni za awali kushindwa kumpata Mkandarasi mwenye sifa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi, lakini nikiri tu kwa masikitiko makubwa niseme sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri, na kwa kuwa swali hili nimeuliza zaidi ya mara nne. Nyakati zote nne pamoja na leo majibu yamekuwa tofauti ndani ya Bunge hili lakini tarehe 28/5/2025, Makamu wa Rais, akiwa Katibu Mkuu wa Chama changu cha Mapinduzi, kwenye mkutano wa hadhara pale Shirati, alimpigia Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Waziri akaahidi toka mwaka 2025 kwamba ndani ya wiki mbili mkandarasi atakuwa *site* kwa ajili ya ujenzi wa lami kwa barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo majibu yamekuwa tofauti na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwenye mkutano ule wa hadhara kwa wananchi wale, lakini yamekuwa tofauti kwa mara nne tofauti namna ambavyo nimeuliza swali kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani kwa muktadha, kwa kuwa wananchi wana hamu kubwa na barabara hii, ninaomba kwa heshima kubwa kama Mheshimiwa Naibu Waziri ataridhia, mimi, yeye, Mheshimiwa Waziri, pamoja na wataalamu baada ya kipindi cha maswali na majibu tukae ili nipate jibu sahihi na wananchi wajue jibu sahihi la muktadha wa barabara yao kwa masilahi mapana ya wananchi wa Rorya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya kipindi hiki mtakutana na Mheshimiwa Mbunge mlijadili jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Bariadi – Nguliati – Kasoli – Salama - Magu inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu na yale Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hii muhimu, siyo kwa uchumi tu, lakini kwa kuokoa wagonjwa mahututi wanaosafirishwa kwenda kwenye Hospitali ya Kanda ya Bugando? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, tunavyoongea sasa hivi tupo tunaifanyia usanifu na wakati tunaendelea na usanifu lakini atakubaliana na mimi kulikuwa na changamoto kubwa sana katika Daraja la Sukuma ambalo lipo kwenye hatua nzuri sana tunalijenga ili kuondoa changamoto iliyokuwepo lakini baada ya kukamilisha usanifu ambayo tunaendelea ni kama kilometa 78. Sasa tutakuwa na nafasi ya kuunganisha Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Mwanza pale Magu kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, swali la nyongeza.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Nyakanga kwenda Rung'abure ndiyo barabara ambayo ni fupi inayounganisha Wilaya ya Butiama na Wilaya ya Serengeti. Barabara hii ilijengwa halafu ikasimama kwa muda mrefu na mkasema kwamba bado mnashughulikia masuala ya usanifu. Nimeuliza hili swali hapa mara mbili nikajibiwa kwamba itakuwa kwenye bajeti mwaka huu. Nilitaka kujua, je, barabara hiyo mwaka huu ipo kwenye mpango wa kuanzwa kujengwa kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tumepitishiwa bajeti yetu wiki iliyopita, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kile ambacho tumekiandika kwenye kitabu ndicho tutakachokwenda kukitekeleza ikiwa ni pamoja na hiyo barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, labda baada ya hapa pia tunaweza tukakaa, tukakubaliana hasa angetaka tuanzie wapi hata kama ni kwa awamu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Barabara ya *keep left Mogabiri* ni muhimu sana

kwa uchumi wa Wilaya ya Tarime, Serengeti na Mkoa wa Mara kwa ujumla; pia kijamii ni barabara ambayo ni muhimu sana lakini imekuwa ikisababisha ajali nyingi, ulemavu na hata vifo. Nimeuliza swali hili mara nyingi sana hapa, na kwa kuwa mkandarasi amesha-*raise certificate* ya shilingi biloni 7.99, ni lini sasa Serikali itapeleka hizi fedha ili mkandarasi amalizie kile kipande cha kilometa 9.3? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara tayari ina mkandarasi na barabara hii kama tulivyosema ni zile ambazo zinakwenda kupewa kipaumbele. Tunakiri bado tulikuwa tunadaiwa na mkandarasi na ndiyo barabara ambazo tunavyoanza utekelezaji zitakuwa za kwanza kulipa wakandarasi ili waendelee na kazi ambayo ilikuwa imesimama, ikiwa ni pamoja na hiyo barabara ya Mheshimiwa ambayo ameitaja ya Mogabiri - Nyamongo kwenda Serengeti, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Igawa - Rujewa, Madibira ni ya muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Mbarali, na hiyo barabara imo kwenye ilani zilizopita. Je, ni lini barabara hiyo itakamilika ujenzi wa kiwango cha lami? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hii ni barabara ambayo inaunganisha Mji wa Igawa – Rujewa, Madibira hadi Mafinga tutaanza kuijenga kwa awamu ambapo maelekezo ilikuwa ni kuanzia Mafinga - Madibira kuja Rujewa na ipo kwenye mpango wa kuanza ujenzi walau kuanzia pale Mafinga - Kinyanambo A kilometa 10.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 455

Fidia kwa Wananchi Wanaopitiwa na Mradi wa Barabara ya Bulambi - Kisorya

MHE. KANGI A. LUGOLA aliuliza:-

Je, lini wananchi walioathiriwa na ujenzi wa Barabara ya Bulamba – Kisorya watalipwa fidia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Bulamba – Kisorya yenye urefu wa kilometa 51 ni sehemu ya Barabara ya Nyamuswa – Bulamba – Kisorya yenye urefu wa kilometa 108.4. Wakati wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara hii jumla ya wananchi 833 waliathiriwa na ujenzi huo na walilipwa fidia yenye jumla ya shilingi 2,384,226,323 kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kangi Lugola, swali la nyongeza.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo majibu ya Serikali, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majibu haya yana dalili na jaribio la kuwakana wananchi wa Mwibara wapatao 1,575 wa Vijiji vya Buzimbwe, Bulamba, Kasuguti, Mahyoro, Nyamitwebili Kasahunga, Namibu, Bunele, Nambaza, Nansimo, Mwitende,

Masahunga na Museni kwamba hawaidai Serikali fidia yoyote. Ni kwa nini Serikali isije Mwibara kuonana na hawa wananchi ili waweze kuweka mambo sawa, kwa sababu majibu haya yanaonesha hakuna mtu hata mmoja anayedai fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Sheria hii Na.13 ya Mwaka 2007 iliyoongeza meta ziwe 30 kila upande wa barabara na kwa kuwa vijijini inaonekana sheria hii haitekelezeki, Serikali inachukua eneo ambalo halitumiki kwa sasa. Serikali inaonaje ikirekebisha sheria hii ili wananchi ambao zaidi ya miaka 12 wamekaa bila kuendeleza maeneo yao ili waweze kuyaendeleza maeneo yao ili kizazi kijacho kitakapokuwa kimejipanga kuwa na uwezo wa kulipa fidia, basi walete tena sheria nyingine ya kuongeza upana wa barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara, tupo tayari kwenda katika vijiji alivyovitaja kuongea na hao wananchi na kuwaeleza nini Serikali inategemea kufanya kuhusu hayo madai yao ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapendekezo yake ya kuhusu sheria, hii sheria ilipitishwa na Bunge hili kuongeza upana wa barabara ikiwa ni sehemu ambayo tunaamini kwa sasa pengine barabara ya njia mbili. Sasa hivi tunaongelea njia sita ili baadaye tusije tukaingia kwenye gharama kubwa ya kufidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane naye pia kwamba utekelezaji wa sheria hii, kwa sababu ilikuwa meta 45 upana wa barabara na sasa tumekwenda 60, ni kweli kwamba kulipa hiyo fidia maeneo mengi imekuwa ni gharama kubwa na Serikali sasa hivi kupitia Wizara ya Ujenzi tunajaribu kufanya tathmini tuone kama maeneo yale ambayo kweli tunayahitaji yanaweza yakagharimu kiasi gani, na yale ambayo tunaamini hayawezi kuhitajika kwa sasa yapo kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishapima tutawakilisha kujadili Serikalini na tuone kama tunaweza tukaleta maombi ya kufanya

mabadiliko yoyote ya kisheria kuhusu maeneo mengi ambayo wananchi (ambao kweli ni wengi sasa hivi) wameshindwa kuendeleza maeneo yao ambayo kisheria wanahitaji kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pamoja na wananchi ambao wapo kwenye Jimbo la Mwibara ambao wapo kwenye meta 7.5 ambao hatujawaondoa, lakini sasa hivi wanahesabika kama wapo kwenye hifadhi lakini ni kweli kwamba wanastahili kulipwa. Ndiyo maana wana alama za kijani lakini tu ni kwamba hatujawabomolea lakini wapo kwenye hifadhi ya barabara. Kwa hiyo, wana haki kwenye hizo meta 7.5 pande zote mbili, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba maswali mafupi.

Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali la nyongeza.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kutujengea barabara nzuri ya lami kutokea Kabingo kwenda Kasulu hadi Buhigwe. Sasa kwenye Kata ya Kasanda eneo la Kewe kuna daraja lilijengwa pale likaelekezwa kwenye makazi ya watu na mvua zikinyesha imekuwa ikisababisha korongo kubwa ambalo ni hatari kwa watoto, ni hatari kwa wananchi wanaoishi maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkandarasi bado yupo, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha eneo lile linadhibitiwa ili kuweka hali ya usalama katika maeneo ya Kasanda? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninadhani ni suala tu la utekelezaji, ninaomba kupitia Bunge hili nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Kigoma aende eneo hilo linaloitwa Kasanda na ikiwezekana awasiliane na Mheshimiwa Mbunge ili kwa kuwa mkandarasi yupo kule bado, waweze kurekebisha na kujenga mfereji ambao hautaathiri makazi ya wananchi ambao hatutamani barabara zilizojengwa ziwe ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Kigoma, kwanza aende eneo la Kasanda na aweze kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili aweze kupata maelekezo sahihi ya nini kinatakiwa kufanyika katika hilo eneo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakulu Kakulu, swali la nyongeza.

MHE. KAKULU B. KAKULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Umuhimu wa barabara ya Kongowe kwenda Kivukoni, kwa sababu ni barabara inayounganisha majimbo matatu ya uchaguzi: Jimbo la Mbagala, Jimbo la Mkuranga na Jimbo la Kigamboni pamoja na kuunganisha wilaya tatu; Wilaya ya Kigamboni, Wilaya ya Mkuranga na Wilaya ya Temeke, je, ni lini Serikali itafanya upanuzi wa ile barabara kwa kuzingatia umuhimu wa viwanda vinavyojengwa Mkuranga pamoja na kule Kigamboni – Kisarawe II.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli barabara hiyo ni muhimu na ndiyo maana ipo kwenye mpango kwanza wa kufanyiwa marekebisho kwa maana ya kuipanua. Pia kule ambapo barabara inakutana ya Kongowe pale kwenda Mjimwema, tunajenga *interchange* kama tulivyosema ili tu kuhakikisha kwamba hilo eneo kwa sababu tunategemea litakuwa na magari mengi, kusiwe na changamoto hata ya kupishana kwa magari ya kwenda Kusini na kwenda Kivukoni. Kwa hiyo, Serikali inalifahamu hilo na tayari tumeshaanza kulifanyia kazi.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Jesca Yuda Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 456

Ujenzi wa Barabara ya Narco – Dosidosi - Kiteto

MHE. JESCA Y. MBOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Narco - Dosidosi - Kiteto yenye urefu wa Km 72 kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Yuda Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Narco – Dosidosi – Kiteto yenye urefu wa kilometa 72 ni sehemu ya barabara ya Mkoa wa Arusha – Kibaya hadi Kongwa yenye urefu wa kilometa 434 inayounganisha mikoa ya Arusha, Manyara na Dodoma. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza inahusisha ujenzi wa sehemu ya Mbauda – Losinyai kilometa 31.8, JKT Oljoro kilometa mbili na Moshono – Losinyai kilometa 36.2 ambapo kazi za ujenzi zimeanza sehemu ya Mbauda – Losinyai. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jesca Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. JESCA Y. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, ingawa wameanza kujenga kuanzia Arusha. Kwa nini Serikali isianzie Kongwa kwenda Arusha?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nimwulize swali la nyongeza. Kutokana na athari za mvua za masika, barabara ya Pandambili – Lenjuru - Kiteto hadi Kwayaki zimeathirika sana, na barabara hizi wakulima wanazitegemea sana kwa ajili ya kupeleka mazao yao pale Kibaigwa. Je, Serikali ina mpango gani na barabara hizi na lini itaanza kuzitengeneza? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara

zote ambazo kimsingi zilikuwa zimeharibika kipindi cha mvua, zote tunakwenda kuzikarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mvua kukatika, kwanza tutazikarabati, halafu tumezitengea fedha kwa ajili yakuzirejesha katika hali yake ya kawaida iliyokuwepo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kupitia Meneja wa Mkoa wa Dodoma, hizo barabara zote zinakwenda kukarabatiwa ili wananchi waweze kufikisha mazao yao katika masoko.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Christina Mndeme, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yustina, sijakutaja, nimemtaja Mheshimiwa Christina Mndeme. *(Kicheko)*

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiboresha miundombinu ya barabara kwa lengo la kurahisisha suala la usafiri na usafirishaji nchini, na sisi wote tunashuhudia. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa panapokuwa na changamoto ya barabara waathirika wakubwa ni wanawake na Watoto, je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Ipole mpaka Rungwa kupitia Kata za Ngoywa – Kitunda – Kiloli – Kilumbi na Kipili ili kurahisisha usafiri na usafirishaji na kuondoa changamoto wanazopata hasa wanawake na watoto katika Mkoa wa Tabora na hususan Wilaya ya Sikonge? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ya kutoka Ipole hadi Rungwa, ni barabara ambayo inaanzia Tabora – Ipole kwenda Rungwa kwenda Makongolosi. Ninakubaliana, sisi katika Wizara tunasema ni kati ya

barabara kubwa kuu ambazo bado hatujazijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa barabara hiyo aliyoitaja ya Ipole hadi Rungwa, kilometa 172 hata katika kitabu chetu cha bajeti tumeipangia bajeti kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali inaangalia uwezekano wa kupata chanzo kikubwa cha uhakika ili kuijenga hiyo barabara yote kwa maana ya Ipole – Rungwa – Makongolosi hadi Mbeya na Rungwa – Itigi hadi Mkiwa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yustina Rahhi, swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara inayotoka Babati kupitia Galapo kwenda Kibaya imeharibiwa vibaya sana na mvua. Ni upi mpango wa Serikali kukarabati barabara hiyo sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika maswali mengine ya ukarabati, tunakiri kwamba barabara nyingi kwa kweli, zimeharibika sana kufuatia mvua iliyonyesha. Kwa hiyo, tumewapa Mameneja wote wa mikoa kufanya uhakiki, tathmini na gharama zake, kwanza, kwa ajili ya kuzijenga kwa utaratibu wa dharura ili ziweze kupitika, na baada ya hapo, kwa kuwa bajeti imepitishwa, kwenda kwenye utaratibu wa kawaida wa kuzitengeneza kurudi katika hali yake ya kwanza. Cha kwanza tunataka zipitike, cha pili kuzirudisha kwenye utaratibu wake wa kawaida kulingana na bajeti ambayo mmetupitishia, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yohana Msita, swali la nyongeza.

MHE. YOHANA S. MSITA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeendelea na ujenzi

wa Barabara ya kutoka Doroto mpaka Itigi kwa kiwango cha lami. Tuna kipande cha Barabara kutoka Itigi mpaka Mkiwa ambacho kwa kweli kimekuwa kina adha kubwa kwa wananchi wanaotoka Makao Makuu ya Mkoa wa Singida, wanalazimika kupita Manyoni kuja Itigi na wanaotoka Itigi inabidi wapite Manyoni kuelekea Singida, kitu ambacho kimesababisha adha kubwa kwa sababu mkandarasi yupo *site*, Serikali haijapeleka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha ujenzi wa kiwango cha lami kwenye Barabara ya Itigi kuelekea Mkiwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza jambo jema ni kwamba, tayari mkandarasi yupo *site*. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, muda wowote tunategemea wakandarasi wote ambao walikuwa wamekwama na wapo *site,* wameleta maombi yao kwa maana ya hati za madai, na Serikali tunaandaa malipo yao ili tuweze kuwalipa waweze kuendelea na hiyo kazi, ikiwa ni pamoja na hiyo Barabara ya Mheshimiwa Mbunge ya kutoka Mkiwa – Itigi – Manyoni na ndiyo hiyo barabara ambayo inaenda Rungwa - Makongolosi, barabara kuu, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Mahenje – Dolezi – Hasamba – Nyimbili hadi Itumba, ni lini Serikali itaanza kuijenga kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara imefanyiwa usanifu na ni barabara ambayo inaweza pia ikatumika kama *bypass* kwa Mji wa Mlowo na Mji wa Vwawa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuijenga kwa awamu barabara hiyo, kwa kiwango cha lami ikiwa

pia, ni kupunguza msongamano mkubwa katika huo Mji Mdogo wa Mlowo na Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mbunge wa Mtwara Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 457

Upatikanaji wa Vituo vya Gesi ya *CNG* Nchini

MHE. ARIF S. PREMJI aliuliza:-

Je, upi mpango wa kuwekeza kwenye Vituo vya *CNG* baada ya kuondoa ushuru wa Sh. 382 kwa kilo ili kuhimiza matumizi ya *CNG* kwenye vyombo vya moto?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Salome Makamba, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* kwa kushirikiana na sekta binafsi, wanaendelea na ujenzi wa Vituo vya *CNG* katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa sasa kuna vituo 18 vya *CNG* vinavyofanya kazi ambavyo vipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa muda mfupi na kati unaondelea ni pamoja na Serikali, kwa kushirikiana na sekta binafsi, kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa vituo kumi vya *CNG* hapa nchini katika Mikoa ya Dar es Salaam, nane; Mtwara, kimoja; na Morogoro, kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia *TPDC* inakamilisha taratibu za ununuzi wa vituo vitano vya *CNG* vinavyohamishika *(CNG Mobile station),* ambapo kati ya hivyo, vituo viwili vitawekwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kimoja, Mkoa wa Morogoro, maeneo ya Chuo cha Ardhi; na viwili Mkoa wa Dodoma, maeneo ya Mji wa Serikali, Mtumba, na Chako ni Chako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na majadiliano na kampuni binafsi sita kwa ajili ya uendelezaji wa miradi midogo ya kubadili gesi asilia kuwa kimiminika *(Mini LNG)* na kusafirishwa kwa magari maalum kwenda mikoa mbalimbali nchini ambayo haijafikiwa na miundombinu ya mabomba ya gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mikoa iliyopitiwa na bomba la gesi, ikiwemo Mtwara, Serikali imejielekeza zaidi katika kusambaza gesi majumbani na kwenye taasisi, kupitia mabomba ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wananufaika na rasilimali hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, swali la nyongeza.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kutoa majibu mazuri sana na yametia faraja. Sasa Serikali inatoa dhamana gani kwa wawekezaji wa vituo vya *CNG,* ili pasije pakatokea uhaba wa gesi, na ukizingatia kwamba nishati ya umeme pia inategemea malighafi ya gesi na 2030 tumeweka lengo la Megawati 8,000? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Nishati ya gesi ya *CNG* ni ya bei nafuu. Tumeshuhudia sasahivi vyombo vingi vya moto vinabadilishwa mfumo kuwekwa kwenye gesi, lakini cha kustaajabisha hatuoni unafuu kwenye nauli wala kwenye bidhaa za sokoni. Je, Wizara inaratibu vipi na mamlaka husika, ili kuleta manufaa na urahisi katika bei na nauli hizo kwa mwananchi wa kawaida? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini, kwani amekuwa anafuatilia kwa karibu kuhusiana na manufaa ya gesi kwenye Mikoa ya Kusini, hasa jimbo lake la Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali, kupitia *TPDC,* inaendelea na utafiti na uchimbaji wa gesi kule *Mnazi Bay*, Songo Songo Magharibi, Lindi, Mtwara, Mtorya na tunaendelea na utafiti. Kwa sasa hatuna upungufu wa gesi nchini, gesi iliyopo inatosheleza mahitaji yaliyopo. Kwa hiyo, ninamtoa wasiwasi na tunaendelea kuwahimiza wawekezaji wa Vituo vya *CNG* nchini waje kuwekeza kwa sababu, mahitaji bado ni makubwa sana na hii ni fursa kwa Watanzania kuweza kutumia magari ya gesi badala ya kutumia mafuta peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli, ukilinganisha na mafuta, matumizi ya gesi yana gharama nafuu zaidi na watu wanapotumia gesi kwenye magari yao inawaraihisishia na kuwapunguzia gharama kubwa ambayo inatumika kwenye mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu, kupitia *LATRA,* namna ambavyo wanatoa bei za nauli, *factors* ni nyingi. Kuna habari ya gharama za vipuri, nishati inayotumika, gharama za uendeshaji na Kamati huwa inakaa kwa ajili ya kujadili. Kwa sasa magari ambayo yanatumia gesi siyo mengi kwa kiasi ambacho kinaweza kikaathiri au kikachagiza kikokotoo kidogo zaidi cha nauli. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, na mimi naendelea kuwahimiza wananchi, tubadilishe magari yetu yaende kwenye mfumo wa gesi ili kuweza kutumia nishati hii, ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki sisi Watanzania, na ni nafuu zaidi ukilinganisha na gharama ya mafuta, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Motto, swali la nyongeza.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Maono ya Serikali ya Dira 2050 ni kuhakikisha tunatumia gesi nchini kote kwa kutambua kuwa, katika maeneo mengi hapa nchini

tuna gesi, hususan Mkoa wa Mtwara. Je, akiba ya gesi tuliyonayo itatimiza maono ya Dira 2050?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Asha Motto kwa swali lake zuri na ninampongeza pia maana amekuwa anatoa ushirikiano kwetu sisi kama Wizara ya Nishati kwa kutushauri namna ya kwenda vizuri kwenye matumizi ya gesi, kwa ajili ya kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Asha kwamba sasa hivi, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, hatuna uhaba wa gesi kwa ajili ya matumizi ya magari na majumbani. Kwa tafiti zinazoendelea kufanyika katika visima vyetu vya *Mnazi Bay* na vingine vya Songo Songo, Songo Songo Magharibi, kule Mtorya, Lindi na Mtwara, vinatuhakikishia kwamba, nishati ya gesi ambayo tutaipata itatufikisha kwenye Dira 2050, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tumefikia mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka kwa upande wa Serikali. Tunayo matangazo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Tuanze na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni wafuatao; Mheshimiwa Anthony Sanga, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu na Mheshimiwa Angelina Mabula, Waziri wa Ardhi mstaafu. Ahsante sana.

Tunaye Ndugu Nathaniel Nhonge, ambaye ni Kamishna wa Ardhi, Dkt. Sophia Kongela, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* Dkt. Lucy Shule, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri Chuo cha Ardhi Tabora, Prof. Ernest Kihanga na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

Yupo Ndugu Minja Jeremiah, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora; Ndugu Charles Saguda, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro; Ndugu Stella Tullo, Msajili Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Ndugu Joseph Mafuru, Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Ndugu Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba la Taifa; na Ndugu Zena Nyange, Makamu wa Rais wa Chama cha Wataalamu wa Milki Tanzania.

Tunaye pia Ndugu Grace Lubaale, *Regional Program Officer East and Horn of Africa Regional Office, UN Habitat;* Ndugu Noadi Tweve, Mdau wa Sekta ya Ardhi Mkoa wa Njombe; na Ndugu Brayco Sanga, Mkuu wa Sekta ya Ardhi. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Akwilapo, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. Kwanza yupo Ndugu Grace Akwilapo, mke wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Felix Akwilapo, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Emmanuel Akwilapo, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Rose Akwilapo, dada wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Felister Akwilapo, dada wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu George Nindie, mjukuu wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Akwilapo ambao ni Viongozi kutoka Jimbo la Masasi, Mkoa wa Mtwara; Ndugu Mwenye Mchopa, Mwenyekiti wa Machifu; Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi na pia alikuwa Mbunge wa Bunge la Kumi, Jimbo la Masasi; Mheshimiwa Sospeter Nachunga, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi; na Ndugu Twahili Mayola, Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Masasi. Karibuni sana wageni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Kaspar Kaspar Mmuya, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. Kwanza tunaye Ndugu Elizabeth Mbilinyi, mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Oscar Mmuya, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; Ndugu Jescar Mmuya, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri; na Ndugu Elina Mulumba, shemeji wa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Naibu Waziri hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mmuya, ambaye ni Naibu Waziri, ni viongozi kutoka Jimboni Ruangwa. Tunaye Mheshimiwa Hassan Ngoma, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa; na Ndugu Saidi Chipenya, Chifu wa Kabila la Wamwera, Wilaya ya Ruangwa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Abubakar Ali Omari, ambaye ni Ndugu Asante Jumapili Masatu, mfanyabiashara kutoka Ilala Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Lucy Damas Simirya Kombani, kutoka Kampuni ya *First Housing Finance Tanzania Limited* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ambao ni wakulima kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, ambaye ni Ndugu Chaina Chacha kutoka Bunda Mkoani Mara. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Godwin Chitungo kutoka Kata ya Kikuyu, Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo Wanafunzi 122 na walimu 10 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya *Junior Scholar,* ya Mkoani Morogoro. Karibuni sana walimu na wanafunzi. *(Makofi)*

Tunao wajasiriamali watatu kutoka Chamwino Mkoani Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo Wajasiriamali vijana, Ndugu Jesca Nsele na Ndugu Caren Msele kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Nane Nane ya Mkoani Morogoro. karibuni sana walimu na wanafunzi kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Tunae Mhadhiri, Ndugu Rachel Yusuph kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini, Kampasi ya Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Maafisa 20 kutoka Taasisi ya *Vodacom* Kanda ya Kati, karibuni sana Bungeni wageni wetu wote. Tunawashukuru kwa kutembelea Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

NAIBU SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamuita Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo, ambaye ni Waziri wetu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, awasilishe Hotuba ya Bajeti yake ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Waziri, karibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ambayo ilichambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi,

Nyuma na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48; na Tume ya Taifa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu Namba 03; Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48; na Tume ya Taifa Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu Namba 03 kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu hayo mawili kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hotuba yangu iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, ambao ni mahususi kwa ajili ya kujadili mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kipekee kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamwahidi kuwa, kwa kushirikiana na viongozi na watumishi wote wa Wizara, nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uadilifu na weledi wa hali ya juu, ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika sekta ya ardhi. Hiyo yote ni kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipatia msaidizi makini, mahiri na mchapaka kazi, Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Mbunge na Naibu Waziri ambaye amekua msaidizi mahiri katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushindi mkubwa wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Ushindi huo ni ishara ya imani kubwa waliyonayo Watanzania kutokana na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imedumisha amani, umoja, upendo na mshikamano nchini. Aidha, umeimarisha utulivu wa kisiasa na diplomasia ya uchumi na hivyo kuvutia uwekezaji katika sekta ya ardhi na uendelezaji wa milki.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa masuala makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika sekta ya ardhi kwa kipindi cha uongozi wake ni pamoja na kuwezesha ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, na hivyo kuwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023, ambayo imetoa mwelekeo mpya wa usimamizi wa ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mheshimiwa Rais ameweza maboresho ya mifumo ya *TEHAMA* na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza kwa umahiri wake katika kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. Ninamshukuru pia kwa maelekezo na miongozo yake ambayo imeendelea kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi mahiri katika kuendelea kudumisha misingi ya Muungano wetu pamoja na kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Ninamshukuru kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi. Miongoni mwa masuala yaliyotiliwa mkazo katika hotuba hiyo ni pamoja na kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati. Vilevile, kuimarisha mifumo ya *TEHAMA*. Aidha, kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia na vilevile, na kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kuendeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuboresha miundombinu ya upimaji wa ramani. Wizara imezingatia na inaendelea kutekeleza maelekezo na maagizo yanayohusu sekta ya ardhi, ili kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini, kudhibiti migogoro ya ardhi, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuifanya ardhi kuwa mtaji hai kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninawapongeza wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini; ambao kwa nyakati tofauti, wamekuwa wakisimamia na kuongoza Shughuli za Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia muhimili huu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, kwa maoni na ushauri ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu 03 kwa Mwaka 2026/2027. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na hivyo kutoa mwelekeo mpya wa utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa ninatoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ismani, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Msiba huu ulitokea tarehe 25 Machi, 2026. Hayati William Lukuvi atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika kujenga misingi ya utawala bora na maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini. Aidha, atakumbukwa kwa kuweka misingi madhubuti ya utawala na usimamizi wa sekta ya ardhi kwa kipindi alichohudumu kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2022. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kutokana na kifo cha Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, ninatoa pole kwa familia za Marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, wapo viongozi na Watanzania wenzetu waliofikwa na ajali, majanga na maafa mbalimbali yanayosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Tutumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa, rafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema Peponi. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji

wa haraka Watanzania wenzetu waliojeruhiwa, ili waweze kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii, katika mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele nane kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishwaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati;

(b) Vilevile, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji;

(c) Kuimarisha mifumo ya *TEHAMA* katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa za ardhi na uthamini;

(d) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, kwenye mabaraza ya ardhi ya nyumba ya wilaya;

(e) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(f) Kuimarisha mipaka ya Kimataifa na kuendeleza miji ya mipakani;

(g) Kuimarisha upatikanaji wa ramani ili kuwezesha uandaaji wa mipango Kitaifa na matumizi mengine; na

(h) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vilivyobainishwa vitawezesha kufikia malengo ya sekta yalioainishwa katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, Dira ya 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la Kumi na Tatu mwezi Novemba Mwaka 2025, Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano,

kuanzia mwaka 2026/2027 hadi 2030/2031, Malengo ya Maendeleo Endelevu Kuelekea mwaka 2030 na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2026/2027 kuelekea 2030/2031.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa nitoe ufafanuzi kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48 pamoja na Tume ya Taifa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu Namba 03 kwa Mwaka 2025/2026; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2026/2027. Aidha, takwimu za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026 ambazo zipo katika hotuba hii, zimeishia tarehe 15 Mei, mwaka 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 290 kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2026 Wizara imekusanya shilingi bilioni 191.90 sawa na 66.17% ya lengo. Katika mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni 300 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali, ikiwemo kuendelea kusambaza miundombinu na mifumo ya *TEHAMA* katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri, ili kurahisisha utoaji wa huduma za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kufuatilia halmashauri ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa miradi ya KKK na kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha Mahakamani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine, inaendelea kutafuta njia bora ya ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kupitia huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi hizo. Ninatoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa msingi wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati, ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufutiwa umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kupitia Bunge lako Tukufu, kuwafahamisha Watanzania wote kuwa, kutokulipa kodi ya pango la ardhi ni kosa ambalo linaweza kukufanya ukakosa sifa ya kukopesheka katika taasisi za fedha, na vilevile kukosa kugombea nafasi za uongozi ikiwemo Udiwani na Ubunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 193.44 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 53.82 zilikuwa kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 37.56 kwa ajili ya matumizi mengineyo; na shilingi bilioni 62.06 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo, shilingi bilioni 5.73 ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 56.33 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni 64.24, ambapo shilingi bilioni 60.94 zilitumika kwa ajili ya kulipa madeni, na shilingi bilioni 3.30 zilitumika kutetea maombi ya eneo la nyongeza nje ya ukanda wa kiuchumi baharini *(extended continental shelf)* yaliyowasilishwa Umoja wa Mataifa, na hivyo, kufanya bajeti ya maendeleo kuongezeka hadi shilingi bilioni 126.29 na bajeti ya Wizara kwa ujumla kufika shilingi bilioni 217.68.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 15 Mei, 2026 Wizara ilipokea shilingi bilioni 141.09, sawa na 64.82% ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 43.85 ni mishahara, shilingi bilioni 31.51 ni matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 65.74 ni kwa ajili ya utekelezajii wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilipanga kukusanya shilingi 18,000,000 kupitia kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Tume ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 16.05 sawa na 89.17% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Tume ilipanga kupokea michango ya shilingi bilioni moja kutoka kwa wadau wa kimkakati. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, shilingi milioni 417.79 zilikuwa zimepokelewa, ambayo ni sawa na 41.78% ya lengo. Kwa mwaka 2026/2027 Tume imepanga kukusanya shilingi 18,000,000 kutokana

na kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Aidha, juhudi za kuhamasisha wadau wa kimkakati kuchangia shilingi milioni 500 kwa ajili ya kugharamia shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni 10.71 kwa ajili ya kugharamia miradi ya upangaji wa matumizi ya ardhi. Aidha, wakati wa utekelezaji wa bajeti, Tume iliongezewa shilingi bilioni mbili, hivyo, jumla ya bajeti ilikuwa shilingi bilioni 12.71. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.71 ni mshahara, shilingi bilioni 3.48 ni matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 4.52 ni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upangaji wa matumizi ya ardhi.

Hadi tarehe 15 Mei, 2026 Tume imepokea shilingi bilioni 10.33 ambayo ni sawa na 81.27%. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.58 ni mishahara, shilingi bilioni 2.23 ni matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 4.52 ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa fedha ambazo zimeongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kuandaa na kusajili hatimiliki 500,000, hati za hakimiliki ya kimila 520,000, hati za sehemu ya jengo 1,000, vyeti vya ardhi ya Kijiji 100 na miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000. Hadi tarehe 15 Mei, 2026 Wizara imeandaa na kusajili hatimiliki 107,683 ambayo ni sawa na 21.54% ya lengo. Hati za hakimiliki ya kimila 99,762 sawa na 19.19% ya lengo, vyeti vya ardhi ya kijiji 148 sawa na 148% ya lengo na hati za sehemu ya jengo 914 sawa na 91.4% ya lengo. Aidha, jumla ya miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 136,681 zimesajiliwa sawa na 137.68% ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kuandaa na kusajili hatimiliki 200,000, hati za hakimiliki 300,000, vyeti vya ardhi ya Kijiji 60, hati za sehemu ya jengo 1,000

na miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000. Ninatoa wito kwa wananchi wahakikishe wanamiliki ardhi zao kisheria ili kuepuka migogoro na kuwawezesha kutumia ardhi kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kiuchumi na yale ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria za ardhi zinamtaka kila mmiliki kuendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki, ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi. Katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba 1,000 ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2026 jumla ya viwanja na mashamba 2,503 yalikuwa yameshakaguliwa. Ukaguzi huo umebaini kuwa wamiliki 1,571 wa viwanja na mashamba walizingatia masharti ya milki, lakini wamiliki 932 wa viwanja na mashamba walikiuka masharti ya umiliki. Wizara imechukua hatua za kisheria kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki, ambapo milki za mashamba na viwanja 15 zimefutwa na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wamiliki 917.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba 1,000 ili kubaini hali ya uendelezaji na kuchukua hatua stahiki. Ninatoa rai kwa wamiliki wa ardhi kuendeleza milki zao kwa mujibu wa masharti ya umiliki wao, ili kuepuka Serikali kubatilisha milki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutenga ardhi kupitia mpango kabambe ulioandaliwa ili kuhakikisha kuwa kuna ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kugawa hekta 5,000 kwa wawekezaji. Hadi tarehe 15 Mei, 2026 Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi imepokea na kuidhinisha maombi 333 ya ardhi ya wawekezaji yenye ukubwa wa hekta 45,371.24. Katika mwaka huu wa 2026/2027 Wizara imepanga kutenga na kugawa ardhi yenye ukubwa wa hekta 5,000 kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma ya Serikali ya kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini, Wizara imeimarisha utoaji wa huduma kwenye Mamlaka ya Uwekezaji wa Maeneo maalum ya Kiuchumi Tanzania *(TISEZA),* kwa kuanzisha ofisi maalum ya ardhi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeimarisha utoaji wa huduma za ardhi kwenye mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza ambayo ina mahitaji makubwa ya huduma. Mikoa hiyo imekuwa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wawili, hatua ambayo itaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kuwafikia wananchi karibu zaidi na maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono na dhamira yake ya kuhakikisha wawekezaji na wananchi wanapata huduma bora za ardhi kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo kwa migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali hapa nchini, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa mkakati wa pamoja wa kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelekezo hayo, Serikali imeandaa na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migogoro ya Ardhi Nchini. Mkakati huo unahusisha wadau na makundi yote muhimu hususan wakulima, wafugaji, wawekezaji na mamlaka za hifadhi, ili kuhakikisha changamoto ya migogoro ya ardhi inapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha migogoro ya ardhi inadhibitiwa, hivyo kuwawezesha watumiaji wa ardhi kufanya kazi zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kutatua migogoro ya ardhi 3,000. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, jumla ya migogoro ya ardhi 5,573 imetatuliwa ambapo kati ya hiyo, migogoro 3,183 imetatuliwa kupitia Kliniki za Ardhi, na migogoro 2,390 imetatuliwa kupitia utaratibu wa kawaida wa kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kushughulikia migogoro 4,000 kiutawala. Ninatoa rai kwa viongozi, watumishi na wananchi kwa ujumla kuzingatia sheria za ardhi, kanuni na miongozo ili kuepuka kuanzisha migogoro mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu ukamilishaji wa kazi zilizobaki za utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri, kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika vijiji na mitaa 975. Maamuzi yameendelea kutekelezwa ikiwemo kurejesha ardhi kwa wananchi ambapo jumla ya ekari milioni 3.13 zimerejeshwa, na shilingi bilioni 95.27 zimelipwa kwa wananchi waliostahili kulipwa fidia katika maeneo 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mpango kazi kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobaki umeandaliwa na unaendelea kutekelezwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu pia inasimamia uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini zipatazo 54,000, kukamilisha uandaaji wa vitalu vya thamani ya ardhi katika mikoa saba na kuendelea na zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa 26. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini 57,293 ambayo ni sawa na 106.10% ya lengo ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni 27,211 na majedwali ya fidia yenye wafidiwa 30,082 pia yamekamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, malalamiko ya uthamini 99 yalipokelewa na kushughulikiwa kiutawala. Vilevile, zoezi la

kuhuisha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi na mazao limefanyika katika mikoa yote 26 nchini na uhuishaji wa viwango vya thamani ya majengo umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuidhinisha taarifa za uthamini 50,000; kushughulikia malalamiko 100 yatokanayo na uthamini; na kuhuisha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi, mazao na majengo katika mikoa 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuanzisha mabaraza mapya katika wilaya mbalimbali nchini ambayo yamekuwa yakisikiliza na kuamua mashauri ya ardhi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuanzisha mabaraza mapya 24 na kushughulikia mashauri 16,000. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2026, Wizara imeanzisha Mabaraza mapya sita na hivyo kuwa na jumla ya mabaraza 121 yanayofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mashauri 23,426 yamesikilizwa ambapo kati ya hayo, mashauri 12,644 yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi ilhali mashauri 10,782 yanaendelea kushughulikiwa. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaanzisha mabaraza mapya 18 ili kufikia lengo la kuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya zote 139 zilizopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kushughulikia mashauri 10,782 yaliyobaki na yale mengine ambayo yatafunguliwa. Ninatoa wito kwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kuzingatia weledi, uadilifu na misingi ya utoaji haki katika kuamua mashauri ya ardhi ili kujenga imani kwa wananchi wanaopata huduma katika mabaraza hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kusimika miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini, kusambaza Mfumo wa *e-Ardhi*, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imesambaza vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.20 katika mikoa na halmashauri zote nchini. Aidha, huduma za uthamini na usajili wa nyaraka zinatolewa kupitia Mfumo wa *e-Ardhi* katika mikoa yote nchini, huku huduma za utawala wa ardhi zikitolewa kupitia mfumo huo katika mikoa mitano ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tanga na Mwanza, pamoja na baadhi ya halmashauri za mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Mtwara, Pwani na Ruvuma. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na juhudi za kuhakikisha huduma zote zinapatikana kupitia mfumo huo katika ofisi zote za ardhi za mikoa na halmashauri hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imerahisisha huduma za malipo ikiwa ni pamoja na wananchi kutumiwa au kutengeneza ankara zao bila kulazimika kufika kwenye Ofisi za Ardhi. Mathalani, kodi ya pango la ardhi inaweza kulipwa wakati wowote na mahali popote kupitia simu, mawakala au benki ambapo kwa sasa namba ya malipo inakuwa ni ya kudumu. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wananchi 127,449 wamejengewa uwezo na kujisajili na wengine tayari wameomba na kuhudumiwa kupitia mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa wananchi kuendelea kufuatilia matangazo yanayotolewa katika vyombo mbalimbali vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara ili kujifunza kuhusu huduma za Sekta ya Ardhi zinazotolewa kupitia Mfumo wa *e-Ardhi*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji ardhi huwezesha kuwa na mipaka inayotambuliwa kisheria na hivyo kuongeza usalama wa umiliki. Pia, thamani ya ardhi inaongezeka na vilevile kuepusha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi. Wizara inaendelea na jukumu lake la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa viwanja 500,000 na mashamba 500. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, jumla ya viwanja 193,317 na mashamba 515 yamepimwa na kuidhinishwa ambayo ni sawa na 38.66% na 103.0% mtawalia. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na dhamira yake ya kupima na kuidhinisha viwanja 500,000 na mashamba 500 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mipaka ya kiutawala. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji 100. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, mipaka ya vijiji 54 imehakikiwa na kuhuishwa na vijiji 189 vimepimwa na hivyo kufanya vijiji vilivyopimwa kufikia 11,996 kati ya vijiji 12,333 vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na wadau wa maendeleo kuhakiki, kuhuisha na kupima mipaka ya vijiji 226. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya Serikali za Vijiji kuhusu kuathiriwa haki zao za ardhi baada ya kubainishwa kwa mipaka ya vijiji. Nitumie fursa hii kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuheshimu haki za ardhi za wananchi ili kuepuka kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness (TACTIC)* ambao unasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inaendelea na maandalizi ya awali ya kuandaa Mipango ya Jumla ya miji mingine 18 hapa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji, inaendelea kufuatilia uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Jumla kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuchochea maendeleo endelevu ya ukuaji wa miji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji wa Mipango ya Jumla pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa

miradi inayopangwa inazingatia mipango iliyopo. Aidha, ujenzi unaofanyika bila vibali udhibitiwe ili kuzuia ukuaji holela wa miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono maono na dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na makazi na miji ya kisasa, Wizara imeanza kutekeleza programu maalumu ya uendelezaji upya wa maeneo chakavu *(Land Readjustment Program)* katika miji mbalimbali hapa nchini. Programu hii inalenga kuwezesha upatikanaji wa makazi bora kwa wananchi, kuongeza thamani ya miji na maeneo yake, kuboresha huduma za jamii, kuvutia wawekezaji, kuboresha mazingira na mandhari ya miji hiyo na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi. Jumla ya maeneo 111 yenye ukubwa wa hekta 24,309.3 yameainishwa katika halmashauri 35 zilizopo kwenye mikoa 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuratibu uendelezaji upya wa eneo la Makangira - Msasani katika Manispaa ya Kinondoni lenye ukubwa wa hekta 17.20 kama eneo la mfano. Kazi ya kuendeleza eneo hilo imeanza kwa kuwashirikisha wananchi ambapo ukusanyaji wa taarifa na utambuzi wa milki za wakazi wa eneo hilo umefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hizo zitawezesha kufahamu hali halisi ya maisha ya wakazi wa eneo hilo, thamani ya rasilimali zilizopo, mahitaji na matamanio ya wananchi na namna ya kufanya mgawanyo wa milki zitakazoboreshwa. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaanza upangaji na upimaji wa ardhi sambamba na kutafuta wawekezaji wenye sifa na uwezo wa kuendeleza eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, Wizara imekamilisha rasimu ya mpango wa uendelezaji upya eneo la Sinza katika Manispaa ya Ubungo ambapo wananchi na wadau mbalimbali wanaendelea kutoa maoni yao. Mpango huu unalenga kuongeza thamani ya uwekezaji wenye tija katika kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza pato la Taifa kwa kusanifu matumizi mchanganyiko yatakayowezesha kuongeza viwango vya ujenzi wa eneo hilo kuanzia sakafu mbili hadi sakafu 20

kulingana na uhimilivu wa uwezo wa ardhi. Katika kutekeleza mpango huu, wamiliki wa ardhi katika maeneo hayo ndio watakaoshiriki katika kuendeleza ardhi zao kwa kuzingatia mpango utakaopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nirudie eneo hilo. Katika kutekeleza mpango huu, wamiliki wa ardhi katika maeneo hayo, ndio watakaoshiriki katika kuendeleza ardhi zao kwa kuzingatia mpango utakaopitishwa. Nitumie fursa hii kuwahakikishia wamiliki wa ardhi katika maeneo hayo kuwa hakuna ardhi itakayochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa mapendekezo ya kutunga sheria ya milki na kuyawasilisha kwenye mamlaka ya maamuzi. Hatua hii inalenga kuimarisha usimamizi wa sekta ya milki. Sheria itakayopendekezwa inalenga kuanzisha mamlaka ya kusimamia sekta ya milki *(Real Estate Regulatory Authority)* ambayo pamoja na masuala mengine itakuwa na jukumu la kuunda mfumo madhubuti wa usimamizi wa sekta ya milki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuratibu mchakato wa kutunga Sheria hii ya Milki na vilevile, kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji milki na kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa wadau wote wa sekta ya milki kuhakikisha kuwa wanasajiliwa na mamlaka hii itakapoanza kufanya kazi ili kutambuliwa na Serikali kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na ukuaji endelevu wa sekta hii ambayo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara inaendelea na azma yake ya kuziwezesha halmashauri za miji, wilaya, manispaa na majiji ili kuziongezea kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi *(Plot Development Revolving Fund - PDRF)*. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, jumla ya shilingi bilioni 50 zimekopeshwa kwa halmashauri 57 ambapo jumla

shilingi bilioni 33.18 zimerejeshwa ambayo ni sawa na 66.41% ya fedha zilizokopeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Fedha kwa lengo la kuchukua hatua stahiki kwa halmashauri ambazo hazijakamilisha kurejesha fedha hizo. Nitumie fursa hii, kwanza kuzipongeza halmashauri ambazo zimekamilisha marejesho ya fedha zilizokopeshwa. Aidha, nizikumbushe halmashauri ambazo hazijakamilisha kurejesha mikopo hiyo zifanye hivyo mara moja ili kutoa fursa kwa halmashauri nyingine nchini kunufaika na fursa hii adhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara inatekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani *(Land Data Infrastructure)* ambao unalenga kurahisisha kazi za upangaji na upimaji ardhi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kukamilisha ununuzi wa vifaa na kuanza uandaaji wa ramani za msingi za uwiano mkubwa wa 1:2,500 kwa miji mikuu ya mikoa na uwiano mdogo wa 1:25,000 kwa nchi nzima. Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa ndege maalumu itakayotumika kupiga picha za anga na kutengeneza ramani za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara inatarajia kumpata mkandarasi atakayejenga Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji *(Continuously Operating Reference Stations)* vipatavyo 30 na kuandaa ramani za msingi za uwiano mdogo wa 1:25,000 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kuimarisha mipaka ya Kimataifa kwa kupima, kujenga na kukarabati alama zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa makubaliano ya uimarishaji wa mipaka. Katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuimarisha sehemu ya mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya upatao kilometa 100 pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi kilometa 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 15 Mei, 2026, Wizara imeimarisha Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya

kutoka Tarakea - Wilaya ya Rombo hadi Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi - Wilaya ya Mwanga kwa jumla ya kilometa 106 na hivyo kufanya jumla ya kilometa zilizoimarishwa kufikia 564 kati ya kilomita 758 za eneo la nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuendelea kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilometa 140, kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilometa 70, kupima na kuimarisha kilometa 100 za mipaka ya Kimataifa kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ya majukumu ya Wizara ni kuratibu na kusimamia shughuli za taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Shirika la Nyumba la Taifa, Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini, Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi, na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Katika mwaka 2025/2026, Tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 240 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2026, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 253 katika halmashauri za wilaya 24 nchini imeandaliwa ikiwa ni sawa na 105.42% ya lengo walilojiwekea na kufanya jumla ya vijiji vilivyopangwa kufikia 4,925 kati ya vijiji 12,333 ambavyo vipo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kati ya vijiji 4,925 vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi tangu tupate uhuru, vijiji 2,750 sawa na 55.83% vimepangwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika mwaka 2026/2027, Tume itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 1,492, ununuzi wa vifaa na vitendea kazi, uzingatiaji wa matumizi ya ardhi, ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuongeza tengeo la bajeti kwa ajili ya kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi hapa nchini. Aidha, tengeo hilo litawezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji vingi kwa muda mfupi ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Hii inadhihirisha azma ya Mheshimiwa Rais ya kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi hapa nchini na kurejesha tabasamu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuenzi kazi nzuri ya kuimarisha upatikanaji wa makazi bora kwa Watanzania inayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita, Shirika la Nyumba la Taifa linatekeleza mradi wa *Samia Housing Scheme* wa ujenzi wa nyumba 5,000 unaotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 466.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Shirika lilipanga kuendelea na awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu kwa kujenga nyumba 908 katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2026, ujenzi wa nyumba 68 za makazi eneo la Iyumbu (Dodoma) umekamilika, hivyo kufanya jumla ya nyumba zilizokamilika kufikia 628. Aidha, ujenzi wa nyumba 260 katika eneo la Mtoni Kijichi umefikia 30% na ujenzi wa nyumba 160 eneo la Medeli (Dodoma) umefikia 25%. Kadhalika, maandalizi ya ujenzi wa nyumba 100 eneo la Njedengwa (Dodoma) na Kawe (Dar es Salaam) yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi iliyokuwa imesimama katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na miradi mingine ya ubia, ukandarasi, ujenzi wa majengo ya makazi na biashara pamoja na ukarabati wa nyumba katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mradi wa Kawe *711* wenye thamani ya shilingi bilioni 169 umefikia 85% ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, mwaka huu. Aidha, ujenzi wa nyumba 196 katika Mradi wa *Golden Premier Residence* wenye thamani ya shilingi bilioni 127 umefikia 50% na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027.

Vilevile, ujenzi wa mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* upo katika hatua za zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Shirika linaendelea na utekelezaji wa miradi ya ubia, ukandarasi, ujenzi wa majengo ya makazi na biashara, uendelezaji wa vitovu vya miji pamoja na ukarabati wa nyumba katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba katika mradi wa nyumba 5,000 wa *Samia Housing Scheme* katika maeneo ya Mtoni Kijichi na Kawe (Dar es Salaam); Medeli na Iyumbu (Dodoma). Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Njedengwa (Dodoma), Urafiki (Dar es Salaam), Sokoine *complex*, Mtaa wa Azimio (Arusha) na Makongoro (Mwanza);

(ii) Kuanza ujenzi wa nyumba 800 za gharama nafuu kwa awamu katika mradi wa *Salama Creek* Kigamboni (Dar es Salaam), Sabasaba (Morogoro), Iyumbu (Dodoma) na Buswelu (Mwanza);

(iii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba 196 katika mradi wa *Golden Premier Residence* na Kiwanja Na. 300 *Regent Estate;*

(iv) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya majengo ya biashara katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo *Meru view shops* (Ngarenaro) na Usa River (Arusha), *Tabora Commercial Complex* (Tabora), *Mkwakwani Commercial Complex* (Tanga), *Uluguru Plaza* (Morogoro), *Iringa Commercial Complex* (Iringa), *Songea Commercial Complex* (Ruvuma), *Bukoba Complex* (Kagera), 17A Mwenge na 1K *Market Street* (Singida), *Uganda Avenues* na RAS Kilomoni (Dar es Salaam).

(v) Kuendelea kutekeleza mpango wa ukarabati wa nyumba za Shirika 2,200; na

(vi) Kutekeleza miradi ya ukandarasi na Ushauri elekezi inayoendelea na mingine itakayojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pia inasimamia utekelezaji wa shughuli za Bodi mbalimbali za wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni pamoja na Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipango Miji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kusimamia maadili ya kitaaluma. Vilevile, Wizara inasimamia Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro. Vyuo hivyo hutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali za ardhi. Aidha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu ni nguzo muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa katika maeneo yanayohusiana na masuala ya uendeshaji wa ofisi, ajira, maendeleo ya kitaaluma, usimamizi wa utendaji kazi na masuala ya ustawi wa watumishi. Katika mwaka 2025/2026, Wizara imepokea watumishi 483 wa ajira mpya ambao wameongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spiia, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutupatia watumishi wapya ambao wataongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaothibitika kufanya makosa au kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria na taratibu zilizopo ambapo hatua za awali za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya watumishi watano, ambao walituhumiwa kukiuka maadili, weledi, sheria na kanuni za utumishi wa umma na kukutwa na tuhuma za kusababisha migogoro ya ardhi. Aidha, Kamati zimeundwa kwa ajili kuchunguza tuhuma hizo ili hatimaye

watumishi hao wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii tena, kuwaelekeza watumishi wote wa Sekta ya Ardhi kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia utu na maadili ya utumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Wizara yetu haitamvumilia mtumishi yeyote atakayekiuka maadili ya kazi kwa kukwamisha nia na dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa huduma bora za ardhi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuweka msisitizo katika uwajibikaji, usimamizi wa misingi ya uadilifu na weledi katika utoaji wa huduma bora za ardhi nchini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi 460, kupandisha vyeo watumishi 672 na kubadilisha kada watumishi 13. Vilevile, Wizara itawawezesha watumishi 1,272 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wakiwemo watumishi 460 wa ajira mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeendelea kuendesha Kliniki za Ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, ambapo huduma zote za Sekta ya Ardhi ikiwemo utoaji wa elimu kwa umma, zimekuwa zikitolewa kwa wananchi. Mathalani, mwezi Machi, 2026 katika wiki ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake, Wizara iliendesha Kliniki ya Ardhi ambayo ilikuwa mahususi kwa ajili ya kutoa elimu kwa wanawake, kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi iliyojulikana kama Samia Ardhi Kliniki, iliyoongozwa na kaulimbiu isemayo “Mwanamke, Haki yako, Miliki Ardhi Sasa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo lilikuwa kuongeza uelewa, hamasa na umiliki wa ardhi kwa wanawake. Kampeni hiyo ilifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yanayoadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi. Kupitia kampeni hiyo, wananchi 16,864 walihudumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote kutoka sekta binafsi wakiwemo Chama cha Wapima Ardhi Tanzania, Chama cha Wataalamu wa Mipangomiji Tanzania, Chama cha Wataalam wa Milki Tanzania, Chama cha Wanasheria Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Asasi za Kiraia kwa ushiriki wao katika kutekeleza majukumu ya sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wao katika upangaji, upimaji na uthamini wa mali, Kliniki za Ardhi na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi umeongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi hapa nchini. Wizara inaahidi kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu ili kufikia malengo yaliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana, Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano ambao wameendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninawashukuru Bwana Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi, Bibi Evelyne Baruti Mugasha, Mthamini Mkuu, Bibi Stella Chaggi Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Bwana Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa, Bwana Joseph Constantine Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa juhudi na maarifa ili kufikia malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Masasi kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa jukumu la kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, ninapenda kuishukuru sana familia yangu na hasa mke wangu Bi. Grace Akwilapo na watoto wangu Catherine Akwilapo, Felix Akwilapo na Emmanuel Akwilapo pamoja na wajukuu zangu kwa upendo, ushauri, uvumilivu na kunitia moyo wakati wote nikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kitaifa. Pia, ninawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zimeendelea kunipa nguvu katika kutekeleza majukumu yanayonikabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya EXIM ya Korea Kusini, *UN-HABITAT, Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources for Development, Tanzania Mortgage Refinance Company*, Watumishi *Housing Company,* Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, *Association for Development of Protected Areas*, Taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mzuri waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi. Kwa hakika, wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi, zaidi ya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Hotuba hii. Aidha, kwa mara nyingine nitumie fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mnaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii, yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina

shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni www.lands.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa vipaumbele na Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka 2026/2027, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha bajeti ya jumla ya shilingi 210,259,515,000 kwa ajili ya matumizi ya mafungu yote mawili yaani Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Shilingi 100,124,553,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 61,134,550,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Tume na shilingi 39,093,003,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na

(ii) Shilingi 110,034,962,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 44,132,469,000 ni Fedha za Ndani na shilingi 65,902,493,000 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru tena wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mnaoipa Wizara wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI MHE. DKT. LEORNAD AKWILAPO (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba

na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**), Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2025/26. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la **13** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27. Aidha, kipekee namshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa kwa kushirikiana na viongozi na watumishi wote wa Wizara nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa uadilifu na weledi ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma katika Sekta ya Ardhi kwa ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipatia Msaidizi makini, mahiri na mchapakazi Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya (Mb.), Naibu Waziri ambaye amekuwa akinisaidia katika kutekeleza majukumu ya sekta.

SALAMU ZA PONGEZI

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Ushindi huo ni ishara ya imani waliyonayo Watanzania kutokana na uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umedumisha amani, umoja, upendo na mshikamano nchini; umeimarisha utulivu wa kisiasa na diplomasia ya uchumi; na kuvutia uwekezaji katika sekta ya ardhi na uendelezaji milki. Miongoni mwa masuala makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais katika sekta ya ardhi kwa kipindi cha uongozi wake ni pamoja na kuwezesha ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya

Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 hivyo kuwa na Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) ambayo imetoa mwelekeo mpya wa usimamizi wa ardhi nchini. Aidha, Mheshimiwa Rais amewezesha maboresho ya mifumo ya TEHAMA na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi nchini.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Balozi, Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza kwa umahiri wake katika kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. Ninamshukuru kwa maelekezo na miongozo ambayo imeendelea kuniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uongozi mahiri kwa kuendelea kudumisha misingi ya Muungano pamoja na kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi. Miongoni mwa masuala yaliyotiliwa mkazo katika hotuba hiyo ni pamoja na kusimamia upangaji na upimaji wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuboresha huduma za uthamini na ulipaji fidia; kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro; kuendeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani ili kuongeza tija, uwazi na kasi ya utoaji huduma. Wizara imezingatia na inaendelea kutekeleza maelekezo na maagizo yanayohusu sekta ya ardhi ili kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini, kudhibiti migogoro ya ardhi, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuifanya ardhi kuwa mtaji hai kwa wananchi.

7. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninawapongeza wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakisimamia na kuongoza shughuli za Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Mhimili huu wa Bunge.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) kwa maoni na ushauri ambao umeiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2026/27. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii na hivyo kutoa mwelekeo mpya wa utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Ardhi.

SALAMU ZA POLE

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa salamu za pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba mzito wa kuondokewa na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) uliotokea tarehe 25 Machi, 2026 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma. Mheshimiwa Lukuvi atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa katika kujenga misingi ya utawala bora na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, atakumbukwa kwa kuweka misingi madhubuti ya utawala na usimamizi wa sekta ya ardhi

kwa kipindi alichohudumu kama Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia mwaka 2015 hadi 2022.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na waheshimiwa wabunge wenzangu kutoa pole kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kutokana na kifo cha Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, natoa pole kwa familia za marehemu, ndugu, jamaa na wananchi walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, wapo viongozi na Watanzania wenzetu waliofikwa na ajali, majanga na maafa mbalimbali yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na mali zao kutokana na maafa hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka Watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

MAJUKUMU YA WIZARA

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Na. 685 la tarehe 19 Desemba 2025, Wizara imekabidhiwa majukumu yafuatayo: -

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023);
ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;
iii) Kusimamia utawala wa ardhi;
iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;
v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;
vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila;
vii) Kusajili Hatimiliki za Ardhi, Miamala na Nyaraka za Kisheria;
viii) Kusimamia uthamini wa mali;
ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;
x) Kusimamia Uendelezaji Milki;
xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi;
xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;
xiv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara; na
xv) Kusimamia maslahi, utendaji kazi na maendeleo ya watumishi wa Wizara.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ardhi ni rasilimali muhimu inayotoa fursa kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Hivyo, sekta ya ardhi imeendelea kuwa sekta wezeshi kwa uwekezaji na uzalishaji katika sekta za viwanda, mifugo, kilimo, madini, ujenzi, uvuvi, maliasili, nishati na miundombinu na hivyo kuchangia katika kuongeza ajira kwa wananchi, pato la mwananchi mmoja mmoja, mapato ya Serikali na kukuza Pato la Taifa.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepanga kutekeleza vipaumbele nane (**8**) kama ifuatavyo: -

i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati;
ii) Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji;
iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma, ukusanyaji wa maduhuli na upatikanaji wa taarifa za ardhi na uthamini;
iv) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;
v) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
vi) Kuimarisha mipaka ya Kimataifa na kuendeleza miji ya mipakani;
vii) Kuimarisha upatikanaji wa ramani ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya Kitaifa na matumizi mengine; na
viii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa vipaumbele.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vilivyobainishwa vitawezesha kufikia malengo ya sekta yaliyoainishwa katika Sera

ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka, 1995 (Toleo la 2023); Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000; Dira 2050; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 13 mwezi Novemba 2025; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27-2030/31); Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; na Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2026/272030/31).

15. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, majukumu na vipaumbele vya Wizara, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2026/27. Aidha, takwimu za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/26 zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2026.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/26 NA MALENGO YA MWAKA 2026/27

16. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Fungu **48** -Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03** -Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mapato na Matumizi ya Fedha (Fungu 48)

Mapato

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **290** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali za sekta ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imekusanya shilingi bilioni **191.90** sawa na asilimia **66.17** ya lengo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni **300** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuendelea kusambaza miundombinu na mifumo ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri ili

kurahisisha utoaji wa huduma za ardhi; kuendelea kushirikiana na OWM-TAMISEMI kufuatilia halmashauri ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa miradi ya KKK; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha mahakamani na kuwasilisha taarifa zao kwa Kampuni ya Taarifa za Mikopo (Credit Information Reference Bureau-CIRB); kuendelea kubuni miradi ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za sekta na kuomba vibali vya ajira mpya ili kukidhi mahitaji ya rasilimaliwatu; kuendelea kuunganisha namba za simu za wamiliki wote wa ardhi ili waweze kupata jumbe fupi za kuwakumbusha kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; na kuhakikisha viwanja vyote vilivyopimwa vinamilikishwa kwa wahusika. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine inaendelea kutafuta njia bora ya ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kupitia huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi hizo.

Matumizi

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni **153.44** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **53.82** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi, shilingi bilioni **37.56** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **62.06** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi bilioni **5.73** ni Fedha za Maendeleo za Ndani na shilingi bilioni **56.33** ni Fedha za Maendeleo za Nje. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni **64.24** ambapo shilingi bilioni **60.94** zilitumika kwa ajili kulipa madeni na shilingi bilioni **3.30** zilitumika kutetea maombi ya Eneo la Nyongeza Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini (Extended Continental Shelf) yaliyowasilishwa Umoja wa Mataifa, na hivyo kufanya Bajeti ya Maendeleo kuongezeka hadi shilingi bilioni **126.29** na Bajeti ya Wizara kufikia jumla ya shilingi bilioni **217.68**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imepokea shilingi bilioni **141.09** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia **64.82** ya bajeti. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **43.85** ni mishahara; shilingi bilioni **31.51** ni Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **65.74** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni **137.55** sawa na asilimia **95.51** zimetumika; ambapo shilingi bilioni **43.84** zilitumika kulipa mishahara ya watumishi, shilingi bilioni **29.82**

zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **63.89** zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 1**).

Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03

Mapato

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilipanga kukusanya shilingi milioni **18** kupitia kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imekusanya shilingi milioni **16.05** sawa na asilimia **89.17** ya lengo. Vilevile, Tume ilipanga kupokea michango ya shilingi bilioni **1** kutoka kwa wadau wa kimkakati. Hadi tarehe 15 Mei 2026, shilingi milioni **417.79** zilipokelewa sawa na asilimia **41.78** ya lengo. Kwa mwaka 2026/27, Tume imepanga kukusanya shilingi milioni **18** kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo mkoani Tabora. Aidha, juhudi za kuhamasisha wadau wa kimkakati kuchangia shilingi milioni **500** kwa ajili ya kugharamia shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi nchini zinaendelea.

Matumizi

21. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni **10.71**. Aidha, wakati wa utekelezaji wa bajeti, Tume iliongezewa shilingi bilioni **2** kwa ajili ya kugharamia Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, hivyo jumla ya bajeti kuwa shilingi bilioni **12.71**. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **4.71** ni Mishahara ya Watumishi, shilingi bilioni **3.48** ni Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **4.52** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imepokea shilingi bilioni **10.33** sawa na asilimia **81.27** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **3.58** ni mishahara ya watumishi (PE), shilingi bilioni **2.23** ni Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi bilioni **4.52** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Aidha, kati ya fedha zote zilizopokelewa, jumla ya shilingi bilioni **10.24** sawa na asilimia **99.13** zimetumika. Kati ya fedha hizo zilizotumika, shilingi bilioni **3.58** zilitumika kulipa mishahara ya watumishi, shilingi bilioni **2.23** zilitumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi bilioni **4.43** zilitumika kutekeleza Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi **(Jedwali Na. 2)**.

UTAWALA WA ARDHI

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za ardhi kwa kushughulikia na kusimamia uandaaji na usajili wa Hatimiliki za ardhi, usimamizi wa masharti ya umiliki, ugawaji wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, usimamizi wa ardhi ya uwekezaji, uhuishaji wa kumbukumbu za ardhi na uthamini wa mali. Huduma hizi zimewezesha kuboresha taratibu za usimamizi wa ardhi na kuhakikisha wananchi wanakuwa na milki salama za ardhi zinazowawezesha kutumia milki hizo kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuandaa na kusajili Hatimiliki **500,000**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **520,000**, Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki **107,683** sawa na asilimia **21.54** ya lengo; Hati za Hakimiliki ya Kimila **99,762** sawa na asilimia **19.19** ya lengo; Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **148** sawa na asilimia **148** ya lengo; na Hati za Sehemu ya Jengo **914** sawa na asilimia **91.4** ya lengo. Aidha, jumla ya Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **137,681** zimesajiliwa sawa na asilimia **137.68** ya lengo ambapo Miamala ya Hatimiliki ni **76,918** na Nyaraka za Kisheria ni **60,763 (Jedwali Na. 3)**.



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akikabidhi Hatimiliki kwa mwananchi wakati wa Kliniki Maalum ya Samia Ardhi Kliniki



Mhe. Kaspar Mmuya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akimkabidhi mwananchi Hati ya Hakimiliki ya Kimila Wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuandaa na kusajili Hatimiliki **200,000**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **300,000**, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **60**, Hati za Sehemu ya Jengo **1,000** na Miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Ili kufikia lengo la utoaji wa Hatimiliki katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kusambaza Mfumo wa e-Ardhi katika halmashauri zote nchini ili kurahisisha na kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi, kuendelea kuhimiza wananchi kuchangia gharama za urasimishaji na umilikishaji ardhi, kuziwezesha halmashauri kutekeleza Programu za Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kuendelea na Kliniki za Ardhi ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. **Natoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanamiliki ardhi zao kisheria ili kuepuka migogoro na kuwawezesha kutumia ardhi kama mtaji wa kujiletea maendeleo.**

Usimamizi wa masharti ya umiliki

25. ***Mheshimiwa Spika***, sheria za ardhi zinamtaka kila mmiliki kuendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya pango la ardhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili

kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya viwanja na mashamba **2,503** yalikaguliwa. Ukaguzi huo ulibaini kuwa wamiliki **1,571** wa viwanja na mashamba walizingatia masharti ya umiliki na wamiliki **932** wa viwanja na mashamba walikiuka masharti ya umiliki. Wizara imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki ambapo milki za mashamba na viwanja **15** zimefutwa na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wamiliki **917**. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kufanya uhakiki na ukaguzi wa viwanja na mashamba **1,000** ili kubaini hali ya uendelezaji na kuchukua hatua stahiki. **Natoa rai kwa wamiliki wa ardhi kuendeleza milki zao kwa mujibu wa masharti ya umiliki ili kuepuka Serikali kubatilisha milki hizo.**

Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia uidhinishaji wa maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Ardhi ya uwekezaji hutambuliwa, hutangazwa na kumilikishwa kwa Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) ambayo hutoa Hatimiliki Isiyo Asili (Derivative Right) kwa wawekezaji. Pamoja na jitihada binafsi zinazofanywa na wawekezaji ili kupata ardhi, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kuna ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Mikakati hiyo ni pamoja na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia Mipango Kabambe inayoandaliwa, Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na ardhi ya mashamba yaliyobatilishwa. Jukumu hilo linatekelezwa na Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi iliyo chini ya Wizara ambayo huchambua, kujadili na kuidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kugawa hekta **5,000** kwa wawekezaji. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi imepokea na kuidhinisha maombi **333** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **45,371.24.** Kati ya maombi yaliiyoidhinishwa, maombi **81** yenye ukubwa wa hekta **5,802.14** ni ya wawekezaji wa ndani na maombi **252** yenye ukubwa wa hekta **39,569.10** ni ya wawekezaji kutoka nje. Katika mwaka 2026/27, Wizara itatenga na kugawa ardhi yenye ukubwa wa hekta **5,000** kwa ajili ya uwekezaji.




Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi ikikagua shamba la mwekezaji jijini Arusha

27. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia azma ya Serikali ya kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini, Wizara imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha utoaji wa huduma kwenye Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania (TISEZA) kwa kuanzisha ofisi maalum ya ardhi kwa ajili ya kushughulikia masuala ya uwekezaji. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi kwenye mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza ambayo ina mahitaji makubwa ya huduma kwa kuanzisha ofisi mpya za ardhi kwenye mikoa hiyo. Hivyo, mikoa hiyo imekuwa na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wawili hatua ambayo itaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kuwafikia wananchi karibu zaidi na maeneo yao. **Napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na dhamira yake ya kuhakikisha wawekezaji na wananchi wanapata huduma bora za ardhi kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.**

Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi

28. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa taarifa sahihi za wamiliki wa ardhi, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu za ardhi na kuziingiza katika

Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa urahisi, usahihi na kwa muda mfupi. Uhuishaji huo unahusisha ubadilishaji wa nyaraka za hatimiliki na majalada kutoka analojia kwenda mfumo wa kidijiti, uhakiki na uhuishaji wa taarifa za wamiliki pamoja na kubainisha ukubwa wa viwanja, matumizi na mahali vilipo. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **500,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, kumbukumbu za ardhi **146,345** zimehuishwa. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **500,000** na kuziingiza katika Mfumo wa e-Ardhi.



Watumishi wakiendelea na kazi ya kubadilisha taarifa za ardhi kutoka nakala ngumu kwenda nakala tete (Data Conversion)

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala

29. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa Kliniki za Ardhi kwenye mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, madawati ya kushughulikia kero na malalamiko, timu na kamati maalum za wataalam wa Serikali na ziara za viongozi wa Wizara katika maeneo mbalimbali nchini. Utatuzi huo unahusisha changamoto za ardhi zinazotokana na masuala ya fidia; milki pandikizi; mwingiliano wa mipaka ya vijiji, viwanja au mashamba; uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi; udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi; madai ya mali za urithi au wanandoa; na changamoto zinazotokana na zoezi la urasimishaji makazi na upimaji shirikishi wa ardhi. Kadhalika, yapo malalamiko yanayotokana na wananchi kutoridhika na uamuzi wa vyombo vinavyotoa haki kisheria.



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akizungumza na wananchi wa Mahomanyika Dodoma wakati wa kushughulikia mgogoro wa ardhi

30. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuwepo kwa migogoro ya ardhi inayoendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali nchini, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** alielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa mkakati wa kupata ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hiyo. Kufuatia maelekezo hayo, Serikali imeandaa na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Migogoro ya Ardhi Nchini. Mkakati huo unahusisha wadau na makundi yote muhimu hususan wakulima, wafugaji, wawekezaji na mamlaka za hifadhi ili kuhakikisha changamoto ya migogoro ya ardhi inapatiwa ufumbuzi wa kudumu. **Napenda kutumia fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha migogoro ya ardhi inadhibitiwa hivyo kuwawezesha watumiaji wa ardhi kufanya kazi zao kwa amani na utulivu.**

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kushughulikia migogoro ya ardhi **3,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya migogoro ya ardhi **5,573** imetatuliwa ambapo kati ya

hiyo, migogoro **3,183** imetatuliwa kupitia Kliniki za Ardhi na **2,390** kupitia utaratibu wa kawaida wa kiutawala (**Jedwali Na. 4**). Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kushughulikia migogoro **4,000** kiutawala. **Natoa rai kwa viongozi, watumishi na wananchi kwa ujumla kuzingatia sheria za ardhi, kanuni na miongozo ili kuepuka kuanzisha migogoro mipya**.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/ Mitaa 975

32. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu ukamilishaji wa kazi zilizobaki za utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa **975**. Uamuzi umeendelea kutekelezwa ikiwemo kurejesha ardhi kwa wananchi ambapo ekari milioni **3.13** zimerejeshwa na shilingi bilioni **95.27** zimelipwa kwa wananchi waliostahili kulipwa fidia katika maeneo **14 (Jedwali Na. 5)**. Kazi hiyo imefanywa na timu ya wataalam kutoka taasisi na wizara za kisekta.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia tathmini iliyofanyika, mpango kazi kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizobaki umeandaliwa. Hivyo, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi na Wizara za Kisekta, itaendelea kuratibu ukamilishaji wa kazi hizo. Utekelezaji husika utahusisha vijiji **349** na mitaa **11** ambayo sehemu ya utekelezaji wa maamuzi umeanza kufanyiwa kazi, pamoja na vijiji **166** ambavyo utekelezaji wake utafanyika katika mwaka 2026/27.

Uthamini wa Mali

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu pia inasimamia uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, uidhinishaji wa taarifa za uthamini na uandaaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi, mazao na majengo. Viwango vya bei ya soko ndivyo hutumika kufanya uthamini ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (premium) wakati wa kutoa milki, mizania ya hesabu, kuweka mali rehani, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kuidhinisha taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa

za uthamini wa kawaida ni **20,000** na majedwali ya fidia yenye wafidiwa **34,000.** Aidha, Wizara ilipanga kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini, kukamilisha uandaaji wa vitalu vya thamani ya ardhi katika mikoa saba (**7**) na kuendelea na zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa **26**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **57,293** sawa na asilimia **106.10** ya lengo ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **27,211** na majedwali ya fidia yenye wafidiwa **30,082**. Aidha, malalamiko ya uthamini **99** yalipokelewa na kushughulikiwa kiutawala. Vilevile, zoezi la kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi na mazao limefanyika katika mikoa **26** nchini na uhuishaji wa viwango vya thamani ya majengo umefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kushiriki katika kufanya uthamini wa mali katika maeneo yanayotwaliwa ili kupisha miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uthamini wa mali za wananchi wanaotakiwa kupisha miradi ya reli ya kisasa–SGR kipande cha Tabora Kigoma na Tabora– Shinyanga; utafiti wa mafuta na gesi katika kitalu cha Lindi– Mtwara; maeneo ya uwekezaji; na miradi ya maji, barabara na umeme. Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuidhinisha taarifa za uthamini **50,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za fidia zenye wafidiwa ni **30,000**; kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini; na kuhuisha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi, mazao na majengo katika mikoa **26**.



Wataalamu wakiwa katika zoezi la uthamini katika eneo la Mradi wa Reli ya SGR Tabora-Kigoma kipande cha sita mkoani Kigoma



Elimu ya uthamini wa fidia ikitolewa kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR Tabora-Kigoma Kipande cha sita

MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

37. ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya jukumu la Wizara ni kuanzisha na kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ambayo yanasikiliza na kuamua migogoro ya ardhi kisheria. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeendelea kuanzisha Mabaraza katika wilaya mbalimbali nchini ambayo yamekuwa yakisikiliza na kuamua mashauri ya ardhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuanzisha Mabaraza mapya **24** na kushughulikia mashauri **16,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeanzisha Mabaraza mapya sita (**6**) na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza **121** yanayofanya kazi. Aidha, mashauri **23,426** yamesikilizwa ambapo kati ya hayo, mashauri **12,644** yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi na mashauri **10,782** yanaendelea kushughulikiwa. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaanzisha Mabaraza mapya **18** ili kufikia lengo la kuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya zote **139** zilizopo nchini. Aidha, Wizara itaendelea kushughulikia mashauri **10,782** yaliyobaki na yatakayofunguliwa. **Natoa wito kwa wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kuzingatia weledi, uadilifu na misingi ya utoaji haki katika kuamua mashauri ya ardhi ili kujenga imani kwa wananchi wanaopata huduma katika Mabaraza yetu.**

HUDUMA ZA TEHAMA

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kusimika miundombinu ya TEHAMA katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri zote nchini, kusambaza Mfumo wa e-Ardhi, kutoa elimu na kuwajengea uwezo watumiaji. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imesambaza vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya shilingi bilioni **5.20** katika mikoa na halmashauri zote nchini. Aidha, huduma za uthamini na usajili wa nyaraka zinatolewa kupitia Mfumo wa e-Ardhi nchi nzima na huduma za utawala wa ardhi zinatolewa kupitia mfumo huo katika mikoa mitano (**5**) ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tanga na Mwanza pamoja na baadhi ya halmashauri za mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Mtwara, Pwani na Ruvuma. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea na juhudi za kuhakikisha huduma zote zinapatikana kupitia mfumo huo katika ofisi zote za ardhi za mikoa na halmashauri nchini, sambamba na kusafisha na kubadili taarifa za kijiografia na majalada ya umiliki wa ardhi kutoka analojia kwenda kidijiti, ambayo ni hatua muhimu ya usambazaji wa mfumo huu.



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (kushoto) akimkabidhi vifaa vya TEHAMA Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mtwara Bw. Fredrick Mrema (katikati). Kulia ni Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imerahisisha huduma za malipo ikiwa ni pamoja na wananchi kutumiwa au kutengeneza ankara zao bila kulazimika kufika kwenye Ofisi za Ardhi, kulipia kodi ya pango la ardhi wakati wowote na mahali popote kupitia simu, mawakala au benki ambapo kwa sasa namba ya malipo ni ya kudumu. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wananchi **127,449** wamejengewa uwezo, kujisajili na kuhudumiwa kupitia mfumo. **Natoa wito kwa wananchi kuendelea kufuatilia matangazo yanayotolewa katika vyombo mbalimbali vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti ya Wizara ili kujifunza kuhusu huduma za sekta ya ardhi zinazotolewa kupitia Mfumo wa eArdhi**.

UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uwekaji wa alama za msingi; upimaji ardhi nchi kavu na ndani ya maji kwa ajili ya shughuli za haidrografia; na utayarishaji wa ramani za msingi, ramani za mipaka ya kiutawala na ramani za matumizi mbalimbali kwa ajili ya *utekelezaji* wa mipango ya Serikali na shughuli za maendeleo. Pia, Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Uwekaji Alama za Msingi za Upimaji Ardhi

41. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa kazi za Upimaji nchini zinatekelezwa kwa ufanisi, Wizara imeendelea kuongeza Alama za Msingi za Upimaji (Control Points) na kuanza usimikaji wa alama za msingi zinazoendana na teknolojia ambazo ni Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji (Continuously Operating Reference Stations- CORS) ambavyo ni miongoni mwa miundombinu muhimu katika kurahisisha kazi za upimaji kwa kupunguza muda na gharama za upimaji.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuweka Alama mpya za Msingi za Upimaji **438** katika halmashauri mbalimbali nchini pamoja na kukamilisha ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** katika mikoa **20** ya Dodoma, Iringa, Pwani, Kagera, Njombe, Mara, Dar es Salaam, Manyara, Rukwa, Arusha, Mtwara, Ruvuma, Geita, Katavi, Mwanza, Kigoma, Shinyanga, Singida, Morogoro na Tanga. Hadi tarehe 15

Mei 2026, Alama za Msingi za Upimaji **55** zimewekwa katika mikoa ya Kilimanjaro (**15**) na Mbeya (**40**). Aidha, ujenzi na usimikaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** umekamilika na vituo vitatu (**3**) vya Kielektroniki vilivyopo mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Tabora vimehuishwa. Vilevile, vituo vyote vimeanza kutumika katika shughuli mbalimbali za upimaji. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaongeza Alama za Msingi za Upimaji **438** pamoja na kuwezesha matengenezo ya vituo vya Kielektroniki vya Upimaji vilivyojengwa maeneo mbalimbali nchini.

Upigaji Picha za Anga

43. ***Mheshimiwa Spika,*** picha za anga ni muhimu kwa ajili ya kupata taarifa za msingi zinazotumika kuandaa ramani za msingi na ramani za matumizi maalum kama vile kupata taarifa za sura ya nchi, kupanga na kutathmini maendelezo ya miji. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imepiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **204.09** katika mikoa ya Dodoma (**44.89**), Geita (**158.3**) na Dar es Salaam (**0.9**). Aidha, ramani za mipaka ya kiutawala katika halmashauri za wilaya tano (**5**) zimeandaliwa ambazo ni Kongwa, Kondoa, Ushetu, Kaliua na Singida. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kupiga picha za anga katika eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba **1,000** na kuhuisha ramani za msingi pamoja na ramani nyingine katika wilaya mbalimbali nchini.

Tafsiri ya Matangazo ya Serikali kuhusu Maeneo ya Utawala (GN)

44. ***Mheshimiwa Spika,*** tafsiri ya Matangazo ya Serikali (GN) kuhusu maeneo ya utawala na hifadhi ni suala muhimu katika kutambua maeneo na kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi nchini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Waziri MkuuTAMISEMI imeendelea kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya maeneo ya utawala na hifadhi. Tafsiri hizo zinawezesha kutatua migogoro ya mipaka ya vijiji, wilaya, mikoa na hifadhi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) **10** ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara

kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imefanya tafsiri ya matangazo ya maeneo ya hifadhi tatu (**3**) za Burigi Chato, Selous na Udzungwa pamoja na mipaka ya kiutawala minne (**4**) katika wilaya za Kongwa, Chemba, Kondoa na Singida. Katika mwaka 2026/27, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Ofisi ya Waziri MkuuTAMISEMI imepanga kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) **10** ili kuwezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya ardhi.

Upimaji wa Viwanja na Mashamba

45. ***Mheshimiwa Spika,*** upimaji wa ardhi huwezesha kuwa na mipaka iliyotambuliwa kisheria na hivyo kuongeza usalama wa milki, thamani ya ardhi na kuepusha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi. Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na mamlaka za upangaji na sekta binafsi. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa viwanja **500,000** na mashamba ***500***. Hadi tarehe 15 Mei 2026, viwanja **193,317** na mashamba **515** yamepimwa na kuidhinishwa sawa na asilimia **38.66** na **103** mtawalia (**Jedwali Na. 6**). Katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kupima na kuidhinisha viwanja **500,000** na mashamba **500**.



Wataalam wa sekta ya ardhi wakiwa kwenye zoezi la upimaji wa mashamba

Upimaji wa Mipaka ya Vijiji

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mipaka ya kiutawala. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, mipaka ya vijiji **54** imehakikiwa na

kuhuishwa na vijiji **189** vimepimwa na hivyo kufanya vijiji vilivyopimwa kufikia **11,996** kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini (**Jedwali Na. 7**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na wadau wa maendeleo kuhakiki, kuhuisha na kupima mipaka ya vijiji **226** nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imeendelea kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya Serikali za Vijiji kuhusu kuathiriwa haki zao za ardhi baada ya kubainishwa kwa mipaka ya vijiji. **Nitumie fursa hii kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuheshimu haki za ardhi za wananchi ili kuondoa migogoro**.

UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

46. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi wa usanifu na upangaji wa miji ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355. Majukumu haya yanajumuisha uandaaji wa Mipango ya Jumla (Mipango Kabambe), Mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, maeneo maalum ya upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji, urasimishaji makazi na usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba.

Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutangaza maeneo yaliyoiva kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355. Baadhi ya vigezo vya kutangaza eneo kuendelezwa kimji ni pamoja na idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kiuchumi na kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi, maeneo ya wazi, soko na maduka yasiyopungua matano (**5**). Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji. Maeneo hayo huandaliwa Mipangokina na Mamlaka za Upangaji kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kuendelea kutangaza maeneo mapya ya upangaji miji na urasimishaji makazi ili kuendelea kusimamia uendelezaji na ukuaji endelevu wa miji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara ilipokea na kutangaza maeneo **42** kutoka katika Mamlaka za Upangaji **29**. Maeneo hayo yamepandishwa hadhi kutoka vijiji na kuwa

maeneo ya mipangomiji (**Jedwali Na. 8**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kuendelezwa kimji.

Uandaaji wa Mipango ya Jumla

50. ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji na uendelezaji wa miji huongozwa na Mipango ya Jumla inayoainisha matumizi mbalimbali ya ardhi katika miji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalam kwenye Mamlaka za Upangaji kuhusu uandaaji wa Mipango ya Jumla. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya Mipango ya Jumla ya miji minne (**4**) ya Mkuranga, Kwala, Mafinga na Manispaa ya Kahama yanaendelea. Vilevile, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango ya Jumla iliyoandaliwa umefanyika katika majiji ya Arusha, Dodoma, Tanga na Mbeya pamoja na Manispaa za Shinyanga na Morogoro. Ufuatiliaji huo umebaini kuwa Mipangokina inayoandaliwa inazingatia Mipango ya Jumla inayosimamia ukuaji wa miji hiyo. Aidha, Serikali kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness* (TACTIC) ambao unasimamiwa na kuratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI inaendelea na maandalizi ya awali ya kuandaa Mipango ya Jumla ya miji mingine **18** nchini **(Jedwali Na. 9)**.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/ 27, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji itaendelea kufuatilia uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Jumla kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuchochea maendeleo endelevu ya ukuaji wa miji nchini. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji wa Mipango ya Jumla pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa miradi inayopangwa inazingatia mipango hiyo.**

Uandaaji wa Mipangokina

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Mipangokina (Michoro ya Mipangomiji) ni mipango inayoongoza matumizi ya ardhi katika kiunga cha mji kwa kusanifu matumizi mbalimbali yanayohitajika kuwezesha jamii kuishi, kufanya kazi na kufurahia mandhari ya eneo husika. Mipango hii hutafsiri Mipango ya Jumla ardhini na huandaliwa na

Mamlaka za Upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo yenye matumizi mbalimbali.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya michoro ya mipangomiji **3,695** sawa na asilimia **184.75** yenye jumla ya viwanja **315,287** imeidhinishwa (**Jedwali Na. 10**). Katika mwaka 2026/27, Wizara itapokea, kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

Urasimishaji Makazi

54. ***Mheshimiwa Spika,*** urasimishaji makazi unahusisha kuboresha makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa kwa kuyatambua, kuyapanga, kuyapima na kumilikisha ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu, kuongeza usalama wa milki na uhifadhi wa mazingira. Katika mwaka 2025/26, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji ilipanga kuendelea kuratibu urasimishaji makazi **200,000** katika halmashauri zote nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya makazi **149,784** sawa na asilimia **74.89** yamerasimishwa (**jedwali Na. 11).** Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuratibu urasimishaji wa makazi **200,000**.

Udhibiti wa Uendelezaji Miji

55. ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa uendelezaji miji ni suala mtambuka linalotekelezwa na Wizara kwa kushirikisha Mamlaka za Upangaji na wadau wengine. Kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kiuchumi na kukua kwa teknolojia, miji hubadilika na kuhitaji uratibu katika uendelezaji wake ikiwemo mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa lengo la kuongeza tija katika matumizi ya ardhi mijini ili kukuza uchumi na Pato la Taifa. Kwa muktadha huo, Wizara ina jukumu la kupokea, kukagua na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanayowasilishwa kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukagua na kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **730** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambayo ni sawa na asilimia **236.67** ya lengo. Ongezeko hilo limetokana na kuboreshwa kwa huduma za sekta ya ardhi na miundombinu inayochochea mahitaji ya uwekezaji na biashara katika maeneo ya miji. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za udhibiti wa uendelezaji wa miji kwa kuidhinisha maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji kuzingatia sheria katika utoaji wa vibali vya uendelezaji ardhi (Planning Consent) kabla ya kutoa vibali vya ujenzi ili kuwaelekeza wamiliki wa ardhi namna ya kutumia ardhi zao kwa kuzingatia ukubwa wa eneo la kiwanja na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, ujenzi unaofanyika bila vibali udhibitiwe ili kuzuia ukuaji holela wa miji. Uendelezaji Upya na Uboreshaji wa Maeneo**

Chakavu Mijini

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 imehimiza uboreshaji wa makazi chakavu kwa kuweka miundombinu na huduma za jamii ili kuboresha mandhari ya miji na kuongeza fursa za kiuchumi na mchango wa maeneo hayo katika Pato la Taifa. Kwa kuzingatia takwa hilo la kisera, Wizara imeanza kutekeleza Programu Maalum ya Uendelezaji Upya wa Maeneo Chakavu (Land Re-adjustment Program) katika miji mbalimbali nchini. Jumla ya maeneo **111** yenye ukubwa wa hekta **24,309.3** yameainishwa katika halmashauri **35** zilizopo kwenye mikoa **25** (**Jedwali Na. 12**).

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kuratibu uendelezaji upya wa eneo la Makangira- Msasani katika Manispaa ya Kinondoni lenye ukubwa wa hekta **17.20** kama eneo la mfano. Kazi ya kuendeleza eneo hilo imeanza kwa kuwashirikisha wananchi ambapo ukusanyaji wa taarifa na utambuzi wa milki za wakazi wa eneo hilo umefanyika. Taarifa hizo zitawezesha kufahamu hali halisi ya maisha ya wakazi wa eneo hilo, thamani ya rasilimali zilizopo, mahitaji na matamanio ya wananchi na namna ya kufanya mgawanyo wa milki

zitakazoboreshwa katika eneo hilo. Katika mwaka 2026/27, Wizara itaanza upangaji na upimaji wa ardhi sambamba na kutafuta wawekezaji wenye sifa na uwezo wa kuendeleza eneo hilo.



Zoezi la ukusanyaji wa taarifa na utambuzi wa milki za makazi kwa wananchi kwa ajili ya uboreshaji maeneo chakavu ya miji katika eneo la Makangira, Msasani wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha rasimu ya mpango wa uendelezaji upya eneo la Sinza katika Manispaa ya Ubungo ambapo wananchi na wadau mbalimbali wanaendelea kutoa maoni. Mpango huu unalenga kuongeza thamani ya uwekezaji wenye tija katika kuboresha maisha ya wananchi na kuongeza Pato la Taifa kwa kusanifu matumizi mchanganyiko yatakayowezesha kuongeza viwango vya ujenzi wa eneo hilo kuanzia sakafu mbili (**2**) hadi **20** kulingana na uhimilivu wa uwezo wa ardhi. **Natoa wito kwa wananchi na sekta binafsi kuchangamkia fursa kwenye maeneo yote mawili na kushiriki kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa mipango hiyo kwa manufaa endelevu ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Nitumie fursa hii kuwahakikishia wamiliki wa ardhi katika maeneo hayo kuwa hakuna ardhi itakayochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa mpango huu.**

Usimamizi na Uratibu wa Uendelezaji Nyumba

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa nyumba nchini zoezi ambalo hufanywa na taasisi za umma, sekta binafsi na Vyama vya Ushirika wa Nyumba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi

mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na: - upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ubunifu wa nyumba za gharama nafuu na utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali. **Mikopo ya Ujenzi wa Nyumba**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilianzisha Taasisi ya *Tanzania Mortgage Refinance Company* (TMRC) kwa ajili ya kuwezesha taasisi za fedha kutoa mikopo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya shilingi bilioni **720.81** zimetolewa kwa wananchi **5,802** kupitia taasisi za fedha **29** (**Jedwali Na. 13**).

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kutoa mikopo kwa watumishi wa Serikali **137** yenye thamani ya shilingi bilioni **2.60**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya shilingi bilioni **2.94** zimetolewa kwa watumishi **111** sawa na asilimia **81** ya lengo na hivyo kufanya jumla ya watumishi waliopata mikopo tangu kuanzishwa kwa mfuko huo kufikia **1,921** yenye thamani ya shilingi bilioni **12.34**. Katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara imepanga kutoa mikopo kwa Watumishi wa Serikali **150.**

Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika

Uendelezaji wa Makazi

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kimataifa yenye lengo la kujenga mahusiano na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na uendelezaji makazi nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kusimamia na kuratibu ushirikiano na taasisi mbalimbali katika uendelezaji wa makazi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeshiriki kwenye mikutano sita (**6**) ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo;

i) Mkutano wa kuhitimisha Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Ushauri wa Utawala wa Ardhi Barani Afrika (SLGA) uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani na kuratibiwa na Tume ya Umoja wa Afrika jijini Addis Ababa Agosti, 2025;

ii) Mkutano wa Pili wa Mabadiliko ya Tabianchi Afrika (ACS2), Addis Ababa Septemba, 2025;

iii) Kikao kazi cha uthibitishaji wa Mpango Kazi wa pamoja wa kukabiliana na Maafa yanayohusiana na kuongezeka kwa kina cha maji katika Ziwa Tanganyika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Burundi, Dar es Salaam, Septemba, 2025;

iv) Kongamano la kimataifa la matumizi ya Akili Mnemba katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi katika nchi zinazoendelea na nchi ya Visiwa Vidogo lililoandaliwa na Umoja wa Mataifa (UNFCCC) uliofanyika Dar es Salaam, Oktoba, 2025;

v) Mkutano wa 30 wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) uliofanyika Belem - Brazil Novemba, 2025;

vi) Jukwaa la Pili la Miji Afrika (The Second African Urban Forum) lililofanyika Nairobi nchini Kenya Aprili, 2026; na

vii) Jukwaa la 13 la Miji Duniani limefanyika Baku-Azarbaijan Mei, 2026.



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akiwasilisha hoja ya Serikali ya Tanzania katika Kongamano la Pili la Miji Afrika (The Second African Urban Forum) lililofanyika jijini Nairobi nchini Kenya

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na taasisi mbalimbali za Kimataifa kwa lengo la kunufaika na fursa mbalimbali katika nyanja za uendelezaji wa miji na makazi.

USIMAMIZI NA URATIBU WA SEKTA YA MILKI

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kuendeleza sekta ya milki nchini ili kuhakikisha soko la milki linaimarika na kuwa na uwazi wa kutosha kwa lengo la kulinda maslahi ya wadau wote wakiwemo mawakala, wamiliki, wawekezaji, waendelezaji na watumiaji wa milki. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ukuaji wa Uchumi iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Desemba 2025, sekta ya milki imechangia Pato la Taifa kwa asilimia **4.40**. Mafanikio haya yameifanya sekta hii kuwa kivutio muhimu kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi hususan katika miradi ya ujenzi wa majengo ya biashara na nyumba za kupangisha na kuuza.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kuratibu ukamilishaji wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki, kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki nchini, kukamilisha kanuni na miongozo ya uendelezaji milki na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya milki. Hadi tarehe 15 Mei 2026, mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki yamewasilishwa kwenye Mamlaka husika kwa ajili ya uamuzi. Vilevile, jumla ya Mawakala wa Milki **350** wamejisajili katika kanzidata ya Wizara na waendelezaji milki **100** wametambuliwa. Aidha, Wizara imeendeleza uhusiano wa kikanda na kimataifa kwa kushiriki katika mikutano sita (**6**) ya kikanda na kimataifa iliyolenga kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya milki. Pia, Wizara imeratibu mikutano sita (**6**) ya wadau wa sekta ya milki kwa lengo la kuwatambua na kutoa elimu kuhusu uanzishwaji wa vyama vya mawakala wa milki na kujadili namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/ 27, Wizara itaratibu ukamilishaji wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Milki; kukamilisha kanuni na miongozo ya utambuzi na usajili wa mawakala wa milki, usimamizi wa majengo na nyenzo na uendelezaji milki; kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya milki; kuboresha mahusiano na wadau wa sekta ya milki; na kuhuisha kanzidata ya mawakala wa milki na waendelezaji milki nchini. **Natoa wito kwa wadau wote wa sekta ya milki kushirikiana na Serikali ili kuimarisha sekta ya milki kwa manufaa yao na uchumi wa Taifa letu kwa ujumla.**

MAPITIO YA SHERIA ZA SEKTA YA ARDHI

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga kufanya marekebisho ya sheria za sekta ya ardhi baada ya kuidhinishwa kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara inaendelea na hatua za marekebisho ya Sheria mbili (**2**) za Sekta ambazo ni Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116 na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138. Katika mwaka 2026/27, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria tatu (**3**) na Kanuni sita (**6**) za sekta ya ardhi kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya

Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la mwaka 2023) na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira.

MIRADI YA MAENDELEO

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (LDI); na Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa.

Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kupima viwanja **15,000**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya viwanja **35,311** sawa na asilimia **235.41** vimepangwa na kupimwa katika halmashauri **13** nchini. Katika mwaka 2026/ 27, Wizara imepanga kupima viwanja **15,000**.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara ilipanga Kuwezesha utekelezaji wa miradi inayohusisha utwaaji wa maeneo na uboreshaji wa miji iliyochakaa katika majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara kupitia programu ya KKK imewezesha uandaaji wa Mwongozo wa Programu ya uendelezaji wa maeneo chakavu ya miji (*Guideline for Land Re-Adjustment in Tanzania*). Katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuhuisha maeneo chakavu ya miji.

72. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuziwezesha halmashauri ili kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi (*Plot Development Revolving Fund* - PDRF) ambao moja ya vyanzo vyake ni marejesho ya fedha shilingi bilioni **50.00** zilizokopeshwa mwaka 2021/22 kwenye halmashauri **57**, Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro, Chuo Kikuu Ardhi na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa (**Jedwali Na. 14**). Hadi tarehe 15 Mei 2026, shilingi bilioni **33.18** zimerejeshwa sawa na asilimia **66.41** ya fedha zilizokopeshwa. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuchukua hatua madhubuti kwa halmashauri

zote ambazo hazijakamilisha kurejesha fedha hizo. **Nitumie fursa hii kuzipongeza halmashauri ambazo zimekamilisha marejesho ya fedha zilizokopeshwa na kuzitaka halmashauri ambazo hazijakamilisha kurejesha mikopo hiyo zifanye hivyo mara moja ili kuziwezesha halmashauri nyingine nchini kunufaika na fursa hiyo.**

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (Land Data Infrastructure - LDI) kwa lengo la kurahisisha kazi za upangaji na upimaji nchini. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kukamilisha ununuzi wa vifaa na kuanza uandaaji wa ramani za msingi za uwiano wa **1:2,500** kwa miji mikuu ya mikoa na uwiano wa **1:25,000** kwa nchi nzima. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imekamilisha kuandaa viwango na miongozo ya uandaaji wa ramani za msingi zitakazotumika kudhibiti ubora wa ramani zitakazoandaliwa na Mkandarasi na wadau wengine wanaotengeneza ramani. Aidha, Wizara imefanikiwa kumpata mkandarasi atakayeleta ndege maalum itakakayotumika kupiga picha za anga zitakazotumika kutengeneza ramani za msingi za uwiano mkubwa katika maeneo yaliyoainishwa kwenye makao makuu ya mikoa. Katika mwaka 2026/27, Wizara inatarajia kumpata Mkandarasi atakayejenga Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **30** (Continuously Operating Reference Stations - CORS) na kuandaa Ramani za Msingi nchi nzima za uwiano mdogo wa **1:25,000**.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo, Wizara imefanikiwa kupandisha hadhi Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mafunzo ya Teknolojia ya Taarifa za Kijiografia (TNGC) kuwa Chuo cha Mafunzo ya Kati. Chuo hiki kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kutoa mafunzo katika Ngazi ya Astashahada. Chuo hicho kitaongeza uwezo wa wataalamu wa ndani kutekeleza miradi ya sekta ya ardhi na hivyo kuokoa matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuajiri wataalam kutoka nje ya nchi na kupeleka watalaam nje ya nchi. Katika mwaka 2026/27, chuo kitaanza kutoa mafunzo kwa wanafunzi **60** katika taaluma za upimaji kwa njia ya satelaiti pamoja na uandaaji

ramani kwa kutumia ndege zisizokuwa na rubani (Satelite Survey and Drone Mapping).

Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kupima, kukarabati alama zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa makubaliano ya uimarishaji wa mipaka. Katika mwaka 2025/26, Wizara ilipanga kuimarisha sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **100** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita **100**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeimarisha Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya kutoka Tarakea Wilaya ya Rombo hadi Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi Wilaya ya Mwanga kwa jumla ya kilomita **106** sawa na asilimia **106** na kufanya jumla ya kilomita zilizoimarishwa kufikia **564** kati ya kilomita **758** za eneo la nchi kavu katika mpaka kati ya Tanzania na Kenya.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ikipata maelezo kuhusu Uimarishaji Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya katika eneo la Holili Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro



Muonekano wa mkuza wa Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya uliopo eneo la Holili Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro

76. ***Mheshimiwa Spika,*** uimarishaji wa mipaka hutegemea makubaliano baina ya nchi na nchi. Ili kuwezesha hayo, Wizara imeshiriki katika mikutano ambayo ni Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama- JPCDS kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji; na Kamati ya Pamoja ya Wataalamu wa uimarishaji mpaka katika ziwa Tanganyika kati ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo- DRC, Tanzania na Zambia yenye lengo la kujadili namna ya kutekeleza zoezi la uimarishaji wa mipaka. Aidha, mafunzo ya pamoja ya wataalamu ya uimarishaji mpaka wa kimaitaifa kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Burundi yanayohusu uhakiki na uimarishaji wa mpaka katika eneo la Mto Malagarasi yamefanyika.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Sheria ya Bahari, nchi zote zinazopakana na bahari na zilizoridhia mkataba huo kabla ya mwaka 1999, zilipewa fursa ya kuwasilisha maombi ya eneo la nyongeza mbele ya Umoja wa Mataifa. Mwaka 2012 Tanzania iliwasilisha maombi ya kuongezewa eneo Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini kwenye Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia mipaka ya Baharini (Commission of the Limits of the Continental Shelf). Eneo linaloombwa linakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba **61,000** (sawa na ukubwa wa mikoa ya Tanga, Pwani na Dar es Salaam kwa pamoja). Umuhimu wa eneo linaloombwa ni

kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali zinazoweza kupatikana katika eneo husika.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Tanzania ilipata fursa ya kutetea andiko hilo mbele ya Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mipaka Baharini (Commission on the Limits of Continental Shelf – CLCS) Jijini New York, Marekani. Kufuatia utetezi huo, Tume ilitoa maoni na mapendekezo ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi na Kikosi Kazi kwa kuzingatia taarifa za kijiolojia, jiofizikia, jiodesia, kihaidrografia na sheria za mipaka ya Bahari. Andiko lililoboreshwa litawasilishwa mbele ya Tume mwezi Julai mwaka huu.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara imepanga kuendelea kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **140**; kuimarisha sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **70**; kupima na kuimarisha kilomita **100** za Mipaka ya Kimataifa kwenye maji; kukamilisha maboresho ya andiko la utetezi kuhusu Eneo la Nyongeza Nje ya Ukanda wa Kiuchumi Baharini; na kuwezesha ukusanyaji na uchakataji wa data zinazohusiana na maji.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

80. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wizara ni kuratibu na kusimamia shughuli za taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini, Baraza la Taifa la Wapima Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini; kufanya tafiti zinazohusu matumizi ya ardhi; pamoja na kufuatilia, kutathmini na kuhakikisha uzingatiaji wa mipango hiyo. Utekelezaji wa majukumu haya unazingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116; na Mpango Mkakati wa Tume (2021/22–

2025/26) uliozingatia Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (2013–2033).

82. ***Mheshimiwa Spika,*** upangaji wa matumizi ya ardhi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali ardhi hasa katika muktadha wa ongezeko la watu, mifugo na mahitaji mbalimbali ya ardhi ikiwemo kilimo, malisho na makazi. Aidha, huchangia kulinda usalama wa milki za ardhi na kudhibiti migogoro ya ardhi nchini. Kupitia mipango hii, maeneo hutengwa kwa matumizi mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji, uwekezaji na makazi ili kuzuia muingiliano wa matumizi hususan katika maeneo nyeti kama shoroba za wanyamapori, mazalia ya wanyamapori, vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi, mapori tengefu, mapori ya akiba pamoja na ardhi ya uwekezaji na malisho. Mipango hii huandaliwa na kutekelezwa katika ngazi mbalimbali kuanzia Taifa, kanda, mikoa, wilaya na vijiji.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Namagondo kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, akiwasilisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Mpangokina wa kijiji mbele ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Kaspar Kaspar Mmuya.

Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **240** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **253** katika halmashauri za wilaya **24** nchini

imeandaliwa sawa na asilimia **105.42** ya lengo na kufanya jumla ya vijiji vilivyopangwa kufikia **4,925** kati ya vijiji **12,333** vilivyopo nchini (**Jedwali Na. 15**). Kati ya vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi, vijiji **2,750** sawa na asilimia **55.83** vimepangwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Katika mwaka 2026/27, Tume kwa kushirikiana na wadau itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,492**. **Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuongeza tengeo la bajeti kwa ajili ya kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Aidha, tengeo hilo litawezesha upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji vingi kwa muda mfupi ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Hii inadhihirisha azma ya Mheshimiwa Rais ya kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi nchini na kurejesha tabasamu kwa Watanzania**

84. ***Mheshimiwa Spika***, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi uliotekelezwa na Tume umewezesha uhakiki na utatuzi wa migogoro ya mipaka ya vijiji **223** katika halmashauri za wilaya **20** ambazo ni Nanyumbu (**13**), Mtwara (**19**), Mtama (**5**), Bahi (**10**), Nyang'hwale (**6**), Mbogwe (**4**), Sikonge (**17**), Nzega (**44**), Simanjiro (**2**), Kilolo (**3**), Gairo (**19**), Masasi (**13**), Mbeya (**2**), Misungwi (**10**), Kisarawe (**6**), Muheza (**11**), Busega (**10**), Morogoro (**12**), Mpwapwa (**10**) na Kiteto (**7**). Aidha, uchambuzi umebaini kuwa miongoni mwa vyanzo vya migogoro hiyo ni mgongano wa maslahi na mgawanyo wa rasilimali kutokana na kuanzishwa kwa maeneo mapya ya kiutawala; kutokuwepo kwa alama za kudumu za mipaka; na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mipaka ya vijiji. Hali hii husababisha migongano ya matumizi ya ardhi na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo; hifadhi za wanyamapori, vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi, mapori ya akiba na mapori tengefu.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini unaratibiwa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji. Hivyo, ni wajibu wa Mamlaka za Upangaji kuhakikisha zinaweka masuala ya mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vipaumbele vyao. **Natoa wito kwa Mamlaka za Upangaji kuhakikisha**

zinatenga fedha kwa ajili ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhakikisha wanazingatia mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandaliwa kwenye maeneo yao.

Uandaaji wa Mipangokina

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuwezesha uandaaji wa Mipangokina katika vitovu vya vijiji na maeneo ya mashamba kwa lengo la kurahisisha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila. Katika mwaka 2025/26, Tume ilipanga kuandaa Mipangokina sita (**6**) pamoja na kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila **2,000** kwa maeneo ya makazi na mashamba. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya Mipangokina **34** imeandaliwa katika maeneo ya makazi na mashamba kwenye halmashauri za wilaya nane (**8**) nchini. Utekelezaji huu umewezesha kutolewa kwa Hati za Hakimiliki ya Kimila **6,231** sawa na asilimia **316.05** ya lengo katika wilaya mbalimbali zikiwemo Rungwe (**739**), Ushetu (**1,022**), Sikonge (**1,156**), Urambo (**333**), Kaliua (**323**), Nyang'hwale (**838**), Ukerewe (**1,308**) na Mlimba (**512**). Katika mwaka 2026/27, Tume itaandaa Mipangokina katika vijiji **145** kwenye maeneo ya makazi na mashamba itakayowezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila **87,000**.

Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Upangaji

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Tume ilipanga kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **248** katika ngazi za wilaya na vijiji pamoja na kutoa elimu kuhusu sheria za ardhi, miongozo na taratibu za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Tume imefanikiwa kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji **277** sawa na asilimia **111.69** ya lengo zikiwemo halmashauri za vijiji **253** na halmashauri za wilaya **24** kuhusu masuala ya uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi yenye wajumbe **21,721** wa Kamati za Usimamizi wa Ardhi ngazi ya wilaya (**192**), wajumbe wa halmashauri za vijiji (**5,819**), Wajumbe wa Kamati za Usimamizi wa Ardhi ya Vijiji (**2,024**), Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji (**11,771**), Wajumbe wa Kamati za Uhakiki wa Mipaka (**1,771**) pamoja na Wajumbe wa Kamati za Uhakiki wa Maslahi ya Ardhi (**144**). Aidha, elimu ilitolewa kuhusu usuluhishi wa migogoro ya ardhi, uhifadhi wa mazingira, ulinzi wa

mapitio ya wanyamapori, vyanzo vya maji, uzingatiaji wa matumizi yaliyopangwa ya ardhi pamoja na uhifadhi wa misitu ili kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. **Natoa wito kwa wadau wa kisekta na Mamlaka za Upangaji kuhakikisha maeneo yaliyopangwa yanaandaliwa Mipangokina na kuwekewa miundombinu ili kuepusha uvamizi na migogoro ya ardhi. Aidha, mamlaka za upangaji ziendelee kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote wanaokiuka mipango ya matumizi ya ardhi iliyopo.**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na kasi ya mabadiliko na maendeleo ya teknolojia katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya ardhi kwa wakati, matumizi ya teknolojia za kisasa hayakwepeki. Kutokana umuhimu huo, Wizara kupitia Tume inaendelea kuhuisha kanzidata ya mipango ya matumizi ya ardhi na Mfumo wa Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Mfumo huu utawawezesha wadau kusajili mipango ya matumizi ya ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi na hivyo kuwezesha uratibu na usimamizi Madhubuti wa wadau wote wanaohusika na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini. Hadi tarehe 15 Mei 2026, jumla ya Mipango ya Matumizi ya ardhi ya vijiji **590** imehifadhiwa kwenye Mfumo na kufanya kuwa na jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **2,584** iliyohifadhiwa kwenye mfumo. Aidha, mafunzo ya uandaaji wa Mipangokina ya matumizi ya ardhi kidijiti yametolewa kwa wajumbe **64** wa Timu za Usimamizi wa Ardhi za Wilaya (PLUM Team) za halmashauri za wilaya nane (**8**) ambazo ni Urambo, Kaliua, Sikonge, Ushetu, Nyangh'wale, Rungwe, Ukerewe na Mlimba.

Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Tume ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji **40**, hususan katika maeneo ya miradi ya kimkakati (SGR, EACOP, JNHPP), wilaya za mipakani na vijiji vyenye migogoro. Hadi tarehe 15 Mei 2026, zoezi limefanyika katika vijiji **33** ndani ya Halmashauri **11** za Handeni (**4**), Wanging'ombe (**4**), Tarime (**4**), Meatu (**4**), Shinyanga (**5**), Sumbawanga (**1**), Musoma (**1**), Butiama (**1**), Makete (**1**), Chato (**4**) na Mbarali (**4**). Matokeo

yanaonesha kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi umechangia kupungua kwa migogoro ya ardhi kwa wastani wa asilimia **71**, kuimarika kwa uhifadhi wa mazingira kwa asilimia **79** na kufikiwa kwa asilimia **83** ya utekelezaji wa matumizi yaliyopangwa kwa maeneo ya makazi, kilimo, huduma za jamii na miundombinu. Mafanikio haya yanatokana na uwepo wa mipango elekezi pamoja na ufuatiliaji katika maeneo ya miradi ya kimkakati.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini pia imebaini kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya malisho na misitu ya hifadhi bado uko chini ya kiwango kinachotarajiwa kutokana na changamoto za usimamizi, uvamizi wa ardhi na ukosefu wa mifumo endelevu ya kiuchumi. Katika mwaka 2026/27, Tume itafanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **232** katika miradi ya kimkakati (SGR, EACOP, JNHPP), vijiji vilivyopo katika wilaya za mipakani mwa Tanzania na nchi jirani pamoja na vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi ili kuongeza uzalishaji. Vilevile, Tume itaimarisha ufuatiliaji wa kidijiti kwa kutumia mifumo ya taarifa za kijiografia (GIS), kuanzisha viashiria mahsusi vya kupima utendaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi endelevu ya maeneo ya malisho na misitu ili kuongeza tija, mapato na kupunguza migogoro.

Shirika la Nyumba la Taifa

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali; kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kusimamia milki za majengo; kufanya ukarabati wa nyumba; kukusanya kodi ya pango la nyumba za Shirika; kutoa huduma ya ushauri elekezi; upangaji wa maeneo ya ujenzi wa nyumba; na kutekeleza kazi za ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 11 (2015/16 – 2025/26).

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa limeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **5,000** wa Samia Housing Scheme unaotarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni **466**.

Katika mwaka 2025/26, Shirika lilipanga kuendelea na awamu ya pili ya utekelezaji wa Mradi wa Samia Housing Scheme kwa kujenga nyumba **908** katika maeneo mbalimbali nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, ujenzi wa nyumba **68** za makazi eneo la Iyumbu (Dodoma) umekamilika hivyo kufanya jumla ya nyumba zilizokamilika kufikia **628.** Aidha, ujenzi wa nyumba **260** katika eneo la Mtoni Kijichi umefikia asilimia **30**, ujenzi wa nyumba **160** eneo la Medeli (Dodoma) umefikia asilimia **25** na nyumba **100** Iyumbu awamu ya pili imefikia asilimia **5.** Kadhalika, maandalizi ya ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Njedengwa (Dodoma), Kawe na 105 Boulevard Residence (Dar es Salaam) yanaendelea.



Mradi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa wa Samia Housing Scheme uliopo eneo la Kawe jijini Dar es Salaam



Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) katika eneo la Kijichi jijini Dar es Salaam

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kukamilisha ujenzi wa miradi iliyokuwa imesimama katika Mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo nyumba **422** katika Mradi wa Kawe 711 wenye thamani ya shilingi bilioni **169**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa mradi huu umefikia asilimia **85** ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni 2026. Aidha, ujenzi wa nyumba **196** katika Mradi wa *Golden Premier Residence (GPR)* wenye thamani ya shilingi bilioni **127** umefikia asilimia **50** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027. Vilevile, ujenzi wa mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* upo katika hatua ya zabuni.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa miradi **21** ya ubia yenye thamani ya shilingi bilioni **351** na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia Sera ya Ubia. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa usimamizi wa miradi hii unaendelea ambapo miradi mitatu imekamilika na miradi mingine iliyobaki imefikia wastani wa asilimia **56** ya utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwaka 2027. Aidha, maombi mapya ya miradi **68** yenye thamani ya shilingi bilioni **607** yapo katika hatua mbalimbali ambapo miradi **38** inatarajiwa kuanza mwezi Juni 2026 na miradi **30** ipo katika hatua mbalimbali za uchambuzi.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na utwaaji wa miradi ya ubia iliyosimama kwa muda mrefu ili iweze kutekelezwa na Shirika lenyewe kwa mujibu wa mikataba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya miradi ya ubia **24** iliyokuwa imesimama, miradi **13** imekamilika na miradi minne (**4**) inaendelea kusimamiwa na Shirika ili wabia waikamilishe, miradi mitatu (**3**) imetwaliwa na utekelezaji wake utaendelea kuanzia Julai, 2026. Vilevile, miradi mingine minne (**4**) inatarajiwa kutwaliwa ifikapo Juni 2026 katika mikoa ya Mwanza (**2**), Dar es Salaam (**1**) na Iringa (**1**).

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa miradi ya majengo ya

biashara katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Meru View shops (Arusha), Tabora Commercial Complex (Tabora), Singida 2F Plaza (Singida), Mkwakwani Commercial Complex (Tanga), Kashozi Commercial Complex (Kagera), Uluguru Plaza (Morogoro), Iringa Commecial Complex (Iringa) na Uhuru shopping centre- Ilala (Dar es Salaam). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa mradi wa Meru View Shops (Arusha) umefikia asilimia **52**; Tabora Commercial Complex (Tabora) umefikia asilimia **46**; Singida 2F Plaza (Singida) umefikia asilimia **85**; Mkwakwani Commercial Complex (Tanga) umefikia asilimia **40**; Kashozi Commercial Complex (Kagera) umefikia asilimia **65**; Uluguru Plaza (Morogoro) umefikia asilimia **42**; na Iringa Commercial Complex (Iringa) umefikia asilimia **40**.



Mradi wa ujenzi wa jengo la biashara katika eneo la Mkwakwani mkoani Tanga (Mkwakwani Commercial Complex)

97. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuanza ujenzi wa miradi mipya katika miji na halmashauri mbalimbali ikiwemo jengo la matumizi mchanganyiko mkoani Ruvuma, majengo ya biashara na ofisi – Masasi, Lindi, Usa River na Ngarenaro. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa jengo la matumizi mchanganyiko mkoani Ruvuma uko katika hatua ya ujenzi wa msingi, miradi ya Usa River na Ngarenaro maandalizi ya ujenzi yako hatua za mwisho. Aidha, Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo ya biashara na ofisi ya Mtanda (Lindi), Zongomela (Kahama) na

Masasi Commercial Complex (Masasi- Mtwara). Vilevile, ujenzi wa maghala tisa (**9**) kwa ajili ya kupangisha katika Manispaa ya Mtwara umeanza ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi wa maghala matatu (**3**) unaendelea na umefikia asilimia **78**.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na kuanza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miradi ya vitovu vya miji vikiwemo Mwashiwawala (Songwe), Kwala (Pwani), Urafiki na Salama Creek (Dar es Salaam) ifikapo Juni, 2026. Nalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upembuzi yakinifu katika miradi ya Mwashiwawala na Usa River, Salama Creek umekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu katika eneo la Kwala na Urafiki unaendelea na utakamilika mwezi Juni, 2026.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea kukusanya madeni ya kodi ya nyumba, miradi ya ukandarasi, uuzaji wa nyumba, viwanja na madeni mengineyo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei 2026, Shirika limepunguza madeni hayo kutoka shilingi bilioni **27.98** mwaka 2024/25 hadi shilingi bilioni **19** mwaka 2025/26. **Nitumie fursa hii kuwataka wadaiwa wote kutekeleza wajibu wao wa kulipa madeni yao kabla Shirika halijachukua hatua kali za kisheria.**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kukarabati nyumba za Shirika **1,600**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Shirika limekarabati nyumba **1,283** sawa na asilimia **80** ya lengo. Aidha, ukarabati wa nyumba **317** uko katika hatua za mwisho za utekelezaji.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilipanga kuendelea na ujenzi wa miradi ya ukandarasi na ushauri elekezi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa majengo nane (**8)** ya Ofisi za Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba umekamilika na kukabidhiwa kwa washitiri. Aidha, usanifu na ujenzi wa jengo la soko la madini (Tanzanite) eneo la Mirerani Manyara umekamilika**.** Vilevile, ujenzi wa miradi ya ukandarasi na utaalamu elekezi wa majengo ya Ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) jijini

Dodoma umefika asilimia **73** na Zanzibar umefikia asilimia **50**. Kadhalika, Shirika limeanza kutoa ushauri elekezi katika miradi mipya ya ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) jijini Dodoma.

102. *Mheshimiwa Spika,* ili kuwezesha upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu, Shirika linaendelea kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa awamu ambapo utekelezaji utaanza mwaka 2026/27 katika mradi wa Salama Creek (Kigamboni, Dar es Salaam), Sabasaba (Morogoro), Iyumbu (Dodoma) na Buswelu (Mwanza). **Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na mamlaka zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ya umeme, maji na barabara kuunga mkono jitihada za Shirika kwa kuwezesha upatikanaji wa ardhi na miundombinu ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba katika maeneo ya utekelezaji.**

103. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/ 27, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kuendelea na ujenzi wa nyumba katika Mradi wa nyumba **5,000** wa *Samia Housing Scheme* katika maeneo ya Mtoni Kijichi na Kawe (Dar es Salaam) na Medeli na Iyumbu (Dodoma). Aidha, Shirika litaanza ujenzi wa nyumba katika maeneo ya Njedengwa (Dodoma), Urafiki (Dar es Salaam), Sokoine complex (Mtaa wa Azimio- Arusha) na Makongoro (Mwanza);
ii) Kuanza ujenzi wa nyumba **800** za gharama nafuu kwa awamu katika mradi wa Salama Creek (Kigamboni, Dar es Salaam), Sabasaba (Morogoro), Iyumbu (Dodoma) na Buswelu (Mwanza);
iii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **196** katika mradi wa Golden Premier Residence (GPR) na Kiwanja Na.300 Regent Estate;
iv) Kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya ubia na kukaribisha wawekezaji wengine kutoka sekta binafsi na zile za Umma ili kufanya uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi kupitia Sera ya Ubia;
v) Kuendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya majengo ya biashara katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Meru view

shops, Ngarenaro na Usa River (Arusha), Tabora Commercial Complex (Tabora), Mkwakwani Commercial Complex (Tanga), Uluguru Plaza (Morogoro), Iringa Commercial Complex (Iringa), Songea Commercial Complex (Ruvuma); Bukoba Complex (Kagera), 17A mwenge na 1K Market Street (Singida), Uganda Avenues na RAS Kilomoni (Dar es Salaam).

vi) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa miradi ya vitovu vya miji ikiwemo Kwala (Pwani) na Salama Creek (Dar es Salaam);

vii) Kuendelea kutekeleza mpango wa ukarabati wa nyumba za Shirika **2,200**; na

viii) Kutekeleza miradi ya ukandarasi na Ushauri elekezi inayoendelea na mingine itakayojitokeza.

BODI ZA USAJILI WA WATAALAM WA FANI ZA ARDHI

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inasimamia utekelezaji wa shughuli za Bodi mbalimbali za wataalam wa sekta ya ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kusimamia maadili ya kitaaluma.

Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji

104. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji ilianzishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Sura ya 426. Lengo kuu ni kusajili, kusimamia maadili na taaluma pamoja na kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu taaluma ya mipangomiji nchini. Katika mwaka 2025/26, Bodi ilipanga kusajili Wataalam na Kampuni za Mipangomiji zitakazokidhi vigezo ili kuimarisha utendaji kazi pamoja na kusimamia na kufuatilia utendaji kazi katika mikoa **26**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Bodi imesajili wataalam **98** na kampuni tatu (**3**) na hivyo kufikia jumla ya watalaam **610** na kampuni **102** zilizosajiliwa tangu Bodi ilipoanzishwa. Aidha, ufuatiliaji wa utendaji kazi umefanyika katika mikoa **15** ya Dar es salaam, Mwanza, Iringa, Njombe, Arusha, Kilimanjaro, Singida, Tabora, Kigoma, Mara, Simiyu, Ruvuma, Songwe, Mbeya na Mtwara na kazi inaendelea katika mikoa **11**. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wataalam wa Mipangomiji **96** na Kampuni tisa

(**9**) na kuendelea kusimamia na kufuatilia utendaji kazi na uzingatiaji wa Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji katika mikoa **26**.

Bodi ya Usajili wa Wathamini

106. ***Mheshimiwa spika,*** Bodi ya Usajili wa Wathamini ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura ya 138 kwa ajili ya kusajili Wathamini na kudhibiti kazi za uthamini nchini. Aidha, Bodi inahusika na utoaji wa leseni kwa wataalam wa uthamini, kusimamia nidhamu na maadili ya taaluma na kuhimiza maendeleo ya elimu na uzoefu katika tasnia ya uthamini.

107. ***Mheshimiwa spika,*** katika mwaka 2025/26, Bodi ya Usajili wa Wathamini ilipanga kusajili wathamini **150** katika ngazi zote, kutengeneza mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Bodi, kufanya mapitio ya mitaala na kukusanya shilingi bilioni **1.70** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Bodi imekamilisha usanikishaji wa mfumo, mapitio ya mitaala na kusajili Wathamini **145** sawa na asilimia **96.67** ya lengo. Kati ya hao, Wathamini wawili (**2**) katika usajili kamili, Wathamini **99** katika ngazi ya usajili wa awali, Wathamini **44** wameorodheshwa kama Wathamini Wasaidizi na Kampuni tatu (**3**) za uthamini zimesajiliwa. Aidha, Bodi ilipokea na kuamua masuala **10** ya kimaadili na nidhamu. Kati ya hayo, masuala matano (**5**) yanahusu Wathamini na matano (**5**) yanahusu kampuni za uthamini. Vilevile, Bodi ilikusanya shilingi bilioni **1** kutoka kwenye ada za usajili, ada ya kila taarifa ya uthamini na ada ya mitihani ya kitaaluma sawa na asilimia **58.82** ya lengo. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wathamini **150** katika ngazi mbalimbali za usajili na Kampuni **10** za Uthamini. Pia, Bodi itaendelea kusimamia maadili ya kazi kwa Wathamini na Kampuni zilizosajiliwa ili kuhakikisha kazi za uthamini zinafanyika kwa weledi na ufanisi. Aidha, Bodi imepanga kukusanya shilingi bilioni **1.40**.

Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Usimamizi na Usajili wa Wapima Ardhi inakuza na kusimamia tasnia ya upimaji ardhi nchini. Katika mwaka 2025/26, Bodi ilipanga kusajili Wapima Ardhi **100** na kutoa

leseni kwa kampuni za upimaji **30**. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wapima Ardhi **93** wamesajiliwa sawa na asilimia **93** ya lengo na hivyo kuwa na jumla ya Wapima Ardhi **920** waliosajiliwa nchini. Aidha, kampuni **10** zimesajiliwa sawa na asilimia **33.33** ya lengo na hivyo kufanya Kampuni za Upimaji Ardhi zilizosajiliwa kufikia **138**. Vilevile, Bodi imeendelea kuandaa na kutoa mafunzo ya kitaalam kwa Wapima Ardhi kupitia semina, mikutano na makongamano mbalimbali ya kitaaluma ambapo Wapima Ardhi **250** walishiriki mafunzo hayo. Kadhalika, Bodi imeendelea kuchukua hatua kwa Wapima Ardhi na Kampuni za Upimaji Ardhi zilizobainika kukiuka maadili ya taaluma ya upimaji ardhi ambapo kampuni mbili (**2**) zimepewa onyo. Katika mwaka 2026/27, Bodi imepanga kusajili Wapima Ardhi **100** na kutoa leseni kwa Kampuni za Upimaji Ardhi **20**.

VYUO VYA ARDHI TABORA NA MOROGORO

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro ambavyo hutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali za ardhi, kufanya utafiti katika fani za sekta ya ardhi na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya ardhi.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Chuo cha Ardhi Tabora kilipanga kudahili wanafunzi **1,580**; kujenga sehemu ya uzio yenye urefu wa mita **410** kati ya mita **1,331**; na kukamilisha ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara (Lecture theatres) zenye uwezo wa kubeba wanafunzi **700** kwa wakati mmoja. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wanafunzi **1,138** sawa na asilimia **85.49** wamedahiliwa. Aidha, ujenzi wa uzio wenye urefu wa mita **410** umekamilika na ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara (Lecture theatres) umefikia asilimia **65**. Katika mwaka 2026/27, Chuo kimepanga kudahili wanafunzi **1,500** katika fani tano (**5**) zinazotolewa na Chuo; kuendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia; kuhuisha mitaala ya kozi za *Geographical Information System* na *Environmental Management* na kuanzisha mitaala mipya ya *Geomatics* pamoja na *Regional and Rural Planning*; kununua mashine ya kuchapisha makala kwa ajili ya kiwanda cha uchapishaji; na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya uzio wa Chuo yenye urefu wa mita **410** kati ya mita **921** zilizobaki.



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akielezwa hatua za upimaji kwa vitendo wakati wa Mahafali ya Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA)



Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi akipokea zawadi ya picha ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyochorwa na Mwanafunzi wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) wakati wa mahafali ya chuo hicho

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Chuo cha Ardhi Morogoro, kilipanga kudahili wanafunzi **768**; kujenga vyumba viwili (**2**) vya madarasa; kuimarisha Maabara ya Kompyuta; kujenga uzio katika eneo la chuo; na kufanya ukarabati wa majengo. Hadi tarehe 15 Mei 2026, wanafunzi **574** wamedahiliwa sawa na asilimia **74.74** ya lengo. Aidha, ujenzi wa vyumba viwili (**2**)

vya madarasa umefikia asilimia **60**. Vilevile, Chuo kinaendelea na ujenzi wa sehemu ya uzio yenye urefu wa mita **120** kati ya mita **587** na uimarishaji wa Maabara ya Kompyuta unaendelea. Kadhalika, Chuo kimeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kukarabati mabweni mawili (**2**) ya wanafunzi na jengo la Zahanati ya Chuo. Katika mwaka 2026/27, Chuo kimepanga kudahili jumla ya wanafunzi **800**; kuboresha miundombinu pamoja na kuongeza matumizi ya TEHAMA; kutekeleza miradi ya ushauri wa kitaalamu; kupanda miti **1,000**; na kujenga uzio wenye urefu wa mita **120** kati ya **467** zilizobaki.

UTAWALA NA RASILIMALIWATU

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu ni nguzo muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa katika maeneo yanayohusiana na masuala ya uendeshaji wa Ofisi, ajira, maendeleo ya kitaaluma, usimamizi wa utendaji kazi na masuala ya ustawi wa watumishi. Katika mwaka 2025/26, Wizara imepokea watumishi **483** wa ajira mpya ambao wameongeza tija na ufanisi, imejaza nafasi nane (**8**) za uongozi na inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi **468** na kubadilisha kada watumishi nane (**8**). **Naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia watumishi wapya ambao wataongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi nchini.**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuwawezesha watumishi kushiriki mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambapo hadi tarehe 15 Mei 2026, watumishi **1,288** wamepatiwa mafunzo. Kati ya hao, watumishi **65** wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na ***watumishi* 1,223** ya muda mfupi. Lengo ni kuwajengea uwezo na kuongeza weledi katika utekelezaji wa majukumu.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi kufanya kazi katika mazingira bora kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa na vitendea kazi katika utoaji wa huduma. Katika kufanikisha lengo hilo, hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imenunua magari saba (**7**) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma. Aidha, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam awamu ya kwanza umekamilika. Vilevile, ujenzi wa

jengo la Makao Makuu ya Wizara lenye uwezo wa kuhudumia watumishi zaidi ya **350** umekamilika na kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2025.



Jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi lililopo eneo la Mtumba jijini Dodoma

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha utendaji wenye tija na ufanisi wa huduma kwa wananchi kwa kutoa elimu kwa watumishi kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza watumishi kuwajibika ipasavyo na kwa wakati, kusimamia matumizi sahihi ya mifumo ya usimamizi wa Ardhi, upimaji utendaji kazi kwa watumishi wa umma (e- Utendaji), Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi), Mfumo wa barua pepe za Serikali (GMS), Mfumo wa Utunzaji wa kumbukumbu wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi (eMrejesho), Mfumo wa kutathmini mahitaji ya watumishi wa e-Msawazo (HR-Assessment) na matumizi ya Kituo cha Huduma kwa Wateja.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaothibitika kufanya makosa au kutekeleza majukumu yao kinyume na Sheria na taratibu zilizopo ambapo hatua za awali za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya watumishi watano (**5**) waliotuhumiwa kukiuka maadili, weledi, sheria na kanuni za utumishi wa umma na kukutwa na tuhuma za kusababisha migogoro ya ardhi. Kamati za uchunguzi mbili (**2**) zimeundwa ili kuchunguza tuhuma hizo kwa mujibu wa kanuni ya 36 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, ili kuchukua

hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni ya 42 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022. **Nawaelekeza watumishi wote wa sekta ya ardhi kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia utu na maadili ya utumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi kikamilifu kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Wizara haitamvumilia mtumishi yeyote atakayekiuka maadili ya kazi kwa kukwamisha nia na dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutoa huduma bora za ardhi kwa Watanzania.**

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi pamoja na kuwekea mkazo katika uwajibikaji, usimamizi wa misingi ya uadilifu na weledi katika utoaji wa huduma bora za ardhi nchini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi **460**, kupandisha vyeo watumishi **672** na kubadilisha kada watumishi **13**. Aidha, Wizara itawawezesha watumishi **1,272** kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wakiwemo watumishi **460** wa ajira mpya.

HABARI NA ELIMU KWA UMMA

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 26, Wizara na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu ya kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni, majarida, tovuti na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuongeza uelewa, ushiriki na upatikanaji wa huduma za sekta ya ardhi kwa wananchi. Hadi tarehe 15 Mei 2026, Wizara imeshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Kilimo ya Nanenane pamoja na Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Kifedha. Aidha, kupitia kipindi cha televisheni cha **"Maisha ni Nyumba"** kinachorushwa kupitia kituo cha ITV, jumla ya vipindi **52** vimeandaliwa na kurushwa. Wizara imeshiriki katika vipindi **183** vya televisheni mbalimbali nchini pamoja na vipindi **428** vya redio. Aidha, machapisho **16,218** yaliandaliwa na kusambazwa ambapo jumla ya wananchi **14,310,111** wamefikiwa.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendesha kampeni maalum ya kutoa elimu kwa wanawake kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi ijulikanayo kama Samia Ardhi Kliniki iliyoongozwa na kaulimbiu

isemayo ***"Mwanamke, Haki Yako, Miliki Ardhi Sasa"***. Lengo lilikuwa kuongeza uelewa, hamasa na umiliki wa ardhi kwa wanawake. Kampeni hiyo ilifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake yanayoadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi. Kupitia kampeni hiyo, wananchi **16,864** walihudumiwa.



Bi. Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (katikati) akishuhudia mkazi wa Dar es Salaam akikabidhiwa Hati wakati wa Samia Ardhi Kliniki

120. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara na wadau katika utoaji wa huduma za ardhi, katika mwaka 2026/27 Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sekta ya ardhi kupitia vipindi mbalimbali vya redio na televisheni, majarida, tovuti, mitandao ya kijamii pamoja na maonesho ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Wizara itaandaa semina kwa watu **100** wenye mahitaji maalum; Kampeni mbili (**2**) za kuhamasisha usalama wa milki za ardhi; mkutano na wahariri wa vyombo vya habari; kusambaza jumbe fupi za maandishi (SMS); na kusambaza vipeperushi **62,150** kupitia makongamano na kampeni.

USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi katika upangaji miji, urasimishaji makazi, upimaji, uthamini na uendelezaji milki. Ushiriki wa sekta binafsi umewezesha urasimishaji kwenye mitaa mbalimbali nchini yenye makazi yasiyopangwa, uthamini

wa kawaida wa mali, uratibu na usimamizi wa shughuli za uwakala. Aidha, sekta hii imeendelea kushiriki katika maboresho ya sera, sheria na kanuni mbalimbali na kutoa maoni kuhusu namna bora ya kusimamia sekta ya ardhi.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote kutoka sekta binafsi wakiwemo Chama cha Wapima Ardhi Tanzania (IST), Chama cha Wataalam wa Mipangomiji Tanzania, Chama cha Wataalam wa Milki Tanzania (AREPTA), Chama cha Wanasheria Tanzania (TLS), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) na Asasi za Kiraia (CBOs) kwa ushiriki wao katika kutekeleza majukumu ya sekta. Ushiriki wao katika upangaji, upimaji na uthamini wa mali; Kliniki za Ardhi; na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi umeongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi. Wizara inaahidi kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu ili kufikia malengo yaliyowekwa.

SHUKRANI

123. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bi. Evelyne Baruti Mugasha, Mthamini Mkuu; Bi. Stella Chaggi Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; na Bw. Joseph Constantine Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi; na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa juhudi na maarifa ili kufikia malengo ya Wizara.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani na pongezi za dhati kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Masasi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa jukumu

la kuwawakilisha Bungeni. Kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu na hasa mke wangu Bi. Grace Akwilapo na watoto wangu Catherine Akwilapo, Felix Akwilapo na Emmanuel Akwilapo pamoja na wajukuu zangu kwa upendo, ushauri, uvumilivu na kunitia moyo wakati wote nikiwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zimeendelea kunipa nguvu katika kutekeleza majukumu niliyonayo.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, *Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources for Development (RCMRD), Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC), Watumishi Housing Company*, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), *Association for Development of Protected Areas* (ADAP), Taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mzuri waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika, wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali.

HITIMISHO

126. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2026/27, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Hotuba hii. Aidha, kwa mara nyingine nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mnaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pamoja na hotuba hii, yameambatishwa majedwali ambayo yanafafanua kwa kina shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni www.lands.go.tz.

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2026/27

127. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha utekelezaji wa vipaumbele na Mpango wa Bajeti wa Wizara kwa mwaka 2026/27, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha bajeti ya jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili na kumi, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tisa, Mia Tano Kumi na Tano Elfu** (**Shilingi 210,259,515,000**) kwa ajili ya matumizi ya mafungu yote mawili (**Fungu 48** - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) na (**Fungu 03** - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi) kwa mchanganuo ufuatao: -

Shilingi Bilioni Mia Moja, Milioni Mia Mbili Ishirini na Nne, Mia Tano Hamsini na Tatu Elfu (Shilingi 100,224,553,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Nne, Mia Tano Hamsini Elfu (Shilingi 61,134,550,000)** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE) wa Wizara na Tume na Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Tisini, na Tatu Elfu (Shilingi 39,090,003,000) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); na

ii) **Shilingi Bilioni Mia Moja na Kumi, Milioni Thelathini na Nne, Mia Tisa Sitini na Mbili Elfu (Shilingi 110,034,962,000)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **Bilioni Arobaini na Nne, Milioni Mia Moja Thelathini na Mbili, Mia Nne Sitini na Tisa Elfu (Shilingi 44,132,469,000)** ni Fedha za Ndani na Shilingi **Bilioni Sitini na Tano, Milioni Mia Tisa na Mbili, Mia Nne Tisini na Tatu Elfu (Shilingi 65,902,493,000)** ni Fedha za Nje.

Mchanganuo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 48) na Tume (Fungu 03) kwa mwaka 2026/27

	AINA YA MATUMIZI	**FEDHA ZINAZOOMBWA**
A	**Mapato ya Serikali**	
	i) Fungu 48	300,000,000,000
	ii) Fungu 03	18,000,000
	Jumla (A)	**300,018,000,000**
	MAKISIO YA MATUMIZI FEDHA ZINAZOOMBWA	
B	**Matumizi ya Kawaida**	
	Mishahara (PE) - Fungu 48	56,711,082,000

	Mishahara (PE) - Fungu 03	4,423,468,000
	Jumla ya Mishahara (PE)	**61,134,550,000**
	OC – Fungu 48	33,803,211,000
	OC – Fungu 03	5,286,792,000
	Jumla ya OC	**39,090,003,000**
	Jumla (B)	**100,224,553,000**
C	**Matumizi ya Maendeleo**	
	Fedha za Ndani - Fungu 48	5,732,469,000
	Fedha za Ndani - Fungu 03	38,400,000,000
	Jumla ya Fedha za Ndani	**44,132,469,000**
	Fedha za Nje - Fungu 48	65,902,493,000
	Jumla (C)	**110,034,962,000**
	JUMLA KUU (B+C)	**210,259,515,000**

128. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja umeitoa na imeungwa mkono. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Ninalo tangazo la wageni wa Naibu Waziri Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Elineema Gladson Kweka, ambaye ni Mwekezaji wa Sekta ya Madini anayetokea Ruangwa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Bwana Shabani Mohammed Msham, ni Mfanyabiashara kutoka Jimbo la Ruangwa, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya kupokea taarifa ya mtoa hoja, nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwa niaba yake, karibu Mheshimiwa Mary Masanja, Makamu Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

MHE. MARY F. MASANJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa za Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa Misingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya tatu inayofafanua Maoni na Ushauri wa Kamati unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha Taarifa ya Uchambuzi wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi. Msingi wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Ardhi unatokana na Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka, 2025. Kanuni ya 121(4) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya uchambuzi wa taarifa. Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha

2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo:-

(i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kufikia mwezi Februari, 2026;

(iii) Utekelezaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini. Kwa kuzingatia, masharti ya Kanuni ya 120(1)(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03). Sehemu hii inafafanua mambo manne yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa na fedha za Bunge;

(iii) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli; na

(iv) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Tarehe 29 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, mambo manne yamezingatiwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Aidha, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa maoni matatu yafuatayo:-

(i) Katika Programu ya KKK, Kamati ilishauri Serikali kuongeza kasi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha kufikia viwanja 100,000 ifikapo Juni, 2026. Taarifa ya Utekelezaji ilionesha kuwa, upimaji umefikia viwanja 24,236 sawa na 24% ya lengo. Kamati haikuridhishwa na kasi hii kwani haioneshi uwezekano wa kufikia lengo la viwanja 100,000 ifikapo Juni, 2026. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa lengo linafikiwa ili kuongeza mapato;

(ii) Serikali kushindwa kuonesha hatua za kisheria zilizochukuliwa kwa wawekezaji 31 waliobainika kutozingatia masharti ya umiliki wa ardhi; na

(iii) Serikali kushindwa kuirejeshea Wizara ya Ardhi 20% ya makusanyo yanayotokana na kodi ya pango la ardhi *(land rent)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili ya Kilimanjaro na Tanga, na kukagua miradi minne inayotekelezwa na Wizara kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Uimarishaji Mipaka ya Kimataifa: kipande cha IV na V Tarakea (Rombo) hadi Mkomazi (Mwanga);

(b) Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe;

(c) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makazi na Biashara la *Mkwakwani Commercial Complex* chini ya *NHC*; na

(d) Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Halmashauri ya Mji wa Muheza

Mheshimiwa Naibu Spika, yatokanayo na ukaguzi. Katika ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha, tathmini ya kina imebainika kuwa, baadhi ya halmashauri kutorejesha fedha za mkopo za Mradi wa KKK kwa wakati na wengine kuzitumia kwa matumizi tofauti, na hivyo kuzinyima halmashauri nyingine fursa ya kupata mkopo huo, wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini hawana elimu juu ya matumizi ya mfumo wa *e-Ardhi* pamoja na Mfumo wa *TAUSI* na hivyo kukosa fursa zinazopatikana kwenye mifumo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa miundombinu muhimu kama barabara, maji na umeme kwenye baadhi ya maeneo ya Mradi wa KKK kunapunguza hamasa na kasi ya wananchi kununua maeneo na kuyaendeleza na mwisho baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa na hivyo kuleta ugumu kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 48 lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 290 na Fungu 03 lilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 1.018. Hadi kufikia mwezi Mei, 2026 Wizara (Fungu 48) ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 191.9 sawa na 66.17%; na Tume (Fungu 03) ilikuwa imekusanya shilingi milioni 243.3 sawa na 24% ya lengo. Taswira ya ukusanyaji inaonekana kwenye kielelezo kilichowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Wizara (Fungu 48) umefikia 66.17% ya lengo na Tume imefikia 24% ya lengo. Kwa kuzingatia muda uliotumika na makusanyo, Kamati haioni ni kwa namna gani Wizara inaweza kufikia lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) iliidhinishiwa shilingi bilioni 217.5 ambapo shilingi bilioni 91.3 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 126.1 ni fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) iliidhinishiwa shilingi bilioni 12.7 ambapo shilingi bilioni 8.18 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4.5 ni fedha za maendeleo. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Fungu 48 – Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ilikuwa imepokea shilingi bilioni 124.99. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 34.68 sawa na 64.45% ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 24.67 sawa na 65.69% ni matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 65.64 sawa na 94% fedha za ndani za maendeleo. Aidha, fedha za nje za maendeleo hazikupatikana. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha ni kama inavyoonekana katika kielelezo kilichowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umeonyesha yafuatayo:-

(i) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo unaridhisha isipokuwa upatikanaji wa fedha za nje za miradi hauridhishi; na

(ii) Kukosekana kwa fedha za nje kunaweza kusababisha miradi kuathirika na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji unaoweza kuambatana na nyongeza ya gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Hadi kufikia Februari, 2026, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ilikuwa imepokea shilingi bilioni 9.023 sawa na 71% kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.8 sawa na 60% ni fedha za mishahara, na shilingi bilioni 1.68 sawa na 48.24% ni fedha za matumizi mengineyo, na shilingi bilioni 1.5 sawa na 100% ni fedha za miradi ya maendeleo.

Kielelezo namba tatu kinaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali ya upatikanaji wa bajeti ya Tume kuonesha mwelekeo mzuri, bado kiwango kinachotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hakiridhishi katika kufikia lengo la kupanga matumizi ya ardhi kwa kila kipande cha ardhi nchini. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi yote nchini ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48 na Fungu 03) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(iii) Ulinganisho wa bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

(iv) Mambo mahususi yanayogusa sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika majedwali kielelezo namba nne na namba tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika kelelezo cha sita na cha saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mahususi yanayogusa sekta za ardhi. Moja, ukusanyaji wa maduhuli. Ardhi ni rasilimali muhimu ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Serikali. Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara hii kwa ujumla hauridhishi. Jambo hili linapunguza uchangiaji mapato ya ardhi katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha vyanzo na ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa za ardhi za kila mmiliki zinaingia kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji. Vilevile, Serikali ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi nyingine, mfano Mamlaka za Maji, Mfumo wa *e-ardhi* pamoja na mifumo mingine irahisishwe ili wananchi wa kawaida wanufaike nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini, bado changamoto hii ni kubwa. Kamati imebaini kwamba sababu za migogoro hii ni pamoja na kuongezeka kwa ushindani wa matumizi ya ardhi kunakosababishwa na ongezeko la watu, sambamba na ongezeko la shughuli za kibinadamu, ukosefu au kutokuzingatiwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, kutokuwa na mfumo wa kidigitali wa usimamizi wa ardhi katika maeneo yote nchini hali inayorahisisha ardhi kumilikishwa mara mbili *(double allocation),* kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sheria na baadhi ya watumishi wa ardhi kutokuwa waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii isipopatiwa ufumbuzi, migogoro itaendelea kuongezeka na kuathiri ustawi wa maisha ya kila siku ya wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi, uandaaji na mipango ya matumizi bora ya ardhi, usimamiaji sheria, ujenzi na usambazaji wa mfumo wa kidigitali wa kusimamia ardhi nchini ili kuondoa migogoro pamoja na kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupanga, kupima na kumilikisha. Serikali ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 50 kwa halmashauri 57, vyuo vya ardhi vya Tabora, Morogoro, Chuo Kikuu cha Ardhi na Ofisi ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha. Lengo lilikuwa ni kuziwezesha halmashauri hizo kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa kutumia fedha hizi na kuzirejesha ili halmashauri nyingine zinufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Kamati inakutana na Wizara shilingi bilioni 33.18 sawa na 66.4% zilikuwa zimerejeshwa. Taarifa zinaonesha kuwa zipo halmashauri ambazo zimekusanya fedha hizi na kuzitumia kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha hizi ni za mzunguko *(revolving fund)*, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha halmashauri zote ambazo hazijarejesha, zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri nyingine kutumia fedha hizo kwenye programu hii. Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo maalumu wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati na kwenda moja kwa moja Wizarani na za halmashauri ziende halmashauri. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ili kurahisisha shughuli za kuendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubakishaji wa 20% ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi *(retention)*. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 ilifanya mabadiliko katika Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 289 kuruhusu halmashauri kubakisha 20% ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi kwa lengo la kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi hiyo. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113 jukumu la ukusanyaji wa Kodi ya Pango la Ardhi ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa pango la ardhi ni miongoni mwa masharti ya msingi ya umiliki wa ardhi nchini na kutolipa kutolipwa kwa pango la ardhi ni moja ya sababu inayoweza kupelekea ubatilishwaji wa hati miliki, jambo linalopaswa kuratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya Ardhi. Licha ya mabadiliko hayo ya Sheria ya Mwaka 2024 kuelekeza 20% ya

makusanyo ya kodi kubaki halmashauri, Serikali haijawahi kupeleka fedha hizo pamoja na mambo mengine sababu mojawapo ikiwa jukumu hilo kutokutekelezwa na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ndiyo inayomiliki na kusimamia kumbukumbu zote za wamiliki wa hati za ardhi nchini. Ili kutekeleza jukumu la ukusanyaji wa pango la ardhi, Wizara inalazimika kutumia fedha zake za ndani kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* kwa shughuli za ukusanyaji wa pango la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kukosa hizo fedha inapunguza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na ujenzi wa mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za ardhi *(e-ardhi)*. Ili kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi nchini, Serikali italazimika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchi nzima, kuongeza na kutunza taarifa za walipa kodi, kuwatambua wamiliki wa ardhi na kupunguza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa haya yote unahitaji bajeti ya kutosha. Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya Ardhi kubaki au kurejeshewa 20% ya makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi ili fedha hizo zitumike kukamilisha shughuli tajwa kwa lengo la kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa maeneo ya wazi *(open space)*. Utengaji na usimamizi wa maeneo ya wazi nchini unaongozwa na Sheria ya Mipangomiji Sura 355. Sheria hii inazipa mamlaka za upangaji, jukumu la kutenga, kupima, kutunza na kulinda maeneo ya wazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi. Maeneo yote ya wazi kama vile viwanja vya michezo, bustani na maeneo ya kupumzikia ni mali ya umma na hayapaswi kubadilishiwa matumizi bila idhini maalumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa maeneo mengi ya wazi ni vigumu kuyatambua kutokana na uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kushirikiana na watumishi wa Wizara ambao huuziana kinyemela na kubadili matumizi. Vilevile, baadhi ya mitaa haitatengewa kabisa maeneo hayo. Vilevile, baadhi ya

mitaa haijatengewa kabisa maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa na kuhakikisha kuwa inasimamia kikamilifu utengaji na utunzaji wa maeneo ya wazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation)*. Shirika la Nyumba la Taifa ni taasisi ya Serikali inayosimamia na kuendeleza sekta ya ujenzi, miliki na makazi nchini. Miradi mikubwa ya shirika hii inajumuisha miradi ya makazi, majengo ya kibiashara, huduma za upangishaji na uwekezaji wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2025/2030 imeielekeza Shirika la Nyumba kujikita katika kuongeza upatikanaji wa nyumba bora na za gharama nafuu hususan mijini na maeneo yenye ukuaji wa kasi wa idadi ya watu. Kuendeleza miradi ya nyumba na majengo ya biashara katika mikoa inayokua kwa kasi, kukuza ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi *(PPP)* na kuboresha mipango miji na matumizi ya ardhi ili kusaidia maendeleo ya makazi yaliyo rasmi na yenye huduma za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati inaishauri Shirika la Nyumba la Taifa kukamilisha miradi yake yote ambayo imechukua muda mrefu kukamilika kufanya ukarabati wa nyumba zake zote za zamani zilizochakaa ili kuongeza mapato, kukuza, kupendezesha mji, na kuongeza ustawi wa jamii. Aidha, kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za gharama nafuu unaotokana na ukuaji wa miji kuliko uwezo wa uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika la Nyumba, kuliwezesha shirika kujenga nyumba za gharama nafuu kuwasaidia wananchi wa makundi ya kipato cha chini na ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi ilianzishwa mwaka 1984 chini ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura ya 116 ya Sheria za Tanzania. Tume hii iliundwa kwa lengo la kuratibu na kusimamia upangaji

bora wa matumizi ya ardhi nchini ili kuhakikisha ardhi inatumika kwa tija uendelevu na kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, tume inakabiliwa na changamoto za upungufu wa rasilimali fedha unaopelekea utekelezaji wa mipango kuchelewa, kuibuka kwa migongano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji, hifadhi na makazi katika vijiji 12,333 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijiji 2,333 nchini ni vijiji 4,873 ndiyo vilivyoandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ili Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ni muhimu Serikali kuimarisha upatikanaji wa rasimali fedha, kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano wa taasisi itolewe elimu kwa wananchi na uwepo wa matumizi ya teknolojia bora na za kisasa katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadi ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati katika maeneo mahususi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Moja, ukusanyaji wa maduhuli: Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa zote za umiliki wa ardhi zinaingizwa kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji;

(ii) Ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi nyingine mfano Mamlaka za Maji na kadhalika; na

(iii) Mfumo wa kidijitali wa uuzaji wa viwanja unakuwa rasmi na rafiki ili wananchi waweze kunufaika na fursa zinazotokana na mfumo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, ni migogoro ya ardhi nchini. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali iongeze kasi katika kuandaa na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi ili vijiji vyote vifikiwe na mipango hii iongeze kasi ya kupima, kupanga, kumilikisha na kusajili hati miliki za ardhi kwa kila kipande cha ardhi ili kuondoa migogoro, lakini pia kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi;

(ii) Iongeze huduma ya Kliniki za Ardhi katika mikoa yote nchini; na mwisho

(iii) Iwachukulie hatua kali na stahiki watumishi wote wanaojihusisha na vitendo vilivyo kinyume na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupanga, kupima na kumilikisha Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali kuhakikisha halmashauri zote ambazo hazijarejesha fedha za mradi wa *KKK* zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri nyingine kutumia fedha hizo kwenye programu hiyo na iweke mfumo maalumu wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati; na

(ii) Kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ikiwemo barabara ili kuhamasisha wamiliki kuendeleza maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo unganishi wa kielektroniki wa huduma za ardhi *(e-ardhi)*. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza mfumo wa *e-ardhi* kwenye halmashauri zote nchini ili shughuli zote zinazohusiana na ardhi zifanyike kwenye mifumo; na

(ii) Ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi na mafunzo endelevu kwa Maafisa Ardhi kuhusu mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza mfumo wa *e-ardhi* kwenye halmashauri zote nchini, ili shughuli zote zinazohusiana na ardhi, zifanyike kwenye mifumo na ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi na mafunzo endelevu kwa Maafisa Ardhi kuhusu mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubakizaji wa 20% ya Makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi. Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya Ardhi kubaki na 20% ya makusanyo ya kodi ya pango, ili fedha hizo zitumike kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na ukusanyaji kodi ya pango la ardhi, sambamba na kusaidia ujenzi na usambazaji wa mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba ya Taifa. Kamati inashauri kuwa, Serikali ijenge nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini ambazo wananchi wa kipato cha chini na kati wataweza kuzimudu. Ianzishe mifumo rafiki ya TEHAMA katika usimamizi wa nyumba, upangishaji na uuzaji. Ifanye uhakiki wa wapangaji halali walioko kwenye nyumba za shirika, ikamilishe miradi yake iliyochukua muda mrefu bila kukamilika na ichukue hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uvamizi wa Maeneo ya Wazi. Kamati inaishauri Serikali kuwa, ifuatilie na kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa, pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria waliohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kamati inaishauri Serikali kuwa, itoe elimu kwa wananchi kuhusu manufaa yanayopatikana kutokana na kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, sambamba na usimamizi wa mipango hiyo. Iongeze elimu kwa umma kuhusu faida za mipango ya matumizi ya ardhi, iendelee kutoa fedha, ili kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ikamilike kwa

vijiji vyote nchini na ikamilishe hatua zote sita za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ili kufikia hatua ya mwisho ya utoaji wa hati miliki za kimila na kupunguza migogoro, kuongeza thamani ya ardhi na kuwafanya wananchi wanufaike na fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ninaomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri. Vilevile ninaomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge kwa umahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa namna walivyojitoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyoonekana katika taarifa hii na kwa ruhusa yako, ninaomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Mbunge na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri; Dkt. Anthony Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy D. Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwa mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa Kamati muda wote walipohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu yaliyopangwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu – 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu – 03, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii unatokana na masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya mwaka 2025 inayozungumzia Muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi inayotoa Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;
(ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na
(iii) Sehemu ya tatu inayofafanua Maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali pamoja na kuhitimisha Taarifa ya Uchambuzi wa Bajeti.

1.3 Msingi wa Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Ardhi unatokana na Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka, 2025. Kanuni ya 121 (4) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Taarifa hii inatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

1.4 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo: -

(i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Bajeti ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
(ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kufikia mwezi Februari, 2026;
(iii) Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48**) na Bajeti ya Tume ya Taifa

ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 *Ufafanuzi wa Jumla*

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Taarifa inaelezea msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na Hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kanuni ya 120 (1) na (2) inazitaka Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

2.2 *Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mara baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03). Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na: -

(i) Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(ii) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli; na

(iv) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

2.2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 29 Mei, 2025, wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo saba (7). Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri

Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Machi, 2026, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alifika mbele ya Kamati kuwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ushauri wa Kamati.

Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, mambo manne yamezingatiwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa Maoni matatu yafuatayo:-

(i) Katika Programu ya KKK, Kamati ilishauri Serikali kuongeza kasi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha kufikia **viwanja 100,000** ifikapo Juni, 2026. Taarifa ya Utekelezaji ilionesha kuwa, upimaji umefikia viwanja 24,326 sawa na asilimia 24 ya lengo. Kamati haikuridhishwa na kasi hii kwani haioneshi uwezekano wa kufikia lengo la viwanja 100,000 ifikapo Juni, 2026. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa lengo linafikiwa ili kuongeza mapato;
(ii) Serikali kushindwa kuonesha hatua za kisheria zilizochukuliwa kwa wawekezaji 31 waliobainika kutozingatia masharti ya umiliki wa ardhi; na
(iii) Serikali kushindwa kuirejeshea Wizara ya Ardhi **asilimia 20** ya makusanyo yanayotokana na kodi ya pango la ardhi (*land rent*).

2.2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa miwili (2) ya Kilimanjaro na Tanga ili kukagua Miradi minne (4) inayotekelezwa na Wizara kama ifuatavyo:-

2.2.2.1 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(a) Mradi Na. 2324: Uimarishaji Mipaka ya Kimataifa - kipande cha IV na V Tarakea - Rombo hadi Mkomazi - Mwanga

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mradi huu ulitengewa **Shilingi 1,000,000,000.** Hadi Kamati inakagua Mradi huu ulikuwa umepokea **Shilingi 900,000,000** sawa na asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa kufikia Machi, 2026 mpaka ulikuwa umeimarishwa kwa umbali wa Kilomita 564 kati ya Kilomita 758, sawa na asilimia 75. Kamati iliridhishwa na hatua ya utekelezaji na kuishauri Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya uimarishaji wa mipaka. Aidha, Kamati inahimiza ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi hili ili kuepuka migogoro itokanayo na wananchi kutoelewa dhana ya uimarishaji wa mipaka.

(b) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni Programu ya miaka 10 unaotekelezwa na Wizara ya Ardhi, kwa kushirikiana na Halmashauri mbalimbali Nchini unaotarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Programu hii ilitoa **Shilingi 180,000,000** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ambazo zimetumika kuchora michoro 5 ya mipango miji na ramani za upimaji 16 zenye viwanja 3,104.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huu umefanyika katika eneo lenye ukubwa wa ekari 1,892. Kamati ilifahamishwa kuwa, halmashauri imeanza awamu ya kwanza ya kuuza viwanja 1,248 kupitia mfumo wa TAUSI, viwanja 1,215 vimeshapandishwa katika mfumo kwa ajili ya kuuzwa na viwanja 33 vitamilikishwa kwa halmashauri kwa ajili ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, Hadi Kamati inautembelea Mradi huu, **Shilingi 1,040,288,619** zilikuwa zimekusanywa kutokana na uuzaji wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwepo kwa deni la **Shilingi 240,000,000** ambazo ni fedha za mkopo zilizotakiwa kurejeshwa baada ya Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi katika Mji wa Mombo kukamilika. Kamati inaitaka Halmashauri kurejesha fedha hizo ambazo ni *revolving fund* ili halmashauri nyingine zinufaike. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa, shughuli zote zilizobaki katika kukamilisha mradi huu, zinafanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, uwekwe utaratibu utakaowawezesha wananchi wenyeji wa eneo hili kupewa kipaumbele wakati wa upimaji na umilikishaji ili wapate ardhi katika mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kupitia mradi huu kamati inaliona lengo zuri la serikali kuondoa/kupunguza migogoro ya ardhi, kuboresha miji na kuongeza mapato. Hata hivyo, ni vizuri Serikali ihakikishe zoezi hili linawanufaisha walengwa katika maeneo yote ambayo Miradi hii inatekelezwa. Kwa maeneo ambayo wananchi hawana uelewa wa mfumo unaotumika kununua na kuuza viwanja, wawekewe utaratibu maalum wa kusaidiwa ili kutoibua migogoro mingine.

(c) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Makazi na Biashara la Mkwakwani Commercial Complex chini ya NHC

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mkwakwani Plaza wa Ghorofa 7 unatekelezwa kwenye Kiwanja Na. 55 A & B, Mtaa wa Mkwakwani katika Jiji la Tanga. Jengo hili limekusudiwa kutumika kwa ajili ya shughuli za biashara, ofisi na nyumba za makazi.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu utagharimu **Shilingi 8,656,365,525.18** na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi 24 kuanzia tarehe 18 Juni, 2025 hadi 17 Juni, 2027. Hadi Kamati inautembelea, tarehe 18 Machi, 2026, Mradi ulikuwa umetumia **Shilingi 1,806,630,734.16** na ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 36.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na malengo pamoja na hatua za utekelezaji wa Mradi huu na kuitaka Serikali kuhakikisha

unakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha. Aidha, Kamati inashauri Shirika la Nyumba kutekeleza yafuatayo: -

(i) kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukarabati majengo yake yaliyochakaa; na
(ii) kuweka mipango ya kujenga nyumba za gharama nafuu ili kuboresha maisha ya wananchi wa kipato cha chini.

2.2.2.2 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)

Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Halmashauri ya Mji wa Muheza

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulitengewa **Shilingi 124,768,000** na ulihusisha vijiji nane (8) vya Mindu, Lunguza, Mkuzi, Mgome, Mpapayu, Ubembe, Misongeni na Enzi ambapo kila kijiji kilitengewa **Shilingi 15,596,000.** Lengo la Mradi huu ni kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliutembelea Mradi huu tarehe 17 Machi, 2026 na imeridhishwa na kasi ya utekelezaji. Pamoja na hayo, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Wananchi waendelee kupatiwa elimu juu ya thamani ya ardhi baada ya upimaji na umuhimu wa kuitunza na kuiendeleza;
(ii) Serikali iongeze kasi ya kupeleka Miradi hii kwenye vijiji vingine hapa nchini ili kutatua migogoro; na
(iii) Serikali iongeze kasi ya kutoa hati za kimila kwenye maeneo yaliyopimwa ili kukamilisha umiliki.

2.2.2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, Katika ziara za ukaguzi wa Miradi inayotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilipokea Taarifa za Utekelezaji wa Miradi na kuona hali halisi ya utekelezaji wa Miradi husika. Lengo likiwa ni kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya Miradi inayohusika. Tathmini ya kina imebainisha yafuatayo: -

(i) Baadhi ya halmashauri kutorejesha fedha za mkopo za Mradi wa KKK kwa wakati na wengine kuzitumia kwa matumizi tofauti na hivyo kuzinyima halmashauri zingine fursa ya kupata mkopo huo;
(ii) Wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini hawana elimu juu ya matumizi ya mfumo wa e.*Ardhi* pamoja na TAUSI na hivyo kukosa fursa zinazopatikana kwenye mifumo hiyo;
(iii) Kukosekana kwa miundombinu muhimu kama barabara, maji na umeme kwenye baadhi ya Maeneo ya Mradi wa KKK kunapunguza hamasa na kasi ya wananchi walionunua maeneo kuyaendeleza; na
(iv) Baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa na hivyo kuleta ugumu kwa baadhi ya maeneo.

2.2.3 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo makisio ya makusanyo yaliyoidhinishwa na Bunge yamefikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Fungu 48 lilikadiriwa kukusanya **Shilingi 290,000,000,000** na Fungu 03 lilikadiriwa kukusanya **Shilingi 1,018,000,000.** Hadi kufikia mwezi Mei, 2026 Wizara ya Ardhi (Fungu 48) ilikuwa imekusanya **Shilingi 191,900,000,000** sawa na **asilimia 66.17.** Aidha, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ilikuwa imekusanya **Shilingi 243,354,000** sawa na **asilimia 24** ya lengo. Taswira ya ukusanyaji inaonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Kielezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Mei, 2026

Fungu	Makadirio	Makusanyo	Asilimia
Wizara (48)	290,000,000,000	191,900,000,000	66.17
Tume (03)	1,018,000,000	243,354,000	24

Chanzo: *Randama za Wizara 2026 na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

(i) Ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Wizara - Fungu 48 umefikia **asilimia 66.17** ya lengo. Kwa kuangalia muda uliotumika na makusanyo, Kamati haioni ni kwa namna gani Wizara inaweza kufikia lengo la makusanyo; na

(ii) Tume - Fungu 03 hadi Kamati inafanya uchambuzi, makusanyo yalikuwa **asilimia 24**. Kamati inaona ni vigumu kufikia lengo kwa mwenendo huu wa makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inaimarisha mikakati yake ya kukusanya maduhuli na pia kuziba mianya ya upotevu wa makusanyo.

2.2.4 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - **Fungu 48** iliidhinishiwa **Shilingi 217,574,892,670,** ambapo **Shilingi 91,380,038,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 126,194,854,670** ni fedha za miradi ya maendeleo. Aidha, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi **(Fungu 03)** iliidhinishiwa **Shilingi 12,708,185,000,** ambapo **Shilingi 8,187,569,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,520,616,000** ni fedha za maendeleo. Kamati ilipokea na kuchambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama ifuatavyo:-

(a) **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, **Fungu 48** - Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 124,999,874,345.18.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 34,687,284,658.48** sawa na asilimia 64.45 ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 24,675,564,016.64** sawa na asilimia 65.69 matumizi mengineyo na **Shilingi 65,637,025,670** sawa na asilimia 94 fedha za ndani za maendeleo. Aidha, fedha za nje za maendeleo hazikupatikana. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha ni kama unavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.

Kielezo Na. 2: Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu 48

MATUMIZI	KIASI KILICHOIDHINISHWA	KIASI KILICHOPOKELEWA	ASILIMIA
MISHAHARA	53,820,915,000	34,687,284,658.48	64.46
(OC)	37,559,123,000	24,675,564,016.64	65.68
JUMLA	**91,380,038,000**	**59,362,848,675.12**	**64.96**
MAENDELEO NDANI	69,869,494,670	65,637,025,670	94.00
MAENDELEO NJE	56,325,360,000	0	0
JUMLA	**126,194,854,670**	65,637,025,670	**52**
JUMLA KUU	**217,574,892,670**	**124,999,874,345**	**57.44**

Chanzo: *Randama ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umeonesha yafuatayo:-

(i) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo unaridhisha isipokuwa upatikanaji wa fedha za nje za Miradi hauridhishi; na

(ii) Kukosekana kwa fedha za nje kunaweza kusababisha Miradi kuathirika na kuongezeka kwa muda wa utekelezaji unaoweza kuambatana na nyongeza ya gharama.

(b) **Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2026, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - **Fungu 03,** ilikuwa imepokea **Shilingi 9,023,839,791.68** sawa na asilimia asilimia 71. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,826,395,000** sawa na asilimia 60 ni fedha za mishahara, **Shilingi 1,676,828,791** sawa na asilimia 48.24 fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 4,520,616,000** sawa na asilimia 100 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kielelezo Na. 3 kinaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha.

Kielezo Na. 3: Upatikanaji wa Fedha (Fungu 03)

UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 03 MWAKA 2025/2026			
MATUMIZI	**KILICHOIDHINISHWA**	**KILICHOPOKELEWA**	**%**
MISHAHARA	4,712,143,000	2,826,395,000	60
(OC)	3,475,426,000	1,676,828,791.68	48.24
JUMLA	**8,185,569,000**	**4,503,223,791**	**53.4**
MAENDELEO (NDANI)	4,520,616,000	4,520,616,000	100
JUMLA	**4,520,616,000**	**4,520,616,000**	**100**
JUMLA KUU	**12,708,185,000**	**9,023,839,791.68**	**71**

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

(i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa asilimia 71 kwa ujumla unaridhisha;
(ii) Upatikanaji wa asilimia 48.24 ya fedha za matumizi mengineyo hauridhishi na unaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za Tume; na
(iii) Upatikanaji wa asilimia 100 ya fedha za maendeleo unaonesha kuwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya upatikanaji wa bajeti ya Tume kuonesha mwelekeo mzuri, bado kiwango kinachotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hakiridhishi katika kufikia lengo la kupanga matumizi ya ardhi kwa kila kipande cha ardhi nchini. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi yote Tanzania ili kuepuka migogoro ya ardhi.

2.3 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;
(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na
(iv) Mambo mahususi yanayogusa Sekta ya Ardhi.

2.3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(a) Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka Fedha 2026/2027 Wizara inakadiriwa kukusanya **Shilingi 300,000,000,000.** Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026**.** Taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027 inaonekana katika Kielelezo Na. 4.

Kielezo Na. 4: Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027 Fungu 48

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027 (FUNGU 48)				
CHANZO	**2025/2026**	**2026/2027**	**Nyongeza/ Pungufu%**	**Nyongeza/ Pungufu%**
	290,000,000,000	300,000,000,000	10,000,000,000	3

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi unaonesha kuwa: -

(i) Makadirio ya makusanyo yameongezeka kwa asilimia 3 ukilinganisha na mwaka unaoisha**;** na
(ii) Kwa kuzingatia hali ya makusanyo ya asilimia 66.17 na muda wa miezi 11 uliotumika, Kamati ina mashaka ikiwa nyongeza ya asilimia 3 ya makadirio inaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka na kusimamia mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli yake ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(b) Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Tume inakadiriwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 518,000,000** ambapo maduhuli yatokanayo na kodi ya pango yamelingana na makadirio ya mwaka unaoisha na maduhuli yatokanayo na michango ya wadau yamepungua kwa asilimia 50. Kielelezo Na. 5 kinafafanua.

Kielezo Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027				
CHANZO	**2025/2026**	**2026/2027**	**Nyongeza/ Pungufu**	**Nyongeza/ Pungufu%**
Kodi ya Pango	18,000,000	18,000,000	-	-
Michango ya Wadau	1,000,000,000	500,000,000	(500,000,000)	50

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo: -

(i) Makadirio ya makusanyo kwa upande wa kodi ya pango yamelingana na makadirio ya mwaka unaoisha. Makusanyo ya maduhuli kwa mwaka unaoisha yalikuwa asilimia 35. Kamati haioni ni kwa namna gani makusanyo hayo yatafikia lengo ikiwa vyanzo na mikakati ya makusanyo ni ile ile; na

(ii) Makadirio ya makusanyo kwa upande wa Michango ya Wadau yamepungua kwa asilimia 50. Hali hii inaakisi hali halisi ya makusanyo yaliyofikiwa ya asilimia 24 kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaishauri Serikali kuongeza vyanzo vya mapato ambavyo ni vya uhakika ili kuhakikisha mapato hayashuki na lengo linafikiwa.

2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - **Fungu 48** inaomba kutengewa **Shilingi 162,149,255,000** kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 153,437,867,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Kwa kuzingatia takwa la Kanuni ya 120(2), Kamati imechambua Makadirio ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa

kulinganisha makadirio hayo na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taswira hiyo inaonekana katika Kielelezo Na. 6.

Kielelezo Na. 6: Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 48 kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na 2026/2027

Na.	Maelezo		Kiasi cha fedha 2025/2026	Kiasi cha fedha 2026/2027	Ongezeko/ pungufu	%
1.	**Matumizi ya Kawaida**	Mishahara	53,820,915,000	56,711,082,000	2,890,167,000	5.4
		Matumizi Mengineyo	37,559,123,000	33,803,211,000	(3,755,912,000)	10
	Jumla ndogo		**91,380,038,000**	**90,514,293,000**	**(865,745,000)**	**1**
2.	**Matumizi ya Maendeleo**	Fedha za ndani	5,732,469,000	5,732,469,000	0	0
		Fedha za nje	56,325,360,000	65,902,493,000	9,577,133,000	17
Jumla ndogo			**62,057,829,000**	**71,634,962,000**	**9,577,133,000**	**15**
Jumla Kuu			**153,437,867,000**	**162,149,255,000**	**8,711,388,000**	**5.7**

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

(i) Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 5.4; na
(ii) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la bajeti ya maendeleo kwa asilimia 15 linaweza kuleta tija ikiwa fedha hizo zitapatikana kwa uwiano sahihi na kwa wakati.

(b) Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 48,110,260,000** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kulinganisha na Makadirio ya Matumizi ya **Shilingi 16,451,351,000** Mwaka wa Fedha 2025/2026. (Kielelezo Namba 7).

Kielezo Na. 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Fungu 03 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027

Na.	Maelezo		Kiasi cha fedha 2025/2026	Kiasi cha fedha 2026/2027	Ongezeko/ pungufu	%
1.	**Matumizi ya**	Mishahara	4,712,143,000	4,423,468,000	(288,675,000)	10
		Matumizi		3,127,883,000	(347,543,000)	10.6

	Kawaida	Mengineyo	3,475,426,000			
	Jumla ndogo		**8,187,569,000**	**7,551,351,000**	**636,218,000**	**8**
2.	**Matumizi ya Maendeleo**		4,520,616,000	38,400,000,000	33,879,384,000	749.44
Jumla ndogo			**4,520,616,000**	**38,400,000,000**	**33,879,384,000**	**749.44**
Jumla Kuu			**12,708,185,000**	**45,951,351,000**	**33,243,166,000**	262

Chanzo: *Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa asilimia 749.44. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Maendeleo ambayo itakuwa na tija endapo itatoka kwa wakati na kuwezesha kupanga vijiji 1,492 kwa mwaka. Hii ina maana kwamba, kiwango hiki cha bajeti kikiendelea kutolewa, kazi ya upangaji wa vijiji 7,460 vilivyobakia nchini, itakamilika ndani ya miaka mitano.

2.3.3 Mambo Mahsusi Yanayogusa Sekta ya Ardhi

(i) **Ukusanyaji wa Maduhuli**

Mheshimiwa Spika, ardhi ni rasilimali muhimu ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Serikali**.** Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara hii kwa ujumla hauridhishi. Jambo hili linapunguza uchangiaji mapato ya ardhi katika pato la Taifa. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha vyanzo na ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa za ardhi za kila mmiliki zinaingia kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji. Vilevile, Serikali ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi zingine mfano Mamlaka za Maji. Mfumo wa e.*Ardhi* pamoja na mifumo mingine irahisishwe ili wananchi wa kawaida wanufaike nayo.

(ii) **Migogoro ya Ardhi nchini**

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kutatua migogoro ya ardhi maeneo mbalimbali nchini, bado changamoto hii ni kubwa. Kamati imebaini kwamba, sababu za migogoro hii ni pamoja kuongezeka kwa ushindani wa matumizi ya Ardhi kunakosababishwa na ongezeko la watu sambamba na ongezeko la shughuli za kibinadamu, ukosefu na au

kutokuzingatiwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, kutokuwa na mfumo wa kidigitali wa usimamizi wa ardhi katika maeneo yote nchini hali inayorahisisha ardhi kumilikishwa mara mbilimbili (*Double Allocation*), kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sheria na baadhi ya watumishi wa ardhi kutokuwa waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Hali hii isipopatiwa ufumbuzi, migogoro itaendelea kuongezeka na kuathiri ustawi wa maisha ya kila siku ya wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi, uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, usimamiaji sheria, ujenzi na usambazaji wa mfumo wa kidijitali wa kusimamia ardhi Nchini ili kuondoa migogoro pamoja na kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi.

(iii) **Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)**

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa mkopo wa **Shilingi Bilioni 50** kwa Halmashauri 57, Vyuo vya Ardhi vya Tabora, Morogoro, Chuo Kikuu cha Ardhi na Ofisi ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha. Lengo likiwa ni kuziwezesha halmashauri hizo Kupanga na Kupima na Kumilikisha ardhi kwa kutumia fedha hizi (*revolving fund*) na kuzirejesha ili halmashauri zingine zinufaike. Hadi Kamati inakutana na Wizara, **Shilingi Bilioni 33.18** sawa na asilimia 66.4 zilikuwa zimerejeshwa. Taarifa zinaonesha kuwa, zipo Halmashauri ambazo zimekusanya fedha hizi na kuzitumia kwa matumizi mengine. Kwa kuwa fedha hizi ni za mzunguko *(Revolving Fund)*, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Halmashauri zote ambazo hazijarejesha, zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri zingine kutumia fedha hizo kwenye programu hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka mfumo maalumu wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati na kwenda moja kwa moja Wizarani na za Halmashauri ziende Halmashauri. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa, maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ili kurahisisha shughuli za kuendeleza maeneo hayo.

(iv) **Ubakishaji wa Asilimia 20 ya Makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi *(Retention)***

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 ilifanya mabadiliko katika Sheria ya Serikali za Mitaa Sura 289 kuruhusu Halmashauri kubakisha asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa lengo la kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi hiyo. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ardhi Sura 113, jukumu la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, ulipaji wa pango la ardhi ni miongoni mwa masharti ya msingi ya umiliki wa ardhi nchini na kutokulipwa kwa pango la ardhi ni moja ya sababu inayoweza kupelekea ubatilishwaji wa hati miliki, jambo linalopaswa kuratibiwa na kusimamiwa na Wizara ya ardhi. Licha ya mabadiliko hayo ya sheria ya mwaka 2024 kuelekeza asilimia 20 ya makusanyo ya Kodi kubaki Halmashauri, serikali haijawahi kupeleka fedha hizo pamoja na mambo mengine sababu mojawapo ikiwa jukumu hilo kutokutekelezwa na halmashauri. Aidha, Wizara ndio inayomiliki na kusimamia kumbukumbu zote za wamiliki wa hati za Ardhi nchini. Ili kutekeleza jukumu la ukusanyaji pango la ardhi, wizara inalazimika kutumia fedha zake za ndani kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa shughuli za ukusanyaji wa pango la ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kukosa fedha hizo inapunguza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na ujenzi wa mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa huduma za ardhi (*e-Ardhi*). Ili kuimarisha mifumo ya taarifa za ardhi nchini, Serikali italazimika Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi nchi nzima; kuongeza na kutunza taarifa za walipa kodi; kuwatambua wamiliki wa ardhi; na kupunguza migogoro ya ardhi. Utekelezaji wa haya yote unahitaji bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya Ardhi kubaki au kurejeshewa asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi ili fedha hizo zitumike kukamilisha shughuli tajwa kwa lengo la

kuongeza kasi ya ukusanyaji wa kodi pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wizara.

(v) **Uvamizi wa Maeneo ya Wazi (*Open Spaces*)**

Mheshimiwa Spika, utengaji na usimamizi wa maeneo ya wazi nchini unaongozwa na Sheria ya Mipango Miji, Sura 355 (*Urban Planning Act, Cap 355*). Sheria hii inazipa Mamlaka za upangaji jukumu la kutenga, kupima, kutunza na kulinda maeneo ya wazi chini ya Usimamizi wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote ya wazi kama vile viwanja vya michezo, bustani na maeneo ya kupumzikia ni mali ya umma na hayapaswi kubadilishiwa matumizi bila idhini maalum ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa maeneo mengi ya wazi ni vigumu kuyatambua kutokana na uvamizi unaofanywa na wananchi kwa kushirikiana na watumishi wa Wizara ambao huuziana kinyemela na kubadili matumizi. Vilevile baadhi ya mitaa haijatengewa kabisa maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa na kuhakikisha kuwa inasimamia kikamilifu utengaji na utunzaji wa maeneo ya wazi nchini.

(vi) **Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation - NHC)***

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ni Taasisi ya Serikali inayosimamia na kuendeleza Sekta ya Ujenzi, Miliki na Makazi nchini. Miradi mikubwa ya Shirika hili inajumuisha miradi ya makazi, majengo ya kibiashara, huduma za upangishaji na uwekezaji wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 -2030 imelielekeza Shirika la Nyumba kujikita katika kuongeza upatikanaji wa nyumba bora na za gharama nafuu hususan mijini na maeneo yenye ukuaji wa kasi wa idadi ya watu; kuendeleza miradi ya nyumba na majengo ya biashara katika mikoa inayokua kwa kasi; kukuza ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (PPP); na kuboresha mipango miji na matumizi ya ardhi ili kusaidia maendeleo ya makazi yaliyo rasmi na yenye huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati inalishauri Shirika la NHC kukamilisha miradi yake yote ambayo imechukua muda mrefu kukamilika, kufanya ukarabati wa nyumba zake za zamani zilizochakaa ili kuongeza mapato, kukuza, kupendezesha miji, kuongeza ustawi wa jamii. Aidha, kuna uhitaji mkubwa wa nyumba za gharama nafuu unaotokana na ukuaji wa miji kuliko uwezo wa uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Shirika kujenga nyumba za gharama nafuu kuwasaidia wananchi wa makundi ya kipato cha chini na kati.

(vii) **Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Adhi**

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (*National Land Use Plan Commission – NLUPC*) ilianzishwa mwaka 1984 chini ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116 ya Sheria za Tanzania. Tume hii iliundwa kwa lengo la kuratibu na kusimamia upangaji bora wa matumizi ya ardhi nchini ili kuhakikisha ardhi inatumika kwa tija, uendelevu na kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Tume inakabiliwa na changamoto za upungufu wa rasilimali fedha unaopelekea utekelezaji wa mipango kuchelewa, kuibuka kwa migongano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji, hifadhi na makazi. Katika vijiji 12,333 nchini ni vijiji 4,873 ndio vilivyoandaliwa mipango ya matumizi bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ni muhimu Serikali kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha; kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano wa taasisi; itolewe elimu kwa wananchi; na uwepo wa matumizi ya teknolojia bora na za kisasa katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

3.1 Maoni ya Jumla

(i) Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu kwa jamii hasa vijana kuhusu taratibu za kumiliki ardhi kihalali na umuhimu wake;
(ii) Wizara ya Ardhi iendelee kufanya maboresho ya kimfumo ili kuondoa kero na changamoto zilizopo; na
(iii) Wizara iongeze kasi ya kupima na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote nchini ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

3.2 Ushauri wa Kamati katika Maeneo Mahsusi kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

a. **Ukusanyaji wa Maduhuli**

Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha taarifa zote za umiliki wa ardhi zinaingizwa kwenye mfumo rasmi wa malipo ili kurahisisha ufuatiliaji;
(ii) Ihakikishe wamiliki wote wa ardhi waliosajiliwa wanaingizwa kwenye mfumo wa kupata jumbe fupi za kukumbushia kulipa kodi kama ilivyo kwenye taasisi zingine mfano Mamlaka za Maji; na
(iii) Mfumo wa kidijitali wa uuzaji wa viwanja unakuwa rahisi na rafiki ili wananchi waweze kunufaika na fursa zinazotokana na mfumo huo.

b. **Migogoro ya Ardhi Nchini**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) iongeze kasi katika kuandaa na kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi ili vijiji vyote vifikiwe na mipango hii.
(ii) iongeze kasi ya kupima, kupanga, kumilikisha na kusajili haki miliki za ardhi kwa kila kipande cha ardhi ili kuondoa migogoro lakini pia kuongeza pato la Taifa litokanalo na rasilimali ardhi;
(iii) iongeze huduma ya kliniki za ardhi katika mikoa yote nchini; na
(iv) iwachukulie hatua kali na stahiki watumishi wote wanaojihusisha na vitendo vilivyo kinyume na Sheria.

c. **Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)**

Kamati inaishauri kuwa, Serikali:-

(i) kuhakikisha Halmashauri zote ambazo hazijarejesha fedha za Mradi wa KKK zinarejesha ili kuziwezesha halmashauri nyingine kutumia fedha hizo kwenye programu hiyo;
(ii) iweke mfumo maalum wa kufuatilia na kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa kwa wakati; na
(iii) Kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayopimwa yanawekewa miundombinu muhimu ikiwemo barabara ili kuhamasisha wamiliki kuendeleza maeneo hayo.

d. **Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa Huduma za Ardhi (*e-Ardhi*)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) ihakikishe inaongeza kasi ya kusambaza Mfumo wa *e-Ardhi* kwenye halmashauri zote nchini ili shughuli zote zinazohusiana na ardhi zifanyike kwenye mifumo; na
(ii) ihakikishe inatoa elimu kwa wananchi na mafunzo endelevu kwa Maafisa Ardhi kuhusu Mfumo wa utoaji huduma katika usimamizi wa Ardhi.

e. **Ubakishaji wa Asilimia 20 ya Makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi (*Retention*)**

Kamati inaishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Fedha na kuruhusu Wizara ya ardhi kubaki na asilimia 20 ya makusanyo ya kodi ya pango ili fedha hizo zitumike kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na ukusanyaji kodi ya pango la ardhi sambamba na kusaidia ujenzi na usambazaji mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa Ardhi nchini.

f. **Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation - NHC)***

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) ijenge nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini ambazo wananchi wa kipato cha chini na kati wataweza kuzimudu;

(ii) ianzishe mifumo rafiki ya TEHAMA katika usimamizi wa nyumba, upangishaji na uuzaji;
(iii) ifanye uhakiki wa wapangaji halali walioko kwenye nyumba za Shirika;
(iv) ikamilishe Miradi yake iliyochukua muda mrefu bila kukamlika; na
(v) ichukue hatua za kisheria kwa wadaiwa sugu.

g. **Uvamizi wa Maeneo ya Wazi (Open Spaces)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(i) Ifuatilie na kurejesha maeneo yote ya wazi yaliyovamiwa pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika; na
(ii) Ihakikishe kuwa inasimamia kikamilifu utengaji na utunzaji wa maeneo ya wazi nchini.

h. **Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Adhi**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) itoe elimu kwa wananchi kuhusu manufaa yanayopatikana kutokana na kazi ya uandaaji wa mipango ya matumzi bora ya ardhi sambamba na usimamizi wa mipango hiyo;
(ii) iongeze elimu kwa umma kuhusu faida za mipango ya matumizi ya ardhi;
(iii) iendelee kutoa fedha ili kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ikamilike kwa vijiji vyote nchini;
(iv) ikamilishe hatua zote sita za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kufikia hatua ya mwisho ya utoaji wa hati miliki za kimila na kupunguza migogoro, kuongeza thamani ya ardhi na kuwafanya wananchi wanufaike na fursa mbalimbali zikiwemo zinazopatikana kwenye taasisi za fedha.

3.3 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuliongoza Bunge letu kwa umahiri. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Naibu Spika -

Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb) na Wenyeviti wa Bunge, kwa kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa namna walivyojitoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha Maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyoonekana hapa chini na kwa ruhusa yako, naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Francis Masanja, Mb -M/Mwenyekiti
3. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Haidary Hemed Sumry, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Cosmas Mtesigwa Bulala, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Fadhili Fabian Ngajilo, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Silvery Luboja Salvatory, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Yannick Ikaya Ndoinyo, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Chiku Athman Issa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Rashid Mohamed Mtima, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Selina Henry Kingalame, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mvita Mustafa Ali, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Hadija Shabani Taya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Joshua Samwel Nassari, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Asia Abdulkarim Halamga, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amina Good Said, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Mb - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Kaspar Kaspar Mmuya, Mb - Naibu Waziri, Dkt. Anthony Sanga - Katibu Mkuu na Bi. Lucy D. Kabyemera – Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuwa

mstari wa mbele kutoa ushirikiano kwa Kamati muda wote walipohitajika.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Masanja, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ahsante sana kwa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati yetu. Hongera sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninatangazo la wageni tena, walioko Bungeni muda huu. Kwa upande wa wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Leonard Akwilapo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kama ifuatavyo:-

Tunaye Ndugu Zidikher Mundeme, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Thamini. Ahsante sana karibu. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Netho Ndilito, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ndugu Emmanuel Chacha, Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi, Wizara ya Ardhi. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Akwilapo, ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni, Makamishna Ardhi Wasaidizi wa Mikoa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia ipo Menejimenti na Watumishi wa Wizara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wasajili Wasaidizi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Mikoa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo Wadau wa Chama cha Wamiliki Ardhi na Nyumba Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Viongozi kutoka Bodi na Taasisi ya Wapima Ardhi Tanzania. Karibuni. *(Makofi)*

Vilevile wapo Viongozi wa Kamati ya Wataalam wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Ardhi na Viongozi wa Bodi ya Mipango Miji na Chama cha Wataalam wa Mipango Miji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi na walimu wa Chuo cha *Paradigims* cha Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wadau mbalimbali wa sekta ya ardhi nchini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kadhalika, wapo marafiki wa Mheshimiwa Waziri na rafiki wa Mheshimiwa Waziri. Pia, tunao wapiga kura wa Mheshimiwa Waziri kutoka Wilaya ya Masasi. Karibuni sana wapiga kura wetu kutoka huko Masasi. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Tunao wageni wa Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni wafanyabiashara na mdau wa maendeleo kutoka Jimbo la Ruangwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 46 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge. Hawa ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Lenchi. Karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi. *(Makofi)*

Wageni 24 wa Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, ambao ni waajiriwa wenzake wa Ofisi ya CCM ya Makao Makuu JK67. Karibu sana. Leo tumejua kwamba, Mheshimiwa Sanga alikuwa mwajiriwa wa Chama cha Mapinduzi Makao Makuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Baada ya kupokea maoni ya Kamati yetu, tunaanza sasa mjadala.

Tunaanza na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, ajindae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango kwenye bajeti hii ya Wizara ya Ardhi. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametujalia na ametuwezesha kuendelea kuwepo kwenye nyumba hii muhimu kwa ajili ya kufanya kazi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninatumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa imani kubwa waliyoipata kutoka kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kukabidhiwa jukumu hili la kusimamia sekta hii muhimu sana kwa maisha ya Watanzania wa nchi hii. Pia, ninawapongeza kwa kazi nzuri, ambayo wanaifanya pale Wizarani yeye Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Kamishna wa Ardhi na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili leo Bajeti ya Wizara ya Ardhi, ikiwa hii ni bajeti ya kwanza katika utekelezaji wa Dira yetu ya Maendeleo ya Mwaka 2050. Kwa mujibu wa dira tuliyojiwekea, ambayo tumeanza utekelezaji wake, dira yetu ya kuelekea 2050 ina nguzo muhimu. Nguzo ya tatu katika dira yetu ni uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye Dira, maeneo ya kipaumbele katika nguzo hii ya tatu muhimu, ni usimamizi madhubuti wa sekta ya ardhi. Nimeanza na hili, ili Mheshimiwa Waziri ajue kwamba, anayo kazi kubwa ya maelekezo ya Dira, lakini tunayo maelekezo mazuri sana ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, kwa ajili ya mwaka 2025 mpaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo ambalo limekuwa ni changamoto kwenye ardhi ni migogoro, tumekuwa na changamoto ya migogoro na imekuwa kubwa. Mkononi kwangu

hapa, ninazo ripoti mbili za kazi nzuri sana iliyofanywa na Watanzania wenzetu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine; Ripoti ya kwanza inaitwa *Land Conflicts and Disputes in Tanzania; Causes Impacts and Resolution,* imetoka Mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo Ripoti ya pili, wenzetu wa *SUA* walifanya utafiti kuhusu migogoro ya ardhi kwenye baadhi ya halmashauri na wilaya hapa nchini, inaitwa *Challenges of Land Conflicts in Kilombero, Kilosa and Mvomero District.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye taarifa hizi ambazo wataalamu wetu kutoka chuo chenye heshima kubwa kwenye nchi hii wamefanya, moja ya sababu kubwa ya migogoro ya ardhi ni kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Wanasema zaidi ya 70% ya migogoro tuliyonayo inapatikana kwenye maeneo ambayo ni *unsurveyed*. Sasa katika mazingira kama hayo, maana yake, namna ya kwanza ya kuhangaika na changamoto ya migogoro ya ardhi ni kutengeneza na kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina vijiji 12,333. Tangu tumepata uhuru mpaka sasa tumefanikiwa kutengeneza na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 4,873; namba hii ni ndogo sana. Pamoja na udogo wa namba hii, kwa dhati kabisa ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyofanya kwenye eneo hili. Pamoja na kwamba, namba hii ni ndogo, lakini zaidi ya 55% ya vijiji vilivyoandaliwa mpango wa matumizi bora ya ardhi ni kazi iliyofanyika ndani ya kipindi cha miaka minne cha Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee tumeona kwenye bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma leo, kwa mara ya kwanza katika historia ya sekta ya ardhi katika Tume ya Mipango ya Ardhi tunakwenda kupata bajeti ya maendeleo ya tume, shilingi bilioni 48, haijawahi kutokea. Mwaka wa fedha uliopita tulikuwa na Bajeti ya Tume ya shilingi bilioni 19 na huko kote tulikotoka bajeti ilikuwa ni ndogo, ndiyo maana kazi ya uandaaji wa mipango ya

matumizi ya ardhi ilikuwa ndogo, lakini Mheshimiwa Rais ameridhia, safari hii ametuletea bajeti ya shilingi bilioni 48.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti hii ya shilingi bilioni 48 wenzetu wa tume wanatuambia watakwenda kufanya kazi ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 1,410. Kwa lugha rahisi ni kwamba, katika vijiji zaidi ya 7,000 vilivyobaki, kama Serikali ikitenga na kutoa fedha, kama ilivyoanza kwenye bajeti hii, itatuchukua angalau miaka mitano kumaliza kazi ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji vyote vya nchi hii. Jambo hili ni kubwa, tunaipongeza Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwenye eneo hili ni maeneo mawili. Jambo la kwanza, tunafahamu suala la kutenga fedha ni jambo moja, lakini kutolewa fedha ni jambo lingine. Haifurahishi, kila Waziri Mkuu anakokwenda, ni migogoro ya ardhi. Kila kiongozi akienda kwenye ziara, ni migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, ili kutatua changamoto za migogoro ya ardhi, ili tutatue jambo hili, tuiombe Serikali, fedha hii ambayo tumeamua kuitenga kwenye bajeti hii, Serikali ikaitoe kama ilivyotengwa ili wenzetu wa tume wakaifanye kazi hii ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji vyetu, tuweze kuondoa changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ninataka nishauri kwenye eneo hili, tunapokwenda kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kazi ya uandaaji ina hatua sita, kuanzia hatua ya kwanza mpaka hatua ya mwisho, ambayo ni hatua ya sita, inayojumuisha utolewaji wa hatimilki za kimila kwa wananchi wetu ndani ya Nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba wenzetu wa Tume, Serikali imetenga fedha. Itakapotoa fedha hizi, kwa ajili ya kufanya kazi ya kutengeneza mipango ya matumizi bora ya ardhi, tukafanye kazi hii kwenye hatua zote, ili tufike mpaka hatua ya mwisho, ya sita, ya kutoa hatimilki za kimila kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza itatusaidia kuendelea kuimarisha utatuzi wa migogoro, itatusaidia kuendelea kuongeza

thamani ya ardhi zetu, pia, itasaidia wananchi kwenda kutumia fursa mbalimbali, zikiwemo fursa zilizopo kwenye taasisi za kifedha kuweza kunufaika na fursa hizo kupitia hatimiliki hizi za kimila ambazo zitakwenda kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninaomba nilichangie na niishauri Serikali, kwamba tumesema hapa kuhusu migogoro. Utengenezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ni njia moja, lakini njia ya pili, hasa kwa maeneo ya mijini, dunia imebadilika, Watanzania wa leo hawafurahii kuendelea kuona kuna kesi za *double allocation* kwenye viwanja. Watanzania wa leo hawafurahi kuona wakati mwingine taarifa zao, kumbukumbu zao, zinapotea, hazipatikani kwa wakati. Ili haya yasitokee, ni nini tukakifanye?

Mheshimiwa Naibu Spika, twende tukaimarishe mfumo wa usimamizi wa ardhi yetu ndani ya nchi. Tukatengeneze mfumo wa kidijitali wa kusimamia ardhi kwenye nchi yetu na siyo tu kutengeneza, tukausambaze nchi nzima. Mpaka sasa ni halmashauri chache sana ambazo tumefanikiwa kusambaza mfumo wa kidijitali wa kusoma ardhi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mambo ya *double allocation* yasiwepo, ili kumbukumbu na taarifa za ardhi zipatikane vizuri, ninamshauri Mheshimiwa Waziri, waende wakasambaze mfumo huu nchi nzima, ili mtu yeyote akiingia kwenye mfumo awe anajua *plot* namba fulani kwenye *block* fulani inamilikiwa na nani. Hii itapunguza utapeli, itapunguza migogoro. Tunawaomba katika fedha ambazo Bunge litawaidhinishia kiwekwe kipaumbele na mkazo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kusambaza mfumo kwenye nchi nzima siyo ndogo. Ninajua inawezekana kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha, kwa sababu ya umuhimu wa ardhi. Ninaomba niishauri Serikali, mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi, kwa maana ya *land rent,* warudishiwe watu wa Wizara ya Ardhi waweze kufanya kazi ya kutengeneza mifumo, lakini pia, iwasaidie kuendelea kukusanya kodi ili tuendelee kutoa mchango kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi za wenzetu mapato ya kodi ya ardhi yanategemewa na yana mchango mkubwa sana kwenye bajeti ya nchi. Naiomba Serikali, tulikuja hapa Mwaka 2024 tukafanya marekebisho ya Sheria ya Fedha kwenye *Finance Bill,* lakini tulifanya kosa moja la kiufundi. Tulielekeza 20% ya mapato yatokanayo na *land rent* yarudi kwenye Halmashauri kwa ajili ya kazi ya ukusanyaji wa *land rent,* lakini kiuhalisia kazi ya ukusanyaji wa kodi ya ardhi, kwa maana ya *land rent,* siyo ya halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, ni kazi inayofanywa na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, unapozungumza masharti ya umiliki wa ardhi makubwa ni mawili. Moja ni kulipa kodi, na pili ni maendelezo. Watu wa ardhi ndio wenye kumbukumbu za wamiliki, ndio wenye *data* zote muhimu. Fedha hii irudi kwenye Wizara ya Ardhi ili waweze kuitumia kuendelea kukusanya kodi, na pia, waitumie kusambaza mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, mwaka huu watu wa ardhi katika malengo ya shilingi bilioni 290 wamekusanya shilingi bilioni 191. Hili lisingewezekana, lakini baada ya Wizara ya Fedha kujua tatizo lilipo na kuamua kuongeza fedha maalum, kwa ajili ya kazi hii, tunaiomba Serikali iipeleke kwa wenzetu wa Wizara ya Ardhi, ili wakaendelee kufanya kazi ya kusambaza mfumo huu na kuitumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni eneo la ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Ninatumia nafasi hii kuipongeza Serikali na pia, kulipongeza sana Shirika letu la Nyumba la Taifa, linafanya kazi kubwa na nzuri, lakini tunayo changamoto. Waendelezaji wengi wa ardhi, waendelezaji wengi wa milki, kazi wanayoifanya na kusema kwamba, wanajenga nyumba za gharama nafuu kwa uhalisia, kwa Watanzania wa kawaida, siyo za gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani Serikali iiangalie nchi hii, iwaangalie vijana wa Kitanzania waliotoka shuleni, wamepata kazi, wanakwenda kuanza kazi na kuanza maisha kwa mara ya

kwanza. Nyumba ya shilingi milioni 150, milioni 200, hawawezi kuimudu. Tunajua, ili nyumba iwe ya gharama nafuu, yako mambo mengi humo ndani yake. Yako mambo ya kikodi na mengine ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ikaliangalie jambo hili na tunawaomba Wizara ya Ardhi itoe mwongozo kwenye jambo hili. Wizara ndio imekabidhiwa sera. Itoe uongozi kwenye jambo hili, ije na mpango utakaowezesha kusaidia taasisi zetu ziweze kujenga nyumba za gharama nafuu ili Watanzania wengi wanufaike nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la wawekezaji wakubwa katika sekta ya ardhi. Nchi yetu inao wawekezaji wengi kwenye sekta ya ardhi na wamemilikishwa mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za uwekezaji. Tunajua wawekezaji hawa ni muhimu sana na mimi wala sipingi, lakini lazima tukubaliane wapo wawekezaji ambao masharti ya umiliki wa ardhi waliyopewa hawaitendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, kule Korogwe tunaishukuru Serikali, ilifuta hati ya Shamba la Mwakinyumbi na wananchi wetu wanaelekea kupata makazi. Ninaiomba Serikali, iwasimamie wamiliki wote wa mashamba makubwa, yaani wawekezaji, ili watumie mashamba haya sawasawa na masharti yao waliyokabidhiwa, ili yaweze kutoa faida. Wale ambao wanashindwa, hatua zichukuliwe, ili nchi yetu ipate maendeleo, tuendelee kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana. Ninaunga mkono bajeti hii. Ninaomba Watanzania na Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono, ili wenzetu waendelee kuifanya kazi hii. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Nilimtaja Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji. Mheshimiwa Jafari Chege, ajiandae.

MHE. MASANJA K. KADOGOSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwanza nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa hii fursa niweze kuchangia kwenye Wizara yetu hii muhimu sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kama mwenzangu alivyofanya, kwa kazi kubwa anayoifanya, vilevile kwa utashi, kuhakikisha kwamba Wizara yetu inatekeleza majukumu yake. Pili, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana inayotoa matumaini na mpango mzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwapongeze watendaji wa Wizara yetu hii, kuanzia Katibu Mkuu, *Engineer* Sanga; Naibu Katibu Mkuu, vilevile na wakuu wa taasisi za *National Housing;* kuna Mkurugenzi imara sana kule, Ndugu Hamad, anafanya kazi nzuri sana; pia tuna Mthamini wetu Mkuu wa Serikali, Dada yangu Evelyn. Tumefanya naye kazi, *almost* kwa miaka 10 ni Dada imara sana huyu, taasisi nyingine ambazo zinajihusisha na miradi mikubwa, ninaamini wanalifahamu jina lake vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni kitu muhimu sana, huwezi ukatenganisha maendeleo ya taifa na ardhi hasa hasa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu amezungumzia mambo ya dira, nisingetaka kurudia huko, dira yetu ni nguzo mojawapo katika nguzo zile tatu. Kuna misingi ya dira na kuna nguzo, ambapo nguzo zinasimama katika misingi ile. Kwa hiyo ni kitu muhimu sana katika Taifa letu, Mheshimiwa Waziri ni lazima alielewe hilo, kwa sababu wasiposimama imara Dira ya 2050 itakuwa ni ndoto kuitimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaihitaji ardhi, kama nilivyosema kwamba huwezi ukatenganisha maendeleo ya kiuchumi na matumizi bora ya ardhi. Ukiangalia hata katika vitabu vya Mungu,

urithi pekee ambao alipewa Ibrahim ulikuwa ni ardhi. Sasa kama Mungu anazungumzia ardhi kwa sisi binadamu *it has to be true*. Kwamba, msingi wa sisi ili tuendelee kama Taifa ni lazima tuwe na matumizi bora ya ardhi. Pamoja na Baba wa Taifa kuzungumzia ardhi, watu, kama sehemu mojawapo muhimu sana katika maendeleo ili tuweze kuendelea, pamoja na uongozi bora na siasa safi lakini ardhi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, yapo mambo ambayo yamefanyika mazuri sana, na ni lazima tu-*acknowledge*, kwa sababu tusipo-*acknowledge* kwa kitu ambacho kimefanyika, kwa wale wakongwe wanajua, ukirudi miaka 10 – 20 iliyopita ardhi ilikuwa ni matatizo. Kuna mambo mazuri sana ambayo yanafanyika. Mambo ya utoaji wa hati, wamefanya kuwa na mfumo sahihi wa utoaji wa hati miliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge sisi wengine ambao tuko tuna-*experience* hiyo kwamba, unaweza ukataka hati yako ndani ya siku kadhaa umeshapata, na wengine ndani ya juma moja umeshapata. Kwa hiyo ni maendeleo ambayo kwa kweli ni vizuri tukawapa hongera wenzetu wa Wizara ya Ardhi; kwamba kuna kazi inafanyika. Hata hivyo ni kweli kwamba bado tunahitaji nguvu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza mwenzangu, tuna migogoro. Mimi ninatoka katika eneo la wafugaji na wakulima. Ile Kamati ya Mawaziri walipokuja walifika maeneo ya kwetu Bariadi, na waliweza kuzungumza na wananchi. Kuna mambo fulani ambayo wameyafanya na ninajua kwamba watarudi tena. Kwa hiyo tuna-*acknowledge* kwa hilo. Lakini ni kweli kwamba katika Taifa letu tuna migogoro na sehemu kubwa kama alivyosema mwenzangu, asilimia 70 ya migogoro ni kwa sababu hatujakuwa na mpango sahihi, yaani Mpango Bora wa Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tunapokwenda na tunapokuwa tumejiwekea shabaha kubwa katika Taifa letu la kuwa na uchumi wa dola trilioni moja inapofika 2050, sehemu mojawapo ambayo tunahitaji kufanya *transformation* kubwa ni kwenye ardhi. Ninaweza nikatoa mfano mmoja tu, kuna kiwanda hapa kimejengwa cha mbolea, ukiangalia *distance* ya kutoka

kwenye kiwanda ukaenda kwenye reli yetu, *almost* ukitaka kufanya kujenga *side*, gharama unayoitumia kujenga ile ile kuipeleka pale yawezekana ikawa sawa sawa na gharama ya kujenga kile kiwanda. Sasa haya ni mambo tunazungumzia ya kuwa na *master plan* kwenye *cities,* kwenye *region,* haya ni mambo ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapojiwekea kwa mfano, sisi tunajenga reli, tunaendelea kufika Kigoma, tunaenda Mwanza ni lazima tunapokuwa tunapanga mipango yetu ya matumizi bora ya ardhi, viwanda vyote viwe *aligned* na kule ambako kuna reli inapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana gani? Unaposogeza viwanda karibu na reli maana yake unapunguza gharama za uzalishaji kwenye viwanda. Hatutoi maeneo ya viwanda kwa sababu eneo limepatikana, tunaangalia katika tulivyojipangia, *land use*s, pale tumepanga nini, na kuna nini ambacho kitasaidia kile kiwanda. Tunapoanzisha kongani za viwanda ni lazima zifuate reli, na ni lazima zifuate barabara zetu. Hiyo ndiyo maana ya matumizi bora ya ardhi. Unaweza ukatoa mifano mingi tu ya *land use integration*. Kwa hiyo, hili tulilozungumza ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunajenga hizi barabara zetu, tunajenga hii miundombinu baada ya muda tunaingia kwenda kubomoa. Inaumiza, *especially* watu ambao tulikuwa tumebahatika kupata nafasi ya kusimamia kubomoa nyumba ya mtu, lakini ni kwa sababu hatuna matumizi bora ya ardhi, watu kujua kwamba mpaka wako ni hapa na kitu kingine kinaanzia hapa. Kwa hiyo, nilitaka nilizungumze hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya upimaji, tuna vijiji 12,333 kama mwenzangu alivyozungumza, vijiji sasa hivi tulishapima 4,000 *plus,* ninafikiri sielewi kama tatizo ni fedha au tatizo ni utashi, au tatizo ni nini? Ninafikiri Mheshimiwa Waziri atakapokuja anapokuwa ana-*wind up* ile hotuba yake atazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kama ni fedha katika jambo hili ninaamini kwamba hatuhitaji fedha nyingi kama ya

kujenga Nyerere *Hydropower* (Bwawa la Nyerere) au kujenga *SGR*; lakini jambo la ardhi siyo tu ni suala la kupata *ownership*, lina *implication* mpaka kwenye maisha ya watu. Wakulima na wafugaji wanauana, kwa hiyo si suala ambalo tunaweza tukasema kwamba eti hatuna bajeti, ni lazima Serikali ije; ninaamini wana mpango, tuanze kujiwekea utaratibu, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati. Kama tutajiwekea mpango wa miaka mitano jambo hili tulimalize, halipendezi katika Taifa vilevile linaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, *transformation* haiwezi ikatokea nje ya watu na ardhi. Maana yake ni kwamba, kama hatufanyi *transformation* kwenye ardhi tunazuia mambo mengine kuendelea. Kwa hiyo, upande wa ardhi ni muhimu sana tukaliona katika jicho hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kuwa kuna kitu kinaitwa *plot development fund*, na wanayo katika Wizara. Pengine kama hili jambo ni gumu sana *in term of* ya kuweka bajeti, *maybe* tuanzishe huu mfuko. Aidha ni kuanzisha au kuutunisha mfuko huo, ili tuutumie kwa ajili ya ku-*fund*. Tutafute vyanzo kama tulivyofanya kwenye barabara, kama tulivyofanya kwenye reli; lakini ni muhimu sana kuwa na matumizi bora ya ardhi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie suala la nyumba. Kama nilivyosema, ninampongeza sana Ndugu yangu Mkurugenzi wa *National Housing*. Wana *approach* nzuri sana ya *pre-selling*. *Pre-selling* maana yake ni kwamba, kama *project* inahitaji bilioni labda 10, unaweza ukajikuta kwamba unatumia fedha ya watu au wanunuzi, na pengine unahitaji asilimia nusu tu ya fedha hiyo. Kwa hiyo ni *initiative* nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenzangu, tunapojenga hizi nyumba kuna *categories*. Kuna watu wa juu, kuna watu wa katikati na kuna watu wa chini; na *approach* zake za *funding* haziwezi zikafanana. Unapo-*approach,* kwa maana ya *high end, financing* yake haiwezekani ikafanana na ya *low end*. Kwa hiyo hili ni suala la ki-*policy,* kwamba si tu suala la Wizara ya Ardhi, ni suala mtambuka. Wizara yetu ya fedha wana sera gani linapokuja suala la ujenzi wa nyumba nafuu? Hata tusipofanya

hivyo tutakuwa tunawaonea watu wa ardhi. Hili ni suala mtambuka katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa ili nami niweze kuchangia Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu nzima kwa bajeti, ambapo wameleta mapendekezo ya 2026/2027, inaleta tija kwa kweli. Na sababu ni moja tu, leo tunapozungumzia hii ardhi ni jambo ambalo tunaenda nalo kwa wakati. Yaani ni *transformation* kubwa sana kutoka kwenye makaratasi tunaingia kwenye *electronics.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina kilometa za mraba 945 kama sikosei, na tupo wananchi kama milioni 60 na zaidi. ukiangalia Katiba yetu Ibara ya 24 ina-*state clearly* kwamba kila mwananchi ana haki ya kumiliki mali; na mali tunayozungumzia ni ardhi. Mataifa mengi sana ulimwenguni hata watu huwa tunapigania ardhi kwa kuwa ndiyo mali kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa ardhi nchini kwetu umepitia *phases* tatu. *Phase* ya kwanza ilikuwa umiliki wa ardhi kabla ya ukoloni; *that was* 1890; mwaka 1890 *or before that*. Wakati ule utaratibu ulikuwa wa kimila, na ndiyo ilikuwa desturi. Watu wanakaa wanajadili, hii ndiyo mipaka yako, hapa utafanya hichi; huu ndio uliokuwa utaratibu. *Phase* ya pili ilikuwa ni wakati wa ukoloni; *that was 1890 up to 1961, in between.* Wakati wa ukoloni palikuwa na sehemu kuu mbili, wakati wa Ujerumani na wakati wa *British,* ndizo *phases* tulizoanza kuzipitia; na hapo ndipo palipotokea mabadiliko makubwa sana kuja kwenye makaratasi, na kuweka sheria. Kwamba tutakuwa tunafuata hivi, tutakuwa

tunafuata vile. Ardhi hii itakuwa kwa ajili ya Kaisar hii itakuwa kwa ajili ya *Queen.* Ndio mchakato uliokuwepo wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, mwaka 1961 baada ya kupata Uhuru ndipo umiliki wa ardhi ukapitia *phase* ya tatu, na pakawa na mabadiliko, tena pakawa na mabadiliko makubwa ambayo yalileta tija kwa wananchi wetu kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hii historia fupi ambayo nimeitoa inamaanisha kabisa kwamba, kabla ya ukoloni walikuwepo wamiliki halali wa maeneo husika. Umiliki wa sasa hivi, bila kuwa na nyaraka za kutosha basi umiliki wako una mashaka; *unless otherwise* iwe *proper documented.* Hata ukienda kwenye mahakama utahangaika lakini kama hauna nyaraka ambayo iko *documented* vizuri, na iwe *acknowledged* na Wizara ya Ardhi basi hapo utadhulumiwa au hiyo haki yako itapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba niongelee vitu viwili tu. Kuhusiana na hati, na hapa ninataka ni-*highlight* baadhi ya sheria ambazo zinaleta changamoto sana katika jamii yetu na hata Mtwara Vijijini tuna shida hapo. Kuna Sheria ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu Sura 146 ya Mwaka 1994. Pia tuna Sheria ya Ardhi, Sura 114 ya Mwaka 1999. Hizi Sheria mbili ukizifuatilia vizuri utaona zinaleta shida kwa wananchi kutokupata hati, hususan wale waliopo kwenye maeneo ya bahari na maeneo tengefu. Sasa cha kujiuliza mfano kuna Kijiji cha Msimbati, Nalingu na Msanga Mkuu. Sheria imekuja mwaka 2016 kama sikosei, ya maeneo tengefu; wameweka *demarcation* pale lakini waliwakuta watu wanamiliki maeneo yale. Leo hii wanapoomba hati hawapewi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, turudi kwenye historia kabla hata ukoloni walikuwepo wamiliki*, it is their right*. Wanastahili wapewe hizo hati. Kwa hiyo ni changamoto ambayo tunapitia lakini unaweza ukastaajabu kitu kingine anaweza akaja mwekezaji kutoka nje ya nchi akapewa *derivative right of occupancy;* kwamba miliki wewe, lakini mwananchi ambaye yupo babu zake na mababu zake kutokea miaka hiyo walikuwepo pale

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii ni changamoto, karibu...

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Arif kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Katani Katani.

TAARIFA

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda eneo la Mafia wapo wawekezaji wa kutoka nje wamepata tayari hati lakini wazawa hawana hati maeneo kama haya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Arif, taarifa unaipokea?

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza katika Bunge lako Tukufu ninapokea taarifa, mimi naipokea na Mungu wa Mbinguni amjalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo changamoto iliyopo. Kwa hiyo unakuta mwekezaji anaweza akapewa *derivative right of occupancy* na mambo yakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala linguine, wote tutakubaliana hapa kwamba inapofikia hatua ya kulipa fidia kwenye nchi yetu pana changamoto mbili. Moja, kutokulipwa kwa wakati, na lingine ni thamani ambayo anayolipwa mwananchi. Sasa ukienda kuangalia Sheria ya Uthamini, Sura 138 ya mwaka 2016, ukipitia humo kuna maneno utayakuta *full,* maana yake kikamilifu, *fair,* maana yake ya haki, na *prompt,* kwa wakati. Kwamba ukishafanya uthamini mwananchi yule inabidi alipwe *full fair* na *prompt*. Yaani vitu hivi vitatu viende kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye utekelezaji haliko sawa. Watu hawalipwi kwa wakati na wakati mwingine hawalipwi *amount* ambayo iko kamilifu. Mfano wa uhalisia Jimbo la Mtwara Vijijini eneo la Msijute, watu wamefanyiwa tathmini kulipwa hawajalipwa, maana yake ni kwamba Wizara ya Ardhi jukumu lao huwa linakuwa pale tu, wakishafanya tathmini baada ya hapo

mwekezaji yule pale au Wizara husika, hapana! ifikie hatua sheria tumezitengeneza sisi wenyewe lakini utekelezaji basi wausimamie hadi mwisho ili wananchi waweze kunufaika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, eneo lingine ni pale Kitele; Kata ya Kitele Jimbo la Mtwara Vijijini kuna mgogoro mkubwa baina ya mwekezaji na wananchi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kengele ya kwanza hiyo.

NAIBU SPIKA: Malizia Mheshimiwa sentensi ya mwisho.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa dakika moja tu.

NAIBU SPIKA: Ni sekunde 30 Mheshimiwa muda wako umekwisha, malizia sekunde 30 za mwisho.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo hiyo hiyo sekunde 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kitu ambacho nitawashauri Wizara ya Ardhi muangalie ile *section* ya *market comparison approach,* sokoni mnapoenda kufanya tathmini. Mara nyingi sana utakuta mnatuma watumishi wenu wanaenda kuuliza tu kwa Wenyeviti na Watendaji wa Vijiji kwamba hawa watu wameuziana kiasi gani. Unaweza ukakuta *knowledge*, au semina, Mwenyekiti wa Kijiji au Mtendaji wa Kijiji hana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya muda ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Jafari Wambura Chege atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele ajiandae.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo kwenye Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea mbele, kwa mujibu wa Kanuni ni vyema nika-*declare interest* kwamba nimekuwa mtumishi kwenye Wizara hii kabla sijawa ndani ya Bunge lakini pia, ni mdau kwenye sekta ya ardhi. Kwa hiyo, nitakayokuwa ninayasema basi yasifungamane kwa namna yoyote na maslahi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameendelea kuifanya. Kwa miaka yote ya Bunge lililopita dani ya Bunge hili ilikuwa ikifika Wizara ya Ardhi, moja ya jambo kubwa ambalo tumekuwa tukilizungumza ilikuwa ni kufanya maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo tulikuwa tunasema tayari tumekwenda mbele zaidi hasa ukilinganisha na sera ya miaka zaidi ya 20 nyuma iliyopita. Kwenye sekta ya ardhi zipo shughuli nyingi za kiuchumi zinafanyika. Yapo maeneo mengi yanashindwa ku-*move* kwa sababu ya maboresho ya kisheria, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia alivyolisikia hili chini ya Wizara hii akaona ni vyema atuletee Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na maboresho yake yakafanyika mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwapongeze sana Wizara kwa namna nilivyoona mnakwenda sasa kufanya maboresho ya sheria ili yaendane na kasi na umuhimu wa mabadiliko ya Sera ya Taifa ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi, Katibu Mkuu pamoja na Makamishna wote. Pia, Kamishna Mkuu pamoja na Makamishna ngazi ya Mikoa kwa namna mnavyoendelea kutafsiri na kusimamia sera hii na sheria mbalimbali za ardhi. Ninaamini mnakwenda hivyo kwa mwitikio mkubwa pamoja na kwamba changamoto bado ziko nyingi kwa sababu shughuli za ardhi

zinafanyika kila siku, lazima mkutane na changamoto mbalimbali. Kazi na wajibu wenu ni kuhakikisha changamoto hizo mnazipunguza kwa namna mnavyoweza ili tuweze kufikia malengo ya Dira ya Taifa pia malengo ya Mheshimiwa Dkt. Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi nitajikita katika maeneo mawili. Wizara hii ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nitachangia kidogo kwenye ardhi lakini nitajikita pia kwenye makazi kwa maana ya nyumba ili niweze kuchangia kwa ukubwa wake wa Wizara yenyewe namna jina lilivyokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wizara kwa namna mlivyoamua kupanga matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji. Niungane na wenzangu wamesema zaidi ya 55% kwenye utendaji wa Mheshimiwa Dkt. Samia ndani ya miaka minne tumekwenda kupanga matumizi bora ya ardhi zaidi ya vijiji 2,700 na kidogo ukilinganisha toka uhuru tulikuwa na vijiji 2,100 na kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona kwa miaka minne Mheshimiwa Dkt. Samia ametoa fedha kupanga vijiji vingi ukilinganisha na tangu tumepata uhuru wa nchi hii. Mnafanya kazi kubwa sana. Pia, Waziri lazima tukubaliane pamoja na kazi kubwa iliyofanyika tunayo kazi kubwa kama Wizara ya kufanya. Migogoro mingi nchini chanzo cha migogoro hii ni kukosekana kwa matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia migogoro ya mfugaji na mkulima ni kwa sababu hakuna matumizi kwenye eneo lile. Matumizi bora ya ardhi hayapo; mmoja anamwingilia mwingine akiamini ana haki kuliko mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ukiangalia maeneo kadhaa ambayo yanavamiwa kwa sababu ya kukosa uhalisia wa matumizi ya maeneo hayo ni kwa sababu hatuna matumizi bora yanayoainishwa kwenye maeneo hayo. Niwaombe sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla wake, kwa kuwa tumedhamiria kutoa fedha kwenda kupanga matumizi bora ya ardhi tuwasaidie hawa watu wa ardhi hasa upande wa tume ili

waende wakafanye maboresho. Wakapima maeneo mengi tuweze kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kutekeleza Dira ya Taifa ya 2050, hatuwezi kufika huko bado sisi kama nchi tunaendelea kuzungumza migogoro peke yake. Ni lazima tufike mahali tubadilike, sasa tuanze kuzungumzia namna ya wananchi wanavyonufaika na ardhi yenyewe kuanzia makazi, shughuli za kiuchumi wanazofanya ili migogoro sasa iwe ni sehemu mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufika huko hatuwezi kufika kama Serikali haijaamua kutoa fedha kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima ili angalau tuondokane na hiyo migogoro. Sasa tuanze kuzungumzia namna bora ya maboresho ya makazi kwa wananchi ambao wanafanya shughuli za kiuchumi kwenye ardhi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ilione hili na ione namna bora ya kuendelea kutoa fedha. Niwapongeze nimeona mmetoa fedha, mmetenga fedha kwenye bajeti inayokuja kwa upande wa tume ili kuhakikisha mnakwenda kupanga maeneo mengine. Ni jambo zuri lakini kama walivyosema wenzangu kupanga ni jambo moja na kutoa ni jambo jingine. Tuwaombe sana muendelee kutoa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuridhia kuanza kutumia Mfumo wa *e*-Ardhi nchini. Mfumo wa e-Ardhi pamoja na *complication* zake, dunia nzima huwa una *complication* nyingi sana. Mifumo mingi ya usimamizi wa ardhi lazima inakuwa na changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, changamoto ambazo ziko ndani ya uwezo wetu hasa kwenye kufanya maboresho ya mfumo huu Mheshimiwa Waziri usisite nenda kafanye maboresho ya mfumo huu kwa sababu, ukiangalia shughuli zote sasa za umiliki wa ardhi, utoaji wa hati, uthamini wenyewe, kupanga na kupima, vyote vinatambuliwa

kwenye mfumo, yaani hakuna shughuli hizi zinavyoweza kufanyika mpaka mwananchi kumiliki hati bila kupitia kwenye mfumo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na *contradiction,* kulikuwa kuna namna ambayo mfumo hau-*perform* vizuri, maana yake shughuli zote hizi zina *compromise*. Zikishasimama shughuli zote hizi tunamnyima haki mwananchi wa mwisho ambaye anatakiwa kupewa hati yake ili aweze kumiliki ardhi. Nikuombe kwenye eneo ambalo unatakiwa ulifanyie kazi kwa nguvu kubwa ni eneo hili la mfumo na kubwa ambalo unatakiwa kufanya ni kuboresha na kusimamia kuhakikisha kwamba unakuwa na *man power* ambayo inaweza kuutumia mfumo kwa usahihi na itoe majibu na itumie kwa ufasaha ili angalau tuweze kuona faida yake kwa wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kama nilivyosema, nitakwenda kujikita kwenye eneo la makazi. Pamoja na Dira ya Taifa ya 2050 pia tunayo hii Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo tumeizungumza, lakini pamoja na miongozo mbalimbali ambayo imekuwepo kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, mapungufu ya nyumba kwa sasa tuna upungufu wa nyumba nchi hii zaidi ya milioni tatu. Huo ni upungufu peke yake, lakini mahitaji kwa kila mwaka tunahitaji nyumba 200,000 mpaka 300,000 *plus* ili kuweza kukidhi yale mahitaji ya kila siku kutokana na ongezeko la watu kwa namna wanavyohitaji nyumba nchini, sasa lazima Serikali ilione hili

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukimbizana na Dira ya Taifa nilitamani tuanze mchakato huo sasa, mchakato huo unaanza kwa kufanya maboresho ya sheria mbalimbali, kwa sababu tayari tumefanya maboresho ya sera, twende tukatafute namna ya kupata miongozo na sheria mbalimbali ili angalau tuweze kuona namna gani tunakwenda kutengeneza makazi bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ninajua umeshiriki hapa juzi kwenye *World Forum,* ambayo inahusiana na uboreshaji wa makazi holela, pia kutafuta namna ya kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi, pamoja na kukimbizana na hayo lazima tutafute sheria

ambayo inaweza ikasimamia. Kwanza, sheria itakayotafsiri maana ya *affordable housing* ni nini, na sheria ambayo itaweza kutengeneza miongozo ya *affordable housing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Shirika la Nyumba, niwapongeze sana Shirika la Nyumba kwa kazi wanayofanya, wakijenga nyumba wakii-*term* shilingi milioni 70 au milioni 60 wao wanaita *affordable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi sana mtu ku-*reason* kwamba kwa nini shilingi milioni 60 iwe *affordable?* Anaweza aka-*reason* na majibu yoyote yanaweza yakapatikana kwa sababu hatuna sheria. Hatuna *affordable housing act* inayosimamia na kutafsiri maana ya *affordable housing* ni nini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya hapa mwaka 2024 wao walitengeneza *affordable house* ndiyo maana wamekuja na *program ya affordable* wanajenga nyumba kwa kasi kwa sababu wametafsiri maana ya *affordable* ni nini. Wananchi wameelewa, *private sector* zimechangamkia ile sheria, zinajenga kwa kupewa mikopo mbalimbali na sasa unaona kwamba wanakwenda kupunguza upungufu wa nyumba nchini. Ningetamani sana Waziri moja ya jambo kubwa zuri, wamechangia hapa wenzangu, lazima tuwe na *affordable housing act* ambayo inatafsiri haya yote ili twende kwa mwongozo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri lazima tuwe na *affordable housing fund*. Wenzetu wa Kenya wanatoa mikopo mbalimbali wanasaidia *private sector* namna ya kupata fedha kuwekeza kwenye *industry* ya nyumba. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tutafute namna ya kupata mifuko hii ili tuweze kusaidia *private sector* pale zinapokwama ili tuweze kupunguza kasi na ndiyo tafsiri ya Dira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaki tufike 2050 bado tunazungumza tuna changamoto ya nyumba, ninaamini itafika wakati huo migogoro ya ardhi imekwisha lakini lazima tuwe tuna sheria ambazo zinatunufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni *issue* ya *RERA,* nichukue nafasi hii, Mheshimiwa Waziri sijaiona ukiizungumza. Niwapongeze Wizara mlizungumza mwaka jana na mlisema vizuri sana, *Real Estate Regulatory Authority* tumekuwa tukiizungumza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sheria au ni mamlaka ya udhibiti ambayo inakwenda kudhibiti madalali wanaofanya shughuli za ardhi nchini. Leo hii madalali wanafanya shughuli yoyote wanayoweza kufanya. Kwanza, hawatambuliki hakuna sheria inayowatambua na kuwakusanya, *developers* wanaofanya shughuli za *real estate* hakuna sheria inayowatambua na kuwakusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukitaka kupata tathmini ya nyumba zinazojengwa na tathmini ya nyumba zinazouzwa ili Serikali iweze kupata *capital gains tax* hakuna sheria na hakuna mamlaka inayodhibiti idadi ya nyumba ili muweze kukusanya mnachokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri, sikuliona ukilisema hapa na ninaamini kwenye majumuisho utakuja kulizungumza vizuri. Watu wamekuwa wakiona kama haina umuhimu. Umuhimu wa *RERA* kwanza Serikali mtaimarisha mapato yenu, tunavyozungumza kwa maana ya kwamba mtakuwa mnajua nani kauza kiwanja na kauza wapi. Nani kamtapeli nani na nani kapata, haya yote mtakuwa na *regulatory authority* ambayo inaya-*control.* Mtapunguza migogoro ya watu kudhulumiana lakini na ninyi mtaweza kupata kipato chenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine itakuwa ni kuzitambua *real estate agents* na *developers* hawa tunawaita *private sectors.* Hatutaki na hatutamani Shirika la Nyumba pekee ndilo liwe suluhisho la kutatua nyumba kwa maana ya makazi nchini. Tunataka *private sector* ziingie huko na ili ziingie huko Mheshimiwa Waziri lazima kuwe kuna sheria ya kuwatambua na kuhakikisha kwamba wanafika mahali ambapo ni pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho *Real Estate Regulatory Authority* ndiyo itakwenda kusimamia mikataba yenu kati ya

mpangaji na mwenye nyumba kwa maana ya kwamba leo wanatakiwa walipe *property tax*. Ni nani anayesimamia kujua kwamba mimi nimepangisha saa ngapi ili niweze kulipa kodi ya *property tax* Serikalini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakapokuwa mna *regulatory authority* itaweza kuwa ina idadi ya nyumba, ina idadi ya madalali...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ... ina idadi ya *developers* na *real estate agents* kwa manufaa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niombe sana hili Mheshimiwa Waziri mwishoni utakapolizungumza kwa kuwa mlizungumza kwenye bajeti ya mwaka jana ulisisitize ili tujue mwelekeo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi. Kwanza, kabisa ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai leo hapa tuko tunachangia Bajeti ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mungu ninapenda nimpongeze Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Akwilapo na Naibu wake Mheshimiwa Kaspar. Pia, nimpongeze Kamishna wa Ardhi, Mheshimiwa Mathew, nimpongeze Katibu Mkuu wa Ardhi, Mheshimiwa Sanga na niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Ardhi kwenye idara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, jinsi ambavyo ameliwekea uzito suala la ardhi. Kwa kipindi chake tangu ameingia madarakani mwaka 2021 mpaka tunavyoongea sasa hivi ameweza kutoa pesa na kupima vijiji takribani 2,700 na kuifanya nchi yetu ya Tanzania ipate unafuu wa matatizo ya migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, pongezi nyingi kwa watendaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Tume ya Mipango inafanya kazi. Maana yake hapo mwanzo kwenye Kamati tulikuwa tumeijiwa na hoja ya kuifuta hii Tume kwa sababu ilikuwa haipewi pesa. Kwa sasa hivi Tume inapewa pesa, tunaiomba Serikali iendelee kuongeza nguvu na kuipatia Tume ya Mipango pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, nimezoea ulipokuwa Mwenyekiti ninaomba sasa niende kwenye mchango wangu wa Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi kweli inafanya kazi vizuri na tumeona *improvement* katika hiki kipindi cha miaka mitano kwenye Wizara hii ya Ardhi lakini yapo mambo ambayo Wizara ya Ardhi inabidi iangalie jinsi ya kuweza kuyatatua. Jambo la kwanza, ninapenda nizungumzie kampuni ambazo zinapima viwanja. Kampuni hizi zinazopima viwanja kwenye Halmashauri zetu na kwenye miji yetu zimekuwa zikiwanyonya sana wananchi kwenye ardhi zao. Zimekuwa zikitumia mwanya kwa sababu wananchi hawajui zile sheria za ardhi na hawaelewi, zimekuwa zikitumia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingi zinapokwenda kupima ardhi huko kwenye Halmashauri zetu mara nyingi zinagawana sawa vile viwanja na wale wenye ardhi. Kwa mfano, mimi nina ekari zangu 100, ninataka kampuni inipimie utakuta yule mpimaji ataondoka na viwanja takribani 20 au 30. Ninaomba sheria iwekwe kwenye hizi kampuni ambazo zinapima ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wamedhulumiwa ardhi zao kupitia kampuni hizi. Zimekuwa zikileta migogoro ya

ardhi mingi. Lakini, pia Wizara ya Ardhi imenunua vifaa vya kupimia ardhi. Ni kwa nini halmashauri hazipimi ardhi? Kama ni hoja ya kuongeza wafanyakazi wa kupima, ningependekeza Halmashauri zote zichukue jukumu la kupima ardhi. Kama kuna kampuni ambayo inapima basi iwe *supervised* na mfanyakazi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa au nitoe tu mfano ili kuweka *point* yangu vizuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye Mkoa wangu wa Katavi, takribani wananchi 600 walisimama na karatasi wakilalamikia mambo ya ardhi. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba baada ya Bunge la Bajeti, Waziri wa Wizara ya Ardhi aende kule kwenda kutatua hiyo migogoro. Hapa nilitaka kuonesha ni jinsi gani wananchi wana matatizo ya ardhi. Huo ulikuwa ni mkutano wa hadhara Tarehe 16 mwezi wa Nne. Wananchi takribani zaidi ya 600 walikuja mbele na karatasi wakilalamikia masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo niende kuchangia suala ambalo Mbunge wa Mtwara ametoka kulizungumza sasa hivi. Wananchi ule ukosefu wao wa kutokujua sheria za ardhi wamekuwa wakidhulumiwa maeneo yao na wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi hawajui hizi sheria za ardhi. Hajui akatafutie hati wapi (ile *process* nzima ya kupata hati) wananchi wengi hawajui. Matokeo yake wamejikuta wamekaa mahali mwekezaji anakuja anachukua maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *content* ya hapo ya mwekezaji ninataka nizungumze kwa watanzania ambao wanaishi nje ya nchi lakini ni wazaliwa wa Tanzania na wamekwenda kule wakatafute maisha. Wengine wao wakabadilisha uraia lakini sasa kwa sababu *the Land Act* ya Mwaka 1999 ile *section* ya 19 na *section* ya 20. *Section* 19 ni *right of occupancy* (jinsi ya kumiliki kiwanja), lakini 20 inamzuia *non citizen* kumiliki kiwanja. Inamruhusu amiliki kwa *deliberate right*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachokizungumza hapa ni kwa nini wale Watanzania ambao wanaishi nje ya nchi kwa

namna nyingine walijikuta wana uraia wa nje ya nchi ya Tanzania, ni kwa nini wasije wakamiliki zile ardhi za babu zao. Wawekewe masharti wamiliki kama wanavyomiliki hao *investors,* kwa sababu kwenye *deliberate right* yule mmiliki *(investor)* anapewa *99 years* ya kumiliki kiwanja. Hivi miaka 99 ni uhai wa binadamu? Kama binadamu anaishi hata ukiwepo utakuwa hujui kama uko ahera au duniani. Sasa kwa nini na hawa wasipewe hiyo ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nizungumzie mradi wa KKK. Mradi wa KKK ni mradi ambao ulianzishwa mwaka 2021. Wizara ya Ardhi, ilitoa shilingi bilioni 50 kwa Halmashauri 57 ili waweze kupima na kumilikisha viwanja, sasa Halmashauri nyingine zimerudisha zile pesa lakini Halmashauri nyingine hazijarudisha. Sasa ili walipe ninaomba nizitaje hizo Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikuletee Halmashauri ambazo hazijalipa, kuna Bunda, Mbeya Mjini, Mbeya *DC*, Buchosa *DC*, Uyui *DC*, Mtwara *DC*, Babati *DC*, Musoma *MC*, Chalinze *DC*, Mbinga *TC*, Butiama *DC*, Meatu *DC*, Tabora *MC*, Babati *TC*, Musoma *DC*, Tarime *TC*, Morogoro *DC*, Ludewa *DC*, Ikungi *DC*, Kishapu *DC*, Msalala, Rorya, Shinyanga *DC*, Maswa, Lushoto, Lindi Manispaa, Chamwino, Mbulu, Shinyanga, Manyoni, Korogwe *DC* na Korogwe *TC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hizi zinadaiwa pesa tangu mwaka 2021 tunaziomba zirudishe hizo pesa ili Halmashauri zingine ziweze kupewa hizo pesa ili waende kupima viwanja kwa sababu pesa hizo wamekaa nazo muda mrefu, sababu ya muda siwezi kutaja wanadaiwa shilingi ngapi lakini kwa kutaja tu kwamba wanadaiwa basi naomba washughulikie jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza hapa ni suala la mipaka ya kimataifa. Tumeangalia mpaka wa Kenya na Tanzania unaendelea na tulienda kukagua kule wanaendelea kuweka ile mipaka lakini tuna mipaka ya Rwanda, tuna mipaka ya Burundi, Congo, Zambia na nchi nyingine. Pia, tuna mpaka wa Tanzania na Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini tukiwa kama nchi

tunatakiwa tu-*resolve* tatizo la mpaka wa Tanzania na Malawi kwenye ziwa Nyasa. Kwa nini nasema hivi? Tuliwahi kuuliza kwenye Kamati tukaambiwa kwamba mgogoro huo unasuluhishwa kimataifa na mwenyekiti wa mgogoro Mheshimiwa Rais mmoja mstaafu na sijui kama *protocol* inaruhusu kumtaja, naomba ni-*reserve* jina hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huo umekuwa ni wa miaka mingi, ninaiomba nchi yangu ya Tanzania sisi hapa tulipo baada ya miaka 100 tutakuwa hatupo duniani. Ninaomba tusiwaachie vitukuu vyetu, watoto wetu, mgogoro wa Tanzania na Malawi kuhusu Ziwa Nyasa. Ninaomba ushughulikiwe, hatuwezi tukajidanganya tukasema kwamba mgogoro umeisha wakati upo na hatujaushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. Nawatakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu awabariki sana wote. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele atafuatana na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai ambao ametujalia na leo tuko Bungeni tukijadili bajeti ya Wizara yetu ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais wetu, Dr. Samia Suluhu Hassan, kwa utendaji mzuri sana na kwa kukubali kuidhinisha fedha nyingi hizi zaidi ya shilingi bilioni 210 kwa ajili ya Wizara yetu hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Akwilapo na Naibu wake Ndugu yangu Muya kwa kazi nzuri sana mliyoifanya katika kuandaa bajeti hii. Pia, nawashukuru watendaji wote wa Wizara kwa msaada mkubwa ambao mmeutoa kwa viongozi wetu na kufikia bajeti hii ambayo tumeisikia hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu mara moja kabisa kuhusiana na suala la migogoro ya ardhi. Wachangiaji wengi wamechangia na wamekuwa wakichangia kuhusu suala la mgogoro ya ardhi na baadhi wamechangia muda si mrefu na kutoa mapendekezo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubaliana na mapendekezo yote lakini mimi naomba niseme kitu kimoja, Wizara yetu ya Ardhi inaitwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hilo ndiyo jina la Wizara yetu. Nasema hivyo kwa sababu maafisa wetu wa ardhi ambao wako kwenye Halmashauri, hawa ni waajiriwa wa Wizara ya Ardhi na wala siyo waajiriwa wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme kwamba moja ya migogoro ya ardhi ni huu mfumo tulio nao wa maafisa wetu wa ardhi kuwepo katika halmashauri zetu lakini ni waajiriwa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pia, mamlaka ya nidhamu ya watumishi hawa haipo Wizara ya TAMISEMI ipo Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba hiki yaweza kuwa ni kiini kikubwa sana cha migogoro ya ardhi katika nchi nzima, nilikuwa ninaomba nipendekeze mapema kabisa, kwamba ufanye uamuzi na ikiwezekana kama taratibu zinaruhusu maafisa hawa wapelekwe moja kwa moja TAMISEMI waweze kuwajibika TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo ambalo linatisha, ni Mbunge Jimbo la Dodoma Mjini lakini migogoro ya ardhi iliyoko hapa na kwa kuwa sasa ni makao makuu ya nchi migogoro ambayo wakati mwingine inatisha na wakati mwingine inawafanya wamiliki wa ardhi wa asili na walioimiliki kihalali kuonekana kama ni wageni katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anaongea na wakazi wenye migogoro ya ardhi pale Ofisi ya Mkuu wa Mkoa watu walikuwa ni wengi. Inasikitisha, unayo ardhi yako umeimiliki toka awali lakini anakuja mtu anakuambia

mimi nina hati yangu hii nimeipata ardhi hii ni ya kwangu wakati wewe umezaliwa pale pale unamiliki ardhi kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba, nikuombe ndugu yangu Mheshimiwa Akwilapo, angalieni utaratibu huo. Ikiwezekana hawa maafisa muwapeleke muwaajiri TAMISEMI, kwani TAMISEMI hawawezi kuwaajiri na kuwalipa mshahara? Ni lazima wawajibike hii Wizara ya Ardhi? Anafanya makosa afisa lakini anachokifanya Mkurugenzi ni kuandika taarifa tu kwamba huyu amefanya *double allocation* lakini kitafanyika nini ni jambo ambalo kwa kweli linakuwa linaleta shida kwa wamiliki halali wa ardhi. Ninaomba niishie hapa kwa suala hili kwa hiyo moja kwa moja naomba tu Wizara hizi mbili zisomane.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninaomba kuongelea kuhusiana na Sera yetu ya Ardhi ya Mwaka 1995 na mapitio yake ya Mwaka 2023. Ukurasa wa 19 wa hii sera yetu unasema hivi, Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007 ilitungwa kukabiliana na kasi ya kukua kwa miji na kuhakikisha miji inapangwa na kukua ipasavyo. Wote sisi ni mashahidi 95% ya Jiji la Dar es Salaam halijapimwa. Maana yake ni kwamba ni makazi holela! Kwa nini tumefikia hapo? Tumefikia hapo kwa sababu ya changamoto ambazo tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, walioko hapa wanafahamu na ambao ni wakazi wa Dar es Salaam, kabla ya mwaka 1995 huko nyuma maeneo ya Mbezi, Kimara, Bunju, Tegeta, Kibamba, Mbweni, Chamazi, Kongowe, Chanika na Gongo la Mboto yalikuwa ni mashamba, lakini sasa nini kinachoendelea kule? Ni makazi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, panda *SGR* sasa hivi, ukifika tu Pugu ukianza kuondoka pale unaona makazi yalivyokaa, makazi ambayo yanatisha, makazi holela. Ni lazima tuangalie tumejikwaa wapi. Tukubaliane tu na ukweli, mwaka 1999 ndipo Wilaya za Temeke, Ilala na Kinondoni zilipotamkwa kuwa halmashauri. Kabla ya hapo zilikuwa ni Wilaya tu na shughuli yote ilikuwa inafanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Sasa yawezekana kwamba kutokuwepo kwa hizi Halmashauri ilikuwa ni moja ya changamoto lazima tuhakikishe tunaziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dodoma kwa sasa ndiyo jiji ambalo ni Makao Makuu ya nchi na ndiyo Jiji kubwa kuliko Majiji yote Sita. Tuseme matano ambayo yapo. Dodoma ina *square kilometre* 2,607. Linalofuata ni Dar es Salaam, lina *square kilometre* 1,590 likifuatiwa na Mwanza kilomita za mraba 1,325 halafu ikifuatiwa na Tanga *square kilometre* 600, Arusha *square kilometre* 272 na mwisho Mbeya *square kilometre* 252. Kwa hiyo, Dodoma ndiyo Jiji lenye eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa maeneo niliyoyataja hapa ambayo yamekuwa makazi holela kwa sasa hapa Dodoma maeneo yaliyo wazi; Kata za Matumbulu, Kata za Mpunguzi, Kata za Mbabala, Kata za Chigongwe, Kata ya Mbalawala na Kata ya Nala. Hizi Kata ziko pembezoni na bado hazina makazi ya kutosha. Mpaka sasa eneo ambalo limejengwa Dodoma ni *square kilometre* 625, zilizobaki bado hazijajengwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nipendekeze kwamba Wizara, Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Akwilapo kwenye bajeti yako sijasikia chochote kuhusiana na tunafanya nini ili maeneo haya yaweze kupimwa mapema na kuwekewa miundobinu. Mheshimiwa kinachoendelea sasa hivi Halmashauri zinapima maeneo lakini hazichongi barabara na ndicho kilichotokea Dar es Salaam, hazichongi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake wakazi hawawezi kujua, maana yake hawana utaalamu wa ardhi, hawawezi kufahamu kwamba hapa kuna barabara, hapa hakuna barabara. Matokeo yake wanajenga na tukija kushtuka majengo yamekuwa mengi, huwezi kupitisha miundominu ya maji, huwezi kupitisha miundominu ya maji taka, huwezi kupitisha nguzo za umeme kwa sababu ya makazi holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wakati wa hitimisho lake nitaomba aniambie vizuri kwa sababu nimesikia tu anataja Iyumbu peke yake. Iyumbu siyo Dodoma peke yote ndugu yangu, yako maeneo Ipala, Chahwa, Hombolo hayajapimwa lakini sijasikia chochote kwamba maeneo haya yatapimwa kwa utaratibu gani ili tuweze kuepuka makazi holela katika Jiji la

Dodoma miaka 50, 60 ijayo. Tuachie watoto wetu na vitukuu vyetu maeneo ambayo yanaweza kutosha miundobinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam asilimia tisa tu ndiyo imewekwa miundobinu ya majitaka *the rest of Dar es Salaam* haina miundombinu ya majitaka ni kwa sababu ya ujenzi holela. Nakuomba Mheshimiwa Dkt. Akwilapo ufanye jambo. Kwa kweli nisipoona mipango endelevu ya Jiji la Dodoma na maeneo mengine ya nchi kwenye upimaji na uwekaji wa barabara kwa ajili ya miundobinu nitakamata shilingi mpaka nitakapopata maelezo sahihi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, maeneo niliyoyataja Dodoma ambayo yako wazi yana milima pia, nataka nikuthibitishie, tusipochukua hatua za haraka sasa hivi milima ile itajengwa makazi holela kama unavyoona Mwanza kule Bugando ama kama unavyoona Morogoro kwenye milima ya Uluguru, watu wanajijengea wanavyojisikia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nipendekeze, maeneo haya ya milima ambayo siyo milima mikubwa sana yapimwe. Kama vile tunavyoona South Africa pale Johannesburg, tunapoona Pretoria, milima imepimwa. Yamepimwa maeneo wanapewa watu wenye uwezo wanajenga kwa masharti maalum, kupanda miti, kuweka utaratibu mzuri. Tukiachia hivi hivi tukanyamaza watajenga watu wetu na hatutaweza kuwabomolea kwa sababu siyo ubinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja lakini naomba Mheshimiwa Waziri unipe maelezo ya kutosheleza kwamba unafanya nini na Jiji la Dodoma lenye *square* kilomita 2,607. Tusije tukawa na Jiji siku zinazokuja ambalo ni kubwa halafu halina miundominu, halina barabara kama tunavyoona katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Naomba tumalizie na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi na ninamshukuru Mwenyezi Mungu ametupa afya njema na tumeamka salama. Ninampongeza Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali, ni maisha, ni uchumi, tamaduni za watu, uhai na ni siasa. Kwa hivyo inahitaji weledi, umakini, utulivu, *professionalism*, ushirikishwaji na teknolojia ili tusaidie katika kutatua matatizo haya. Hii timu ya ardhi mimi sina tatizo nao ninyi mmekidhi vigezo hivi vingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu tu ni kwamba, ninyi mnatakiwa muendelee kuwa *clean* kuliko mtu mwingine yeyote, wote na watumishi wenu kule chini kwa sababu migogoro ya ardhi inaleta magomvi makubwa sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yako, mkiendelea kusisitiza hilo msiwe sehemu ya migogoro, muendelee kuwa *neutral* mtamaliza migogoro mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza Kamati ya ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, wameandika ripoti nzuri sana na wamejaribu kuainisha matatizo ambayo yanawakabili Watanzania walio wengi, ni ripoti nzuri sana. Kabla sijasahau Mheshimiwa Waziri, Bunge lililopita kliniki ya ardhi mliileta Bungeni hapa, kulikuwa na nukuu nzuri sana ya Mheshimiwa Rais mliweka kwenye bango lenu lile. Nukuu ilikuwa nzuri sana, hiyo mchukue mchapishe kwenye magazeti yenu na kila mahala sasa halafu mtafsiri vizuri sasa kwa sababu Mheshimiwa Rais amesema kwamba ardhi ni uhai yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kama walivyosema wengine, matumizi bora ya ardhi ndiyo jawabu peke yake la migogoro hii ardhi. Kwa hiyo, kwa kweli nashangaa sana, pamoja na kwamba bajeti imeongezeka kwenye tume lakini kwangu mimi *it is not enough*. Unajua ukitaka kuelewa nchi, *focus* ya nchi iko wapi unaangalia tu bajeti. Kwa suala linalohusu ardhi lilitakiwa liwe kipaumbele kwa kitu chochote. Tupunguze mambo mengine ili Watanzania wasiwe na migogoro inayoendana na inayotokana na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma ripoti ya Kamati hapo, mmetengeneza *formula* mkasema bajeti mkipata hii mtaweza vijiji 1,492 na kwa sababu vimebaki 7,460 mkiendelea kupata bajeti mnayopata kwa miaka mitano mtakuwa mmemaliza zaidi ya 7,000 lakini mimi nataka hili suala la ardhi limalizike *within 2years,* wala huhitaji miaka mitano. Kwa nini? Kama ni suala la bajeti, tutoe pesa haraka hii kazi ifanyike. Unajua pia unavyo-*drag* hili jambo na pesa zisipotoka kwa haraka inakuwa *expensive* halafu na migogoro inaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, itoke *lumpsum* tu watu waende *field* tumalizane na habari ya migogoro ya ardhi. Siyo sawa. Acha tuhangaishwe na mambo mengine. Wacha tuhangaishwe na mafuta na vitu vingine hivi vinavyotoka huko kwingine lakini angalau masuala ya ardhi na migogoro isiwepo. Mheshimiwa Waziri ninakushukuru sana, baada ya ziara ya Waziri Mkuu na ninyi mlivyokuja Kiteto imepata vijiji 20 na kuna kazi inaendelea vizuri sana, sana ndiyo maana nafurahia sana kazi yenu na ushauri wangu hili liendelee

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ushauri mwingine Halmashauri hizi lazima zitenge pesa za matumizi bora ya ardhi. Haiwezekani hizi Wilaya zenye migogoro ya ardhi ambayo ni *hotspot*, hata kama bajeti zao ni ndogo lakini angalau vijiji viwili, vitatu, lazima. Kama mkurugenzi wangu ananisikia na madiwani wote wananisikia hapa, tunataka bajeti za halmashauri na zenyewe zinavyopata *boost* ya kutoka wizara vijiji 20 angalau na wao vijiji viwili, vitatu lazima. Hilo wala siyo ombi *otherwise* hauwezi kuendelea kupambana na watu huku wanaendelea kugombana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine migogoro inatokea kwa sababu ya *confusion*. Haki za ardhi, haki za madini, haki za ardhi, haki za uhifadhi wakati fulani. Mheshimiwa Waziri ninasema kila wakati Wizara ya Ardhi muwe *firm* kwa sababu migogoro hii wala isingekuwepo kama ninyi mkiwa *firm*. Sheria ilishawapa mamlaka hayo. Wewe ni Waziri mkubwa kuliko Waziri mwingine yeyote inapokuja kwenye suala la ardhi. Hakuna Waziri mkubwa kwako na Bunge liliweka kwenye sheria, *Section* 181 ya Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 na inasema hivi;

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu, ''*on and after the commencements of this Act, notwithstanding any other written law to the contrary, this Act shall apply to all land in Mainland Tanzania mid any provisions of any other written law applicable to land which conflict, or are inconsistent with any of the provisions- of this Act shall to the extent of that conflict or that inconsistency cease to be applicable to land or any matter connected with* land''.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Bunge lilishakupa madaraka haya na sheria, maana yake wewe ulitakiwa uwe *neutral* kwa sababu mamlaka ya Rais kwenye kuangalia ardhi imeletwa kwako wewe. Haiwezekani mtu wa mali asili anakaa anachora ramani yake peke yake anaenda kuvuruga sijui anaenda kuvuruga na wewe upo. Wewe ulitakiwa uwe *neutral* na mikutano yote inayofanywa inayohusu masuala ya ardhi wewe ndiyo unatakiwa wewe Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *neutral* lakini *you have power*, lazima wewe uweze ku-*decide* kwamba hapana hiki kijiji tulishapitisha na TAMISEMI na sisi tumeshapima ardhi. Hii ni ardhi ya kijiji *period*, acheni kuogopana ogopana hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa utulivu wako mimi naamini utafanya hili, hii mantiki yake ni kwamba hata maafisa wako wanakuwa wakiendelea kusimamia madaraka haya ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki yake ilikuwa ni *clear* ili kuondoa migogoro hiyo ya ardhi, Waziri migogoro mingi sasa ukienda utaskia *GN*, hii habari ya *GN* halafu bado mnatuletea *GN* za Kiingereza ni mambo ya kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishapitisha sheria hapa kwamba sheria zote tutafsiri ziende kwa lugha ya Kiswahili na Bunge limepitisha sheria hapo na kazi zinaendelea kufanyika na Wizara ya Katiba na Sheria, sasa mkileta *GN* tena zianze kugombanisha watu eti kwa sababu ya lugha tu! Kwa nini? Kwani hizi *GN* mnawaandikia wazungu wa kutoka wapi sasa? Lazima *GN* ziwe kwa Kiswahili ili tuelewane vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaenda kule wazee wanahangaika wanasema huyu *GN* ni nani? Wanaanza sasa hata huko Mbeya huko nadhani hata wameanza kuita majina watoto kwamba *GN* sijui namba 28, sijui namba ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongezeka ukilinganisha wakati wa uhuru na leo tumeongezeka. Ukiangalia masuala ya kimataifa inaitwa *arch biodiversity targets,* walikuwa wanataka nchi angalau tuhifadhi *17 percent only*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ukiangalia *Montreal Biodiversity Framework* ya 2022 *at least 30 percent* halafu sisi tunaangalia 32, 40 na watu wanaendelea kuongezeka. Maeneo yaliyohifadhiwa tayari yanatosha. Waambie wa-*manage* kama hawawezi ku-*manage* usi-*accept* tena mambo ya ku-*create* maeneo mengine ya hifadhi kwa sababu inatuletea *pressure* na itatugombanisha, tuhifadhi kwanza hayo tuliyonayo na ilete *value* kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hatutegemei tena tusikie sijui wapi imeanzishwa hifadhi mpya na vitu kama hivyo. Tu-*manage* kwanza yale tuliyonayo ili watanzania waanze kufurahia haki zao au siku hizi mtu wa madini anatoka anakwenda anachukua hati anaanza kuvamia pori lao tu anaanza kulima, haangalii habari ya ile *land rights fine* mnasema ardhi siyo sehemu ya madini, kwanza ni *definition* ya kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunavyozungumza habari ya Dira ya 2050 lazima tuingie kwenye mjadala wa kui-*define* ardhi, ku-*include certain percents of rights* za madini na wanyamapori. Kama mnataka watanzania wawe na Dola 7,000 *in the next 25 years*, haiwezekani! Hii *definition* ya kikoloni ya kusema ardhi eti una-*remove all these precious resources*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wakoloni wali-*define* na sisi baada ya kupata uhuru tunashindwaje kuanza kuzungumza mjadala wake ili kuondoa vurugu hizi. Kila wakati unakaa tu unashangaa mtu ametoka sijui madini yamekuja na hati yake.

Yes, madini *rights but there are surface rights*. Lazima iwe *negotiated* Mheshimiwa Waziri. Siyo watu wanatengeneza tengeneza tu vitu halafu wanafikiri kwamba haki za watu wengine hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze jambo lingine la vijiji na Tanzania, Bunge lililopita nilimuuliza Waziri hivi siku hizi tuna *percent* ngapi ya ardhi? Akaniambia 58, *I was shocked* kwa sababu wakati ule ardhi ya vijiji ilikuwa ni 70% kati ya vitu vinavyofanya Tanzania iwe *unique* ni watanzania maskini kumiliki ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni maisha ya watu, tusikubali, hakuna nchi yoyote ambayo maskini anamiliki ardhi isipokuwa Tanzania na choko choko hizi zinaletwa kwa sababu mtu akiwa *jobless* na akiwa *landless* ni hatari sana! Lazima nchi ya ujamaa i-*affirm* na kulinda haki za watanzania walio wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ya mwisho kabisa, sitaki kushika shilingi.

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri uliniambia utamleta Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi, sasa Mzee hiyo si ni karatasi tu unaandika kesho tumpate? Hatutaki tena kumpata Mwenyekiti wa kututembelea. Kiteto ni *hotspot* kwa hiyo utuletee Mwenyekiti haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mwenyezi Mungu akubariki na nawashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Edward Olelekaita alikuwa ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu, tutaendelea jioni na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly na orodha hii itaendelea kutajwa jinsi muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa Kumi na Moja Kamili Jioni.

(Saa 7.01 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninamwita sasa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ili kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu. Ninaanza kabisa kwanza kwa kuunga mkono Hoja ya hii, ninaunga mkono sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioko katika taasisi hii kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara hii. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iendelee, Baba wa Taifa aliwahi kutuambia miaka ya nyuma, akasema ili nchi iendelee inahitaji vitu vinne. Tunahitaji watu, Ardhi, siasa safi na

uongozi bora. Haya ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote, sasa ukija leo tunajadili suala la ardhi, maana yake tunajadili nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika muundo wa Wizara, Wizara ya Ardhi imepewa jina Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa hiyo, kukiwa na migogoro ya ardhi mahali popote, tunaona ni Wizara ya Ardhi inahusika. Kukiwa na nyumba hazina ubora, kukiwa na makazi watu wanajenga kiholela, nyumba ziko za kiwango cha chini, tunapata picha kwamba hii ni Wizara ya Ardhi inahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona Wizara hii ina majukumu ya msingi, ina kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba wanatutengenezea utaratibu, wanatuletea sera ya namna ya kujenga nyumba zetu ili ziweze kukidhi mahitaji yetu. Nyumba za kila namna, iwe ni nyumba za daraja la juu, daraja la kati, daraja la chini. Iwe ni nyumba za bei nafuu, nyumba za bei ya juu, nyinyi ndiyo mnatakiwa mtuambie sera, lakini mtuelekeze hizi nyumba zijengwaje na tunapojenga tuweke mpangilio gani? Ni kazi ya Wizara hii kutuambia, wakishirikiana na Wizara ya TAMISEMI. Sasa hivi kasi ya maendeleo ya wananchi imekuwa ni kubwa. Ni kubwa sana, wananchi wanajenga kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupanga mji, kupanga, kupima, kurasimisha liko nyuma, haliendani na kasi ya maendeleo ya wananchi, ndiyo maana katika maeneo mengi watu sasa hivi wanajenga nyumba, hawana maelekezo, hawajaambiwa hapa patapita barabara, hawajaambiwa hapa patakuwa ni *open space*, hawajaambiwa hapa patakuwa ni kituo cha afya, hapa patakuwa ni shule, wao wanajenga tu. Baadaye Serikali inakuja kutumia fedha nyingi kuanza kutoa fidia kwamba sasa tunarasimisha hapa patakuwa na barabara, hapa patakuwa na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta barabara sasa zinazoenda kujengwa haziwi katika viwango vinavyotakiwa kwa sababu sasa unarasimisha watu walishajenga tayari. Kwa hiyo, tunadhani sasa ifike mahali, tuweke rasilimali nyingi kwenye Wizara hii, ipime ardhi yote, ipangilie ardhi yote irasimishe. Nimekusikiliza

Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yako, malengo ya mwaka jana kwa mimi kama Mhasibu na kama Mkaguzi, ninaweza nikasema hayajafikiwa. Kwa nini hayajafikiwa? Kwa sababu nimekusikiliza, suala la urasimishaji, suala la utoaji wa hati kwa wananchi halijafika zaidi ya 20%, umesema mwenyewe kwenye ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati walizopata wananchi kwa lengo tuliyoweka hatujafika 20%, sasa hii maana yake hatukufikia malengo. Kwa hiyo, hata kama tumepanga, hata kama tumerasimisha, lakini kama watu hawana hati maana yake malengo hayajafikiwa na thamani ya fedha inakuwa haijafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya fedha inafikiwa pale ambapo kile kilichokusudiwa kifanyike kinakuwa kimefikiwa, wananchi wanakuwa na hati wanazitumia hizo hati kwa ajili ya maendeleo yao. Tunajua wakiwa na hati wataenda benki watakopa, wataweka kama dhamana, wakiwa na hati watafanya lolote wanaloliweza. Hata mwekezaji akitoka nje ya nchi anataka eneo hilo wakaingia kwenye ubia, yeye atathaminisha kwamba mimi nina kipande hiki cha ardhi, miliki yangu ni hii. Kwa hiyo ninaomba muweke mkazo kwenye kupanga, kupima na kumilikisha, hili ni suala muhimu. Bunge hili lazima tusimamie kipande hiki tuhakikishe nchi yetu inapangiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo itaondoa migogoro mbalimbali ambayo inaendelea katika maeneo mbalimbali, ndiyo tutaondoa ujenzi holela, tutaondoa makazi yasiyofaa na ndipo tutajenga miji yetu ambayo itakuwa inapendeza. Tunahitaji maeneo yote yapimwe, na yapangiliwe ili tuhakikishe maendeleo yanakuwepo. Tunahitaji ardhi ya kilimo Mheshimiwa Waziri, tunataka ilindwe. Sasa hivi ongezeko la watu ni kubwa na hili ongezeko la watu, watu wanaenda kujenga sasa kwenye ardhi ya kilimo. Itafika mahali tutakuwa hatuna hata ardhi ya kulima, lazima twende kwa mipangilio ardhi ya kilimo ilindwe, ardhi ya ufugaji ilindwe ili hayo majukumu yaendelee kwa sababu hatutaacha kula hata siku moja, tunahitaji kuendelea kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Chuo chetu cha Ardhi kifundishe wataalamu na kinafanya kazi nzuri. Ninataka

kuwapongeza Chuo cha Ardhi, mnafanya kazi vizuri sana na mimi ninasema kwa sababu mnafanya kazi vizuri, mje sasa na Nyanda za Juu, njooni Mkoa wa Songwe. Sisi tutawapa ekari 200 mjenge tawi pale ili muwafundishe watu namna ya kuwa na nyumba nzuri, namna ya kupangilia maeneo na mambo mengine. Kwa hiyo tunawakaribisha, eneo lipo tutawapa bure nyinyi mje mfanye hayo mambo sisi tuweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji taasisi zetu zipangiliwe. ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na wa Awamu ya Sita kwa uamuzi wao wa kupangilia Mji wa Dodoma, tukaamua kwamba sasa Ofisi za Serikali zikae Mtumba. Zimekaa mahali pamoja, majengo mazuri, sasa kule ni mahali kwa utalii tunaenda kutalii kunapendeza kweli kweli, ninawapongeza sana. Sasa tunahitaji hata mikoani huko nayo ifananefanane namna hiyo, ipangiliwe wapi patakuwa na ofisi za kisasa, wapi patakuwa na *super markets*, wapi patakuwa ni maeneo ya biashara, wapi patakuwa ni nini, yapangiliwe. Mheshimiwa Waziri, tusiende kwenye utaalamu mkubwa sana, najua mnahitaji hela nyingi ili kutumia utaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Zanzibar, Hayati Karume alisema mnahitaji hela ngapi? Wakasema tunahitaji 'uhama' akasema hapana! Nyoosha kamba hapa, weka hapa barabara, weka hapa kila kitu. Tunahitaji kwenye vijiji, kama hela hazipo tupime kwa namna hiyo (kwa kunyoosha kamba) tuweke barabara, tuweke mipaka halafu baadaye utaalamu utakuja kuonesha namna jinsi sasa ya kutumia maeneo kama hayo. Tunahitaji maeneo ya viwanda yaeleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Songwe sasa hivi tunahitaji maeneo ya viwanda, wapi tujenge viwanda? Viwanda vikae maeneo ambayo yanafanana. Sasa sasa hivi kwa utaratibu uliopo, watu wanajenga viwanda kwenye makazi ya watu ambapo kunakuwa na mwingiliano na afya zetu zinakuwa siyo salama. Kwa hiyo, hilo ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mimi ninataka kusema, Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya kazi nzuri na sisi mwelekeo wa nchi yetu ndiyo tuliungana na Jumuiya ya Afrika

Mashariki. Tunataka kuunda nchi za Afrika Mashariki tuwe na Serikali *(Federal Governments)* za *East Africa*, na huenda twende mpaka Afrika tuwe na *United States of Africa*. Ili tuwe na *United States of Africa,* ili tuwe na umoja tukaungana, suala ambalo tuliona kwamba ni kitu muhimu cha kukiangalia ni suala la ardhi. Tukasema wakija tukiungana hapa watanyang'anya ardhi yetu. Sasa njia nyepesi pimeni, wamilikisheni yote, halafu twende sasa kwenye umoja huko wananchi wakiwa wanamiliki ardhi, itakuwa siyo tatizo na umoja wetu utakwenda kuwa na mafanikio mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri mimi kwa kweli ninasisitiza sana suala la kupima, kumiliki na kumilikishwa ardhi ni muhimu sana. Mkafanye hilo mje mlifanye Mkoa wa Songwe, sisi mlituletea fedha pale, tulijitahidi mlizotukopesha, tulifanya na tulilipa deni hatudaiwi, Wilaya ya Mbozi hatudaiwi. Tupeni nyingine, tupime makazi yapendeze hiyo itakuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Shirika la Nyumba. Shirika la Nyumba linafanya kazi nzuri na ninawapongeza sana kwa kazi wanazozifanya. Hili Shirika Mheshimiwa Waziri liwe la kibiashara, wapeni Mamlaka kamili waendeshe kibiashara tuondokane na taratibu zingine zile ili waweze kujenga nyumba nyingi na Watanzania waishi kwenye nyumba zenye ubora zinazokidhi mahitaji yetu. Kwa hiyo, Shirika hili likiwezeshwa, likiruhusiwa linaweza kufanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Songwe tunahitaji lije lijenge nyumba kama lilizojengwa huku pale Iyumbu na maeneo mengine, tunazihitaji na Songwe kule ili angalau na sisi mazingira yapendeze. Pia, tunahitaji pia Sera, Mheshimiwa Waziri tuletee Sera, tunapojenga nyumba nje pale panatakiwa pakae vipi mpaka kuingia kwenye barabara pakae vipi, hapo ndipo tukija na Sera ya namna hiyo, ndiyo itatuonesha sasa kwamba mji wetu utapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba hata kama ni ndogo, patapendeza, sasa hivi tunajenga nyumba mazingira ya nje hayapendezi, hata mtu akija hawezi kuvutiwa, ni wajibu wenu

kulifanyia kazi hilo na kuhakikisha mambo yanaenda vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri boresheni mazingira haya ya nyumba zetu, na makazi yetu ili sisi tufanye biashara na wananchi hawa wapige hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuhitimisha, mimi ninataka kusema kwamba mnafanya kazi nzuri na sisi Bunge tutawaunga mkono kwa kila namna ila tunataka mhakikishe kwamba majukumu yenu mnayatekeleza sawasawa kwa sababu hili suala la ardhi ni nguzo muhimu sana, suala la nyumba ni kitu muhimu sana, suala la makazi ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, na ninakushukuru kwa nafasi.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela atafuatia na Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo ajiandae.

MHE. FADHILI F. NGAJILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo. Ninapeleka pongezi zangu kwa Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake makubwa sana juu ya hii sekta ya ardhi. Mambo makubwa sana yamefanywa katika hii sekta na kila mtu ni shahidi, tukianza kuyaeleza hapa yatakuwa mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulifanikiwa kwenda kuona uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ambayo inaimarishwa nchi nzima. Tuliweza kwenda pale Holili Kilimanjaro tukaona ule mpaka kati ya Kenya na Tanzania jinsi ulivyoimarishwa, kwa kweli tunapongeza sana kwa ile kazi. Maana sasa unaziona alama, hata ukiwa kipofu utajua tu kwamba hapa kuna mpaka kwa sababu zimewekwa alama zinazoonekana na zinazoshikika na zipo kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Serikali kuendelea kuweka msukumo ili tuweze kumaliza maeneo ambayo bado hatujaimarisha mipaka, yale maeneo ambayo yanahusiana na historia yetu, zile kesi ambazo ziko kwa wasuluhishi wa kimataifa basi ziishe haraka, tuzisukume kwa wakati ili tusije tukarithisha haya matatizo kwa watoto wetu. Maana yake kuacha mpaka ambao haujaimarishwa maana yake unaacha matatizo, unaacha mpaka dhaifu. Kwa hiyo, siyo vizuri kuacha mpaka wa namna hiyo kwa vitukuu na vijukuu waweze kurithi changamoto ambazo zilitukumba sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia Wizara, mmefanya kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri Dkt. Akwilapo, Mheshimiwa Naibu Waziri Caspar na Katibu bingwa kabisa Dkt. Anthony Sanga, mnafanya kazi nzuri sana ya kuisimamia Wizara na kusimamia taasisi zake. *National Housing* ya zamani siyo ya leo, sasa hivi kwa kweli ni ya kibiashara imebadilika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia, amenibariki sana pale Iringa Mjini, ametuletea mradi wa shilingi bilioni 13.5. Katujengea *Iringa Commercial Complex frame* ambazo zitakuwa za biashara nyingi na za kisasa zilizojengwa kwa mitindo mbalimbali, zitakazovutia watu wengi sana wa kitaifa na kimataifa. Kama mnavyojua kwamba Iringa Mjini ni *hub of the Southern Highland.* Kwa hiyo, tunaamini sisi tutaweza kufanya jambo kubwa sana katika ile *Iringa Commercial Complex* ambayo inapatikana pale *opposite* na Chuo Kikuu cha *RUCU* au Benki ya Mkombozi. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu kwamba changamoto hazikosekani. Kwa mfano, *National Housing*, tuna hoja ya kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhusu nyumba za gharama nafuu imezungumzwa sana. Mimi ninafikiri Wizara sasa muwasaidie *National Housing* waje na mpango mzuri wa kujenga nyumba za gharama nafuu. Kama imeshindikana sasa twende tukajifunze kwa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mwananchi wa kawaida unapomweleza kwamba kuna nyumba ya shilingi milioni 200, 300

hakuelewi unachokisema, hiyo ni fedha nyingi sana. Hivi tunashindwaje kujenga nyumba ya shilingi milioni 30 ya chumba kimoja, viwili, sebule ili huyu anayeishi aishi kwa uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini basi bodaboda wataweza kununua nyumba za *National Housing*? Ni lini bajaji wataweza kununua nyumba za *National Housing*? Tufike mahali tuwe na vifurushi vinavyofanana na watu wenye kipato kidogo cha nchi yetu. Tunafahamu tunaishi kila mtu na kipato chake, sasa kuna watu ambao kipato chao kiko chini. Nitafurahi siku nikisikia *National Housing* wana *package* maalumu kwa ajili ya bodaboda tu. Wewe unajua yule bodaboda kwa siku anamrudishia yule mwenye pikipiki yake shilingi 10,000, *National Housing* umeshindweje kuwa na marejesho ya kila siku ili umjengee mtu nyumba, akufanyie marejesho? Umeshindweje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi iwe shilingi 10,000 lakini ninasema hivi kama wameweza watashindweje kufanya hayo marejesho? Bajaji watashindweje? Wanarejesha mpaka shilingi 30,000 kwa wale wenye bajaji zao. Mama Lishe na kadhalika, wote hawa tuwaguse tuanze programu hizo. Kama utaalamu ule tumeukosa, twendeni tukautafute duniani popote. Maandiko yanasema itafuteni elimu popote, hata ikiwa China nendeni mkatafute hiyo elimu kwa sababu jambo hili ni la muhimu sana kwa wananchi wenye kipato cha chini kuwagusa kwa miradi ya *National Housing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaomba kuzungumzia kuhusu uboreshaji wa nyumba zenye umri mkubwa, watu wamejenga makazi yao lakini yana umri mkubwa sana hasa kwenye miji yetu. Mimi huwa nikifanya ziara kwenye Kata mbalimbali kwa mfano pale Iringa Mjini, nikipita Kata zangu zote malalamiko ni hayo kwamba bwana tuna nyumba zina umri mkubwa, Serikali mnatusaidia kuziboresha? Siyo kwamba wanataka Serikali mkawajengee au mkawaboreshee hapana, ila Serikali inatengenezaje mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaboreshewa nyumba zao? Mbona nchi nyingine wanafanya? Mbona nchi nyingine wanafanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana majina yao utaona wengine nchi nyingine wanasema *housing rehabilitation programs*, nchi zingine wanaziita *settlement upgrading programs*, wengine wanaziita *housing enhancement programs*, wengine wanaziita *home improvement programs*. Hizi ni *program* za ku-*improve* nyumba ambazo zipo, wanaziboresha. Sasa ukipita kwenye Kata za Iringa Mjini hasa zile za katikati ya mji, kuna nyumba pale zina umri zaidi miaka 100 ziko pale. Nenda Kitanzini, Miyomboni nenda Makorongoni, ukienda Mshindo, ukienda Kwa Kilosa, angalia Gangilonga na Mkwawa, kote huku utakuta zipo nyumba ambazo zimeshakuwa na umri mkubwa sana zinahitaji tu kuboreshwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kutumia watalamu wako kuona namna mtakavyokuja na *mogaging system* nzuri, mfumo mzuri wa kuboresha hizi nyumba, la sivyo tutakuja kuwa na miji yenye majumba ya kale. Tutaishi kwenye nyumba za kale kwa muda mrefu kwa sababu, zitakaa kwa muda mrefu haziboreshwi na tayari watu wako na zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, hawafanyi maksudi kutokuziboresha, wengine wamezirithi zile nyumba zikiwa namna hiyo na uwezo wao ni mdogo, hawana uwezo wa kuziboresha zile nyumba zikawa za kisasa ili ziendane na wakati huu maisha yaweze kuwa mazuri. Kama unavyojua Mheshimiwa Waziri, tumewafundisha watoto wetu tangu shule tunawaambia kwamba, ili binadamu aishi anahitaji mahitaji matatu ambayo ni chakula, mavazi na malazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *there are three basic needs; food, clothes and shelter,* sasa huyu kijana anakuja kugundua kwamba, hii *shelter,* kwa maana ya makazi anayokaa, haifanani na ile tuliyosema *basic needs,* uhitaji muhimu kwa hiyo, nawaomba sana boresheni. Tutengeneze mfumo wa kuboresha makazi ya kale yenye umri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, nizungumzie suala la huu mfumo wetu wa *TAUSI,* ambao ni *e-Ardhi.* Mfumo ambao ni mzuri, unatusaidia katika kumilikisha ardhi. Ni mfumo mzuri sana, lakini pamoja na uzuri wake, una changamoto zake. Changamoto kubwa ni kwamba, walio wengi unawaacha huu

mfumo na sababu kubwa ni kwamba, hawana *accessibility to* TEHAMA! hawajui kutumia hii Mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hata hapa Dodoma mmegawa viwanja, wiki kama mbili-tatu hivi, lakini ndani ya nusu saa vile viwanja vilikuwa vimeisha. Mimi sitaki kuamini kwamba, viwanja vile walivichukua wananchi wa kawaida, siamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi wa kawaida hawana uwezo wa kuona ule mfumo. Kwamba, viwanja vile vimetoka ndani ya nusu saa! Siyo kweli. Wako ambao wamejiongeza, sitaki kutumia lugha nyingine, nataka kusema hawa wamejua ule mfumo na siyo ajabu wana taarifa za ndani kwamba, leo Saa Tano Asubuhi viwanja vitapandishwa kwenye mfumo, kwa hiyo wao wanaenda pale wananunua vile viwanja kwa urahisi kabisa. Wakivinunua, wengine wana *accumulate,* vinakuwa vya kwao, lakini wengine wanafanya *for business purpose,* wanakuja kuviuza kwa gharama kubwa. Sasa, ukiisoma hii Sera ya Taifa iko wazi tu, ililenga kuhakikisha walio wengi wananufaika na ardhi ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye Sera ya Taifa ya Mwaka 1995 imeweka kabisa, imeandika pale mwanzoni, hii Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 imeweka mfumo uliowazi wa kuwezesha raia wote kuwa na haki sawa katika kupata na kumiliki ardhi kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie huu mfumo ueleweke kwa watu. Tengenezeni mfumo ambao utafika kwa wananchi wengi, tusaidieni ili mfumo huu uweze kutumika na walio wengi, hasa hawa ambao hawana *accessibility to* TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu kodi ya ardhi. Naomba nusu saa tu! Nusu dakika…

MWENYEKITI: Mheshimiwa, nusu saa tena!

MHE. FADHILI F. NGAJILO: Mheshimiwa nusu dakika tu. Kuhusu kodi ya ardhi, mimi ninavyozungumza hivi, Mkoani kwangu watu wengi sana wameandikiwa deni la kodi ya ardhi. Mheshimiwa Waziri naomba hebu tulitazame hili suala, hawakatai

kulipa kodi, kodi ni haki, ni wajibu wa kila mwananchi kulipa kodi, lakini namna ya kulipa hii kodi ya ardhi! Watu wame-*accumulate* sana na unakuta wanadaiwa kodi kubwa, wengine wamerithi haya madeni kutoka kwa wazazi ambao wamefariki, kwa hiyo huwezi kujua hili deni limetoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaushauri wa aina mbili, ushauri wa kwanza ni Mheshimiwa Waziri kuhusu hii kodi, tunaomba walipe *by instalment*. Toa tamko walipe *by instalment,* watu wasipelekwe Mahakamani. Pili, nakuomba Mheshimiwa Waziri kama tuliweza kwenye kodi ya nyumba kupeleka kwenye mita za umeme, hii nayo itafutiwe mahali ikae ili wananchi wasiwe wanasahau kuilipa, inaleta bughudha, inaleta hali ya taharuki huko kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, haya. Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo atafuatia. Mheshimiwa Isack Joseph Copriano ajiandae na baada ya hapo, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniweka hai mpaka hivi leo na kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Lulindi na hali kadhalika, naishukuru familia yangu kwa kuwa makini na uvumilivu mkubwa, mimi nikitumikia Wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye suala la mfumo, kama ingekuwa nachangia karibuni ningetoa taarifa kwa mzungumzaji aliyepita kuhusiana na mfumo. Mimi ni miongoni mwa watu ambao nafikiri wameathirika na huo mfumo juzi, siyo wiki mbili, Nafikiri ilikuwa ni Jumamosi iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile kulikuwa na utaratibu wa kuuza viwanja ambavyo vilisemwa, mpaka Saa Nne kamili, viwanja hivyo 208 vingeuzwa. Mimi nikiwa na *laptop* yangu, nimekaa, nimeifungua, nasubiri na nimeshika kabisa ile *mouse,* nimegusa kabisa kiwanja, nasema hapa sitoki mpaka hiki kiwanja! Nifanyeje nikikamate?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufika Saa Nne kamili, nina-*click* hapohapo, naambiwa kwamba hicho kiwanja kimeuzwa. Nimejaribu kuangalia ndani ya sekunde tatu viwanja vyote 208 havipo! Siyo nusu saa, kama wewe ulivyosema, sekunde hazizidi tatu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida nilishangaa kwa sababu, mimi ni mtaalamu wa masuala ya *IT*. Pia, nimeshangaa nimekosaje kile kiwanja! Kwa hiyo, suala hilo nafikiri kuna changamoto sehemu. Mheshimiwa Waziri unatakiwa uangalie wapi panavuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shaka na wewe, kwa kweli natumaini sana uelewa na uwezo wako mkubwa na ninakuomba kwamba, uzingatie *history* ya Wizara hii isije ikaja ikakuhukumu siku za usoni. Wewe anza pale ulipoanzia kaza kwa nguvu zote. Nina uhakika utakuwa umefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kurudi katika changamoto za ardhi ziko nyingi sana, lakini mimi naweza kuzigawa katika makundi muhimu mawili. Kundi la kwanza ni lile la mpango, upimaji na umilikishaji; pale kuna tatizo kwa sababu, upimaji, umilikishaji na huo mpango umefanyika kwa kiwango kidogo sana. Hali hiyo imesababisha kuwa na kukosa taarifa sahihi zinazohusiana na masuala ya ardhi, ambazo zingeweza kutumika kwa namna moja au nyingine katika kufanya maamuzi au mipango mingi sana ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni lile la taarifa za ardhi, linalotokana na kutokuwa na ile tabia ya uadilifu. Tabia ya uadilifu na yenyewe imekuwa ni eneo kubwa muhimu sana, ambalo linachangia changamoto za ardhi zipatikane. Kwa mfano, kumekuwa na shida kwamba,

baadhi ya watendaji ambao siyo waaminifu wanashirikiana na baadhi ya madalali kufanya vitendo ambavyo siyo rafiki kwa kushawishi wadau, kwa maana ya wanunuzi wa ardhi, kuwauzia maeneo ambayo kwa namna moja yanakuwa yameuzwa hapo mwanzo, lakini pia, kuwauzia maeneo ambayo yametengwa kwa shughuli maalum. Hali hii imesababisha migogoro mikubwa sana ya ardhi na miongoni mwa inayotatuliwa ni ya namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana tu na kukosa uadilifu wamefanya kuichafua hii wizara kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kama nilivyosema pale mwanzo unayo kazi ya kuhakikisha kwamba, unafanya jitihada ya kudhibiti hali yoyote inayosababisha kuwa na changamoto inayofanya ardhi isitoke kwa uadilifu. Njia mojawapo kubwa ya kutatua changamoto hizi ni ile ya kufanya mipango, kwa maana ya mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la mipango miji linatusaidia sana kuhakikisha kwamba, maeneo yamepangwa kwa uhakika. Maeneo haya yatatengeneza taarifa sahihi katika mifumo, taarifa ambazo zitatuwezesha sisi wanunuzi pia kufahamu kiwanja hiki labda kinamilikiwa na nani au kimeuzwa au hakijauzwa, lakini hata katika mipango sahihi ya maendeleo Serikali inakuwa na uwezo mkubwa wa kujua tufanye nini kwa maeneo haya, ambayo yamepangwa na huku ambako hakujapangwa tunatakiwa tufanye kitu gani. Hiyo itakuwa imesaidia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningejaribu kushauri pia ni suala hilo la upangaji hususan katika maeneo ya vijiji. Uzuri Tanzania, maeneo mengi ya vijijini changamoto hizi ndiyo zinaanza, bado hazijawa kubwa sana kwa hiyo, Serikali kama mkiamua kupanga vizuri katika maeneo yale, bila shaka kwa kiasi kikubwa mtakuwa mnahangaika na migogoro hii, ambayo imejitokeza huku mijini kwa sababu, kule vijijini kwa maeneo mengi hayana migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia, maeneo kama vile halmashauri kuwe na mkakati madhubuti kabisa kuhakikisha halmashauri zote, hususan katika makao makuu kuwe kunapimwa, kwa ajili ya kujenga picha nzuri ya miji hii ambayo

itatengeneza muonekano mzuri wa nchi yetu. Sisi tukienda huko kwa wenzetu huwa tunaona jinsi mpangilio wa miji ulivyo na unatushawishi kuona kwamba, mambo kama haya yanafanyika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka mipango hii iko vizuri lakini shida kubwa ninayoiona ni katika utekelezaji. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, natamani sana kukushauri kwamba, kama inawezekana basi kuwe na kitengo maalum ambacho kinasimamia utekelezaji wa yale mambo ambayo mmeyapanga. Ile mipango miji iliyoandikwa katika makaratasi iwe inasimamiwa vizuri kabisa kusudi kuwe na hali njema katika utekelezaji wa mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja kama nilivyosema hapo mwanzo, naendelea kumtia nguvu Waziri na timu yake, wanafanyakazi nzuri, wote kwa pamoja, mitazamo yao, hali kadhalika dhamira zao ni njema kabisa, ninaziona kwa kadri wanavyoanza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchungahela ahsante sana. Nilimuita Mheshimiwa Naomy Duncan Mwaipopo, atafuatiwa na Mheshimiwa Isack Joseph Copriano. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

MHE. NAOMY D. MWAIPOPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi na mimi kuchangia kwenye Wizara hii muhimu na nyeti kwenye Taifa letu. Kwanza naanza na pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, naomba ninukuu kwenye Isaya 1:4, inasema, "*dhuluma inaleta laana na uharibifu*"; Methali 14:34, inasema, "*haki huinua Taifa bali dhambi ni aibu ya watu wote*". Hii Wizara ni nyeti na unavyozungumzia ardhi unazungumzia chakula, unavyozungumzia ardhi unazungumzia elimu kwa watoto wetu, unavyozungumzia ardhi

unazungumzia ustawi wa familia, lakini kwenye Wizara hii pamoja na jitihada kubwa ambazo zinafanyika, kule chini bado kuna migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri, hii migogoro asilimia 90, kwa *research* zangu nilizozifanya, inasabishwa kwa makusudi kabisa na watu wa Wizara ya Ardhi, Maafisa Ardhi. Kwa hiyo, naomba kupitia fursa hii, Waziri, mchukue jitihada za makusudi kwenda kutatua migogoro kule chini kabisa kwa sababu, sasahivi sisi tuko huku juu upatikanaji wa hati, angalau unaweza ukapata kwa urahisi, lakini yule mwanakijiji kule kwetu Kigoma kupata hati ni kanakwamba, anaomba ajira. Naona jitihada za Wizara, kweli wanajitahidi, wanafanya-*clinic,* wanatumia nguvu kubwa, lakini kule chini bado kwa hiyo, naimba Wizara, kwenye kipengele hiki waongeze juhudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hii mianya ya hawa watu kutokuwa waaminifu nadhani ni kutokana na mfumo uliopo kwa hiyo, naishauri Wizara, naishauri Serikali, hii Mifumo ya *e-Ardhi* isomane kwa sababu, Dira ya 2030, Mheshimiwa Rais anataka mifumo yote isomane, lakini hapa, kwa changamoto ambazo mimi naziona, hii mifumo haisomani. Unaweza ukaenda ardhi *document* haionekani kwenye mfumo! Leo haionekani, ukienda kesho inaonekana, kwa hiyo, nashauri hii mifumo isomane, ili kuepusha hizi changamoto na pia, kuepusha wale watu ambao siyo waaminifu kufanya mambo ambayo hayafai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo mifumo kusomana nashauri kwenye kipengele cha ukusanyaji wa kodi ya pango itafutwe namna nzuri, iwekwe kama kwenye LUKU, popote pale iwekwe, huyu mwananchi awe anakatwa moja kwa moja ile kodi ya pango, ili kuepusha ulimbikizwaji wa madeni ya pango la ardhi. Hii itasaidia ukusanyaji wa mapato na tutapata mapato kwa sababu, sasahivi tunapoteza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hati hazitoki, ina maana mtu kama hana hati hawezi kulipa pango lakini mtatoa hati na mtapata pango kwa njia nzuri ya namna ya kukusanya kupitia huko kwenye mifumo itakavyokuwa inasomana. Kipekee kabisa pia naiomba Wizara kuwa na mpango mkakati wa kuweka

dawati maalum kwenye ofisi za ardhi kila Mkoa, kusaidia wanawake wajane na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi hili la wanawake ndiyo waathirika wakubwa kwenye kipengele hiki cha ardhi. Huyu mwanamke *may be* amefiwa na mume wake, akiwa kwenye maumivu ya kufiwa na mume wake unaibuka mgogoro, ardhi hii siyo ya kwako! Mume sijui ilikuaje! Changamoto, yaani yuko kwenye maumivu anaongezewa maumivu, lakini kukiwa na dawati ambalo litamsaidia huyu mwanamke nadhani tutamsaidia na tutapunguza yale maumivu ambayo anayapitia. Hali kadhalika, wanawake wazee pamoja na wanaume wazee, kuwe na dawati maalum. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, atafuatia Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

MHE. ISACK. J. COPRIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa sehemu ya wachangiaji kwenye hii Wizara ya Ardhi, naomba Mungu anisaidie nichangie kwa upendo na niseme kabisa, sitaunga mkono hoja mpaka nipate majibu ya kuwarudishia wananchi Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza na upande wa uwekezaji, nchi yetu tunapenda sana wawekezaji na Mheshimiwa Rais amezungumza kinagaubaga juu ya kupenda wawekezaji. Mimi nilipata fursa ya kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa zaidi ya miaka 15 kwa hiyo, nilikuwa sehemu kabisa ya Serikali kuhakikisha tunatenga maeneo, kwa ajili ya uwekezaji, lakini maeneo mengi ambayo tumewapa wawekezaji wameyachukua yale maeneo wameyahodhi yale maeneo, wametengeneza hati yale maeneo, wamekwenda kutumia na si ndivyo kama tunavyokubaliana kwenye sera zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, wanakwenda kuchukulia mikopo. Ninataka nitoe mifano miwili, na nimwombe Mheshimiwa Waziri anisikilize, na nimwombe aende *site*. Kuna shamba lililoko Lolkisale la *Swiss Brothers*, zaidi ya miaka 20 miaka 30 mwekezaji alishika *acres* karibu 4,000 analima *acres* 100. Ukienda pale unakuta vikondoo kondoo pale basi. Wananchi wa Monduli wanapata tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye shamba lililoko Lolkisale la *TanFoam*, zaidi ya *acres* 6,000 mtu analima *acres* 200, *acres* takribani 4,000 hazina kazi. Ukienda kule unakuta shamba lile ameenda kuchukulia mikopo. Sasa, mimi ninafikiri ni lazima wizara hii irudi sasa ifanye tathmini ya uhakika juu ya wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si Monduli tu, nenda sehemu yoyote, nenda Karatu nenda Simanjiro utakuta hayo. Sasa, tukiwa tuna mitambo mizuri, na mimi ninawapenda sana, na ninawakubali sana wataalam wa Tanzania kwa kuandika *papers* na kutengeneza, lakini ku-*implement* hizo *paper* zao sifuri, na wako hapa wananisikiliza. Sifuri! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwa hapa tunakuja tu tunazungumza mambo mazuri tunawaaminisha Watanzania mambo mazuri tunakwenda kupima, tunakwenda kufanya nini, hamna kitu. Miji yetu imejengwa kiholela holela kila mahali, ilihali Maafisa Mipango Miji wapo, ukiuliza wanasema walishagawa, wao kazi yao ni nini? Kwa hiyo, mimi la kwanza ninahitaji kwa uhakika Wizara hii iende ikatathmini kuhusu wawekezaji walioko kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Wilaya ya Monduli, nenda Wilaya ya Karatu, nenda Wilaya ya Simanjiro, nenda Wilaya ya Longido, nenda wilaya zote zile, fanya tathmini. Hivi hawa wawekezaji tunapata faida gani? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu migogoro. Mimi ninafurahi sana Wenyeviti wa Vijiji watanisamehe; ninawapongeza sana TAMISEMI kwa kuwanyang'anya Wenyeviti wa Vijiji mihuri. Wanyang'anyeni hawa na msiwarudishie. Kama watanihukumu kwa hilo 2030 wanihukumu nayo. Katika watu

wanachangia nao kwenye hii mihuri yao ni Wenyeviti wa Vijiji. Unakuta viwanja vinagawanywa, maeneo yanagawanywa bila kufuata utaratibu Mwenyekiti amegonga pale muhuri. TAMISEMI ninawapongeza kwa hilo na wasirudi nyuma, wasiwarudishie mihuri hiyo. Wameiharibu sana nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hiyo tunasema wenyeviti wanaharibu lakini watumishi wao Mheshimiwa Waziri, na nitampa mifano; kwa mfano hivi juzi tumeona kwenye mtandao nikihangaika juu ya eneo la wananchi, eneo lililopimwa kwa ajili ya malisho lakini watu kwa kushirikiana na wenyeviti wanakwenda kupima wanaweka hati ya kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ni hati hii hapa niliyonayo na baadaye nitampa Mheshimiwa Waziri halafu muhtasari wa kijiji wa mkutano mkuu ambao huna saini unakwenda kutiwa saini na Afisa Ardhi Mteule, halafu unamuuliza mtaalamu ambaye analipwa fedha za watanzania anasema muhtasari hauna shida. Muhtasari ya Serikali ya Kijiji ambao unagawa ardhi lazima usainiwe na wajumbe wote na mkutano mkuu uliohudhuria pale kwenye ule mkutano. Sasa unapomuuliza mtaalam wako uliyenaye kule Halmashauri anakwambia ooh sasa! Huo mkutano umekaa saa ngapi, ukachapa muhtasari ambao haujasainiwa? Haya ungechapa basi ambatanisha na huku nyuma na yale...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Waitara.

TAARIFA

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mchungaji na mkulima mwenzangu, Mbunge wa Monduli, kwamba pale Tarime Vijijini kuna muhtasari ambao Mwenyekiti wa Kijiji aliyekuwepo anaukataa, sasa anaukataa. Maafisa Ardhi wa Wilaya na Wizara wametoa hati ekari 351 na kuna wananchi zaidi ya kaya 75 wanakaa pale. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ISACK J. COPRIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa mikono miwili, ndugu yangu kumbe tuna-*face* mambo magumu wote kwenye hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kwenye mkutano, unauliza, unataja majina, unaambiwa sisi hatujui, hili hatulijui. Jana nimemaliza mkutano na leo mtauona. Sasa, hawa wataalam kazi yao ni nini? Wao si ndiyo washauri wa kushauri na kujiridhisha na jambo ambalo limeletwa Halmashauri kwa ajili ya uhakiki ili kuruhusu kusajili hii hati ya kimila inayotoka? Hii si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu ninamwambia Mheshimiwa Waziri atoke ofisini aende *site*, hatumwoni. Tunaona *operations* za Waziri Mkuu zinakaa, zinakuja hoja za ardhi nyingi za kutosha. Ndiyo sababu siku ile nikauliza swali hapa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya tathmini na ufuatiliaji kazi yao nini? Imewezeshwa? Sasa hawa Wizara wakikaa tu wakasema wanawategemea Makamishna, Makamishna ndiyo watakwenda kutatua matatizo hayo? Haya, tatizo kama hili, eneo la malisho mtu ameuziwa, eneo ambalo limetengwa na vijiji na wananchi wanalijua! hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo ndilo ninaliomba nipate majibu ili niachie shilingi, kwa sababu nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lililoko Lolkisale la mwekezaji anayeitwa Brown Matthew, ambapo Kamishna alishaandika barua ya kumtaka Brown ku-*surrender* hati yake ili eneo lililozidi la Monduli liondolewe kwenye hati yake ili lirudishwe kwa wananchi, lakini kila siku kukicha wananchi wangu ni kushikwa kupelekwa Mahakamani, kupigwa faini kwa ardhi yao ambayo imepimwa na wana hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti nimekwenda kwa Mheshimiwa Waziri, nimeshawaonesha mpaka Wizarani, Kamishna ameandika

barua kumtaka ku-*surrender* hati, kwa nini tunakula muda? Kila siku tunakula muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate majibu ya kuwarudishia wananchi wangu Kijiji cha Odonyo juu ya ardhi yao ambayo imehodhiwa na mwekezaji. Mwekezaji amepewa hekta 2,000 sawa na *acre* 5,000 akajiongezea hekta 1,420 za Wilaya ya Monduli. Kwenye barua nimemwelekeza kabisa, wakati unapokwenda kutengeneza hati jiridhishe usiingie Wilaya ya Monduli; iko wizarani, na kamishna anayo. Halafu kila siku tunaomba haifanyiwi kazi. Kwa nini mnataka Watanzania waache kufurahia ya matunda ya Mama Samia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Waheshimiwa Mawaziri wanapokaa kwenye Baraza hawauoni kwamba Mama Samia anataka kuacha tabasamu kwa Watanzania? Hawaoni? Mama yetu mpendwa Mama Samia anakaa anawaambia ninataka nione Watanzania wakifurahi, wao wakikaa, wakimaliza Baraza wanaondoka, hawajui kuwa kuna machungu Watanzania wanakutana nayo huko nyuma. Ndiyo sababu Mheshimiwa Rais amewateua wawe mawaziri ili wamsaidie kazi nyingine ndogo ndogo ambazo yeye hawezi kuzifikia. Wanataka akifika Monduli apate bango, akifika Waziri Mkuu apate bango, inawezekana? Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka Mheshimiwa Waziri akisimama kwa ajili ya jambo hili nipate majibu kwa sababu yote ninajua, wamewaandikia sijui ku-*surrender*, wameandikia sijui Kamishna Arusha ku-*surrender*, hivi maana yake nini? Ninakwenda kwenye mkutano ninakosa majibu. Ninakuta watu 2,000, Mheshimiwa Mbunge tupe majibu tumekuchagua wewe. Ninawaomba kwa kweli mimi sitaunga hoja mkono bila kupata majibu nitakayowarudishia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, niombe hizi mahakama za ardhi huko kwenye wilaya zetu, kama kutawezekana, mabaraza sijui mabaraza; kama zitawezekana hebu zirudishwe huko mahakamani. Kwa sababu nayo pale jamani jamani jamani, hivi nyini hamuoni?...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatana Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Sigrada Mrigo ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara muhimu sana katika nchi yetu. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ameteuliwa kwenye Wizara ngumu sana yenye migogoro mingi. Tunamwomba aendelee na kasi, Naibu wake tunamshukuru sana, Katibu Mkuu ni mzoefu ametoka Wizara mbalimbali, Naibu Katibu Mkuu, makamishna na Watendaji wote wa Wizara. Ninawashukuru sana kwa sababu wanatulindia ardhi yetu tunaendelea kuijenga na kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote ninapoangalia hii Wizara huwa ninasama kitu kinaitwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sasa, huwa wajiuliza, hivi hiki kitengo kingine cha maendeleo ya makazi kiko wapi? Kiko wapi? Hivi *National Housing* inalinda tu watu wenye fedha na watumishi ndio inawajengea? Yaani hiki kitengo sijawahi kumwona mtumishi wa ardhi au *National Housing* anakwenda kuhubiri vijijini watu wafugaji ambao tuna ng'ombe 200, 300, 400, kwamba tutakujengea nyumba ya bei nafuu halafu wewe utalipa polepole kwa kupitia mnada. Hatujawahi kuona! Ni nini kinaendelea sasa? Hapa tunasoma ardhi mimi ninaona watu wanapima, wanamilikisha ni kweli kwenye Majiji lakini vijijini kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine najiuliza, kuna kitu kinaitwa *slums* halafu kingine kinaitwa *squatters*. *Slums* ni makazi mabovu kidogo. *Squatter* ni makazi mabovu zaidi. Mimi kwa Kiswahili changu niseme hivyo. Nani anatengeneza *slums* na nani anatengeneza *squatter*? Nani anatengeneza? Kama leo Bunda kuna Mji wa Nyamswa umekua, wapimaji hawapo. Leo kuja kupima kiwanja ni mamilioni ya hela. Mji wa Bunda umekua, wa Nayamswa umekua hamna wapimaji; na wa Hunyari umekua hamna wapimaji, Mugeta umekua hamna wapimaji, Mihingo imekuwa hakuna wapimaji, yako maeneo yamekuwa *centre*

hayana wapimaji. Nani anatengeneza *squatter* kama si Wizara ya Ardhi? Nani anatengeneza *squatter*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wewe utaenda watu hao wamekaa pamoja kwa muda mrefu wamejikusanya, halafu wanaenda. Ninajiuliza tena swali, hivi leo tulipimaje nchi nzima makazi ya nyumba? Wanaita makazi gani yale; leo hata nyumbani kwangu kila nyumba ina namba. Tulipimaje? Tulitumia fedha kiasi gani? Leo tuna vyuo vina watoto 200, 300 maelfu. Leo tukisema Chuo cha Ardhi cha Dar es Salaam vije hapa Dodoma wakae hapa wiki tatu ardhi yote itapimwa. Kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kwa mpango huu ambao waziri ametuletea kwamba ana kasi ya kupima maeneo na kumilikisha inawezekana? Hili neno tumeliimba hapa; hadi naenda kugombea Ubunge, kila miaka mimi ninaimba hili neno. Tunafanyaje? tusaidiewe namna ya kuleta mtu wa kupima, waache mambo ya fedha. Tuvitumie vyuo vyetu vikuu, vile vyuo walete wataalam wapime. Tulipelekaje makazi leo kila mtu ana namba? Leo tumekuja Dodoma tunaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge wameongea mambo mengi sana; nimwombe hili la viwanja 28 la juzi, akaunde tume uone kuna nini. Hivi, Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tunazungumza hapa tunaondoka hakuna hata kitu kinaamuliwa. Aende akafuatilie hivi viwanja vimeuzwa kwa dakika moja vimeuzwaje? Tupate majibu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lina uwezo wa kuunda Kamati ya kuangalia jambo, kuna nini kimeendelea? Tuletewe taarifa kwamba kuna kitu gani kimekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii wizara ina viongozi wote ni wageni. Ninajua wanachapa kazi; Mungu atawasaidia wachape kazi. Haya maneno tunazungumza. Niombe kwenye mji wangu wa Bunda iko miji saba ambayo ni miji mikubwa na inayokua, waje wakanisaidie kupima ile miji ili tuweze kupata unafuu, tusitengeneze tena *Squatter* wala *slums*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wengi wamenunua nyumba, ama amepewa na baba yake, ama amepewa na ndugu yake ama amenunua nyumba yake, uhamisho wa kuhamisha kiwanja kwenda kwenye mmiliki mwingine ni mamilioni ya fedha. Wanatoa wapi? Kwa nini tusitengeneze mfumo ambao kwa kweli mtu akipima ardhi anapima kwa bei nafuu? Akihamisha kiwanja ambacho amepewa tuone amepewaje? Kuna nini sasa hata kama kila kitu ni fedha? na sisi ardhi ndiyo inaleta hela. Leo nchi yetu tungepima viwanja vyote vya ardhi vyote tungefuta kodi nyingi nyingine ambazo hazina faida kwa wananchi. Zote tungekuwa tumefuta watu wangekuwa wanapata fedha kwa kutumia ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, amezungumza mtu hapa kwamba ardhi tunafanyaje walipe? Tuweke kwenye LUKU. Kama kuna maeneo yana umeme yamepimwa na mtu analipa kiwanja chake kinampa shida, viwanja vyote anapolipa tuviweke kwenye LUKU, akilipa umeme analipa na fedha ya ardhi humo humo ndani, hataona madhara au tuweke kwenye maji, tuweke kwenye LUKU. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri atengeneze taratibu, Aamke na watu wake, wafanye kazi. Tupime ardhi, bila kupima ardhi wakamilikishwa watu itakuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina uwezo mwingi sana wa kuwasema, nitaunga mkono hoja yao. Serikali wapeni fedha ili wafanye kazi vizuri kwa sababu sasa nyie mmekuja juzi, tukisema mmalize matatizo yoyote ya miaka 300 hamtamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Nilikwishamwita Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Sigrada Mligo atafuata, Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas ajiandae.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninawapongeza sana Watendaji wa Wizara hii kwa sababu kwa kweli kazi katika ardhi ni kubwa. Ninaona takribani kila maeneo wakipita wanakutana na migogoro ya ardhi na kila jambo, Mungu awatie nguvu wapambane, ardhi ni kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ni mmojawapo wa kuamini hizi falsafa za Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, kwamba, kwa maono yake aliyosema ili nchi iendelea inahitaji mambo mane. Ni kweli hakuna jambo unaweza ukafanya bila ardhi, lakini tunashukuru kwa uongozi bora uliopo, pia rasilimali watu ambao wanaleta maendeleo, pamoja na siasa safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka kabisa kwamba, ardhi mwanadamu wa kwanza alivyotoka katika bustani ya Edeni Baba yetu Adamu, kitu pekee ambacho alipewa na Mungu ni ardhi, alimwambia nenda kalime ardhi, jasho likutoke ili upate maisha. Kwa hiyo, ustawi wa mwanadamu huwezi kutenga na ardhi. Mwanadamu yeyote ili awe na ustawi anahitaji ardhi. Hakuna uwekezaji utaufanya bila ardhi, hakuna kilimo bila ardhi, hakuna malisho ya mifugo bila ardhi. Hakuna uwekezaji utaufanya bila ardhi. Kwa hiyo ardhi ni jambo muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushukuru Tanzania yetu waasisi wetu wametuweka kwenye ujamaa mzuri sana. Ndiyo maana kila Mtanzania ana uwezo mkubwa wa kurithi ardhi tena kiasi chochote anachotaka, tena popote. Kama mimi ninaweza nikatoka Manyara nikaenda Mbeya pia nikamiliki ardhi. Kwa hiyo, tushukuru Mungu kwa waasisi wetu waliotuweka katika ujamaa wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinanipa hofu ni hii kasi kubwa ya uvamizi wa ardhi. Watu wanavamia maeneo ya wazi. Maeneo yalikuwa ya watoto wanacheza hapo, maeneo watu walikuwa wanafanyia mikutano, maeneo ya milima, vyanzo vya maji, maeneo ya uwekezaji, migogoro mitupu. Mtu anavamia eneo ambalo miaka yote lilikuwa liko wazi, lakini ukikuta anajenga ana vibali vyote, ana *title* anayo mpaka *building permit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji watusaidie, maeneo ya wazi ni lazima yawepo na watoto lazima wapate maeneo ya kucheza, maeneo ya bustani. Hatuwezi kuwa na sehemu zote zimevamiwa na tunanyamaza. Wakivamia maeneo ya wawekezaji kuna debate. Wakulima wanaambiwa labda basi sawa, ukivuna labda usiendelee, anavuna anapanda tena. Sasa kama tuna sheria tujaribu kutumia hizi sheria ili kuona kwamba uvamizi huu ambao mwisho wake ni migogoro uweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la migogoro ya ardhi. Wenzangu wamelisema sana, mimi hasa nimesimama kwa ajili hiyo. Kwa sababu ukifika Manyara kila sehemu kuna migogoro mikubwa ya ardhi. Migogoro kati ya mtu na mtu, ya kifamilia. Hii migogoro inaendelea kuwepo ingawa kuna mabaraza ya ardhi huko. Sijajua utaratibu wa mabaraza ya ardhi. Pengine hao watu wanaoendesha haya mabaraza ya ardhi kule Wilayani ikifika mahali kuwe na ukomo wa kufanya hizo kazi zibadilishwe, kwa sababu wengine kwa kweli wamekuwa sababu ya watu wengine kukiukwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji, kwa bahati nzuri kuna vijiji ambavyo tayari wana mipango bora ya ardhi lakini hazifuatwi ilihali jamii iko pale na sheria iko hapo. Hebu tujaribu kuona hivyo kwa sababu wakulima na wafugaji ni sehemu ambayo wanapigana hadi wanauana, wanakosa ile *political rest* ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wawekezaji, hivi wawekezaji, kwa mfano kule kwangu kuna wawekezaji wengi wa mashamba akina Ngano *Limited*, siku zote kuna vurugu. Mwekezaji ambaye ana mkataba ana andiko kwamba amechukua eneo hili kwa sababu labda azalishe ngano, lakini panabaki pori na wakulima ambao wana mahitaji ya eneo wakiona lile pori bado liko pale inakuwa sehemu ya uvunjifu wa amani, inakuwa hata tishio kwa wakazi wa hapo. Kwa nini sasa tusichukue hatua tukaona kwamba haya maeneo ya mwekezaji ambae hayaendelezi sheria yetu inasemaje kwa mwekezaji ambaye amechukua eneo letu na haendelezi? Hivyo ni lazima tufanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna wawekezaji hawa ambao nimesema ni wachimba madini. Hao ni sababu mojawapo ya migogoro pia, kwa sababu akienda mahali akipata leseni yake wale anaowakuta pale ni kama hawana haki. Ni kweli lazima yule mwenye eneo pale anapaswa aidha afidiwe au waongee, sasa nilikuwa ninafikiria hii sheria mchimbaji wa madini mpaka apewe leseni, kwa nini tusiletewe sheria huku kwamba, asipewe leseni mpaka kuhakikisha kwamba amekuja na *document* inayoonesha umiliki wa eneo analoenda kuweka uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limeathiri watu wengi sana kule Manyara ndiyo maana ninalisema. Kwa sababu akifika hapo anathaminisha ile ardhi yako na bei ya soko na kule vijijini thamani ya ardhi ekari moja ni shilingi 500,000; 400,000 au 200,000 huku yeye anaenda kupata mabilioni ya hela. Ni kwa nini isingekuwa ni bahati ya yule mtu anayemiliki eneo pale, kwamba huyu mwekezaji pengine tufanye ubia au kwa namna yoyote na yeye akanufaika kutoka pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kuhusu mipango miji. Tunajua mamlaka ya mipango miji kweli ni ya Mkurugenzi, kwa hii kasi tunayoenda watu wanahitaji maendeleo, wanahitaji nyumba bora, wanahitaji umeme kwenye nyumba zao, na wanahitaji maji kwenye nyumba zao, watu wameongea hapa tunashindwa nini kupanga miji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hizi wanasema *squatters* ndiyo ambazo zinashika kasi na tunaona mtu anaanzisha kijiwe, anaweka labda mgahawa hapo kidogo kidogo kamji kanahamia na watendaji wanaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hii miji midogo haijakuwa ingekuwa ni *role*, aidha Mkurugenzi au Wizara kuhakikisha kwamba hii miji midogo inayoanza kukua lazima ipate mipango bora ya ardhi ili Tanzania siku moja makazi yetu yaonekane bora. Ukitaka kupeleka umeme kusiwe na shida, ukitaka kupeleka maji kusiwe na shida, jinsi ya kutoa maji taka kusiwe na shida na ikitokea majanga ya moto kusiwe na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kuna *TBA*, wakala wa majengo, kuna Watumishi *Housing*, kuna *National Housing* hawa wapo *special* kwa ajili ya watumishi wa umma pengine na watu wenye fedha kwa sababu sijawahi kuona wakisaidia huko vijijini na watu wa chini. Wakijenga nyumba wanakopesha watumishi, wakijenga nyumba tunakopeshwa sisi Wabunge. Ni lini sasa watajenga nyumba ambayo ni kwa gharama ndogo kulingana na malighafi iliyopo eneo wawasaidie wale wakulima na wafugaji wakawajengee nyumba *at least* tukaenda na mipango bora ya ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye KKK. Ninakumbuka Halmashauri hata nyingine ziliwahi kukopeshwa hela ili ku-*facilitate* mpango wa KKK. Ni mpango muhimu sana ili kila mmoja aweze kumiliki ardhi na hii itapunguza migogoro. (Kupanga, Kupima na Kumiliki ardhi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninajua limeingiliwa na siasa lakini bado tunayo *role* ya kurudi kwa wananchi wetu tukawa-*organize* wenyewe wakatambua ili wakubali huu mpango shirikishi wa kuwapimia maeneo na kuwapa hati. Nimeona sijui ni kwa nini hata Wizara ilikuwa imeshaweka lengo la kupima hati miliki, hati 520,000 lakini wameweza ku-*facilitate* kwa asilimia 19 na *point*. Sijajua ugumu upo wapi lakini tukiweza kuwashawishi na kuwaelimisha wananchi wakaelewa umuhimu na faida iliyopo kwo ya KKK hizi tatu, hamna mtu ambaye hapendi kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi itamsaidia kwenda kukopa, ardhi itamsaidia kumpa *confidence* ya kufanya maendeleo katika eneo lake. Kwa hiyo, tuwasogelee wananchi ili huu mpango wa KKK uweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *speed* hii ya utoaji wa hatimiliki pamoja na hizo hati za kimila. Sijajua kwa nini Wizara inachukua muda mrefu sana ili mtu aje apate hatimiliki au aje akate hati hii ya kimila, pengine hizi mngezi-*digitalize* na ninaona hata mafanikio yenu ni madogo. Katika malengo yenu ya kutoa hatimiliki 500,000, mmeweza kutoa 107,000 nafikiri, sawa na 21%. Kwa hiyo, kuna *something wrong in between*. Tunawaomba

hawa watusaidie waongeze *speed* ili wananchi wengi waweze kumiliki ardhi yao na wakiwa na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Rahhi. Nilimwita Mheshimiwa Sigrada Mligo atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo ajiandae.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupewa nafasi hii ya kuchangia jioni ya leo. Kuna sababu nyingi ambazo zinasababisha migogoro ya ardhi lakini mimi nitajikita kwenye sababu kuu kama tatu au nne hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wakati Sheria ya Ardhi inatungwa mwaka 1999, ikaja mwaka 2002 tukaanzisha Mabaraza ya Ardhi, lengo lilikuwa ni kutenganisha kati ya kesi za kawaida na kesi ambazo zinahusika na mambo ya ardhi. Kwa wakati huo kesi zilikuwa zikichanganywa kwenye Mahakama moja lakini cha ajabu ninataka nikupe *principle* fupi ya huu mfumo ulivyo na sijui nani alidanganya kuwachoresha kwenye huu mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwenye hatua ya Kijiji, Mwenyekiti wa Kijiji, mpaka leo hii ana-*transfer* ardhi, anauza, anasimamia ununuzi wa kuuziana ardhi na anachukua kitu kinaitwa 10% mpaka leo hii ninavyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, mmetunga Mabaraza ya Ardhi ya Kata, haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanawajibika Halmashauri. Ukitoka pale huyu Mwenyekiti wa Baraza a Ardhi anawajibika Halmashauri chini ya wale wanasheria wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka pale ukienda kwenye Mahakama ya Ardhi ya Wilaya, Mwenyekiti yule au Hakimu yule hawajibiki popote zaidi ya Wizarani, lakini hiyohiyo kesi ikishatoka Mahakama ya Ardhi ya Wilaya ukitaka kukata rufaa unaenda Mahakama Kuu ya kawaida, huu mfumo tangu lini usitarajie kesi au migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anawajibika anapojua yeye lakini mmeenda mbele zaidi, haya mabaraza ya ardhi ya kata hamuwalipi hata posho na ndio maana Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanatenga kesi, yanawaambia *parties* unatakiwa uchange shilingi 150,000 na wewe 150,000 yanaenda *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Mabaraza ya Ardhi ya Kata sasa hivi ni Mahakama ndogo, tena watu wanaona bora ya Mahakama ...

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Motto.

TAARIFA

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Sigrada, siyo kweli Mabaraza ya Ardhi ya Kata kwamba hawalipwi. Mimi nimefanya kazi Wizara ya Fedha, nimeidhinisha malipo mengi tu yanayohusika na vikao vya Mabaraza ya Kata ya Ardhi, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, unapokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Motto?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa taarifa. Taarifa nilizonazo wanapeleka posho ya shilingi 10,000. Kwa hiyo kama ni hizo unamaanisha ninapokea lakini hawana mshahara, *trust me*. Kama mimi ni muongo fuatilia, huenda ulikuwa unalipa *wrong person*. Baba yangu mdogo mwenyewe ni mjumbe kwenye baraza, kwa hiyo nina taarifa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea nimetumia dakika moja. Ukifika Mahakama ya Ardhi ya wilaya unakata rufaa kwenye Mahakama Kuu ya kawaida lakini huyu Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi *administratively* anakuwa *treated* na Wizara. Ukija kimahakama anakuwa *treated* na Mahakama Kuu, unawezaje ku-*solve* migogoro ya ardhi kwa *style* hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Mitaa, ambao kuna watu walipendekeza hapa ambao wanafanya kazi ngumu sana kwenye nchi hii na wakati wa uchaguzi mmekuwa mkiwatumia sana, hawana hata posho, atashindwaje kuhukumu kesi ya Juma na John waliopigana usiku mtu na mume wake achukue shilingi 50,000? Ndio maana leo hii mtu akigombana na mke wake asubuhi jioni wamepatana, anawaza akienda Ofisi ya Kijiji hela atakazotozwa bora apatane tu na mke wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakwambia ukweli vijiji vimekuwa vikinyanyasa watu, vikitoza mara ya mgambo, mara sijui ya mlinzi, vijiji vimeenda mbele zaidi vinawaweka wananchi hadi *lock up*. Hawana posho, walipeni posho hawa Wenyeviti hata shilingi laki moja, moja kwa mwezi. Mnawatumia sana hamuwapi chochote ndio maana wanahukumu kesi wanategemea posho wamnyonye mwananchi. Ofisi za vijiji na kata, tulitarajia iwe ni huduma kwa wananchi na siyo iwe ni biashara kama ambavyo ipo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; tumekuwa tukichukua maeneo ya umma kwa lengo la miradi ya Serikali, siyo kosa lakini sheria imeenda mbele zaidi. Sheria inayoitwa *The Land Acquisition Act*, (Sheria ya kutwaa eneo) lakini imeenda mbali zaidi, sheria ile imeruhusu Serikali kuchukua eneo la mtu yoyote, wakati wowote pale ambapo lile eneo ni kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hiyo imeenda mbali zaidi, *subject to compensation*. Huruhusiwi kuchukua eneo la mtu, wala Serikali, wala mtu binafsi hata kama ni kwa mradi wa Serikali kama hujalipa fidia. Hata hivyo, sisi kama Serikali tumegeuza kwamba kwa sababu mradi ni wa Serikali na mnaenda mbali zaidi mnadanganya wananchi kwamba ardhi ni mali ya Serikali, aliyewaambia ardhi ni mali ya Serikali ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the law is too clear*, sheria ipo wazi, imesema, *all land is public under the trusteeship of the President*. Maana yake ni nini kwa tuliokimbia shule? Ardhi yote ni mali ya umma, Rais ni mdhamini tu. Tusidanganye wakulima wa viazi vijijini, tunachukua maeneo yao, mnaishia kusema ni mradi wa

Serikali, ni mradi wa Serikali. tulipe fidia pale tunapopitisha miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto bahati mbaya siku hizi leo unakutana na Waziri huyu, kesho ameshatenguliwa anakuja mwingine. Tumekuwa na matamko ya kisiasa, tukifika kwenye vijiji, kwenye mikutano ya siasa tunaahidi kuwalipa watu fidia, kesho na kesho kutwa yule Waziri aliyeahidi ameshatenguliwa, anakuja mwingine hana taarifa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* hakuna mwenye hati miliki na uwaziri wake kwa sasa hivi, (ninaweza nikasema), tofauti na miaka ya nyuma unakaa miaka mitano. Kwa hiyo ukirudi tunakuhoji bwana uliahidi. Sasa hivi anaahidi mwingine, atakayerudi ni mwingine, ndio maana migogoro haiishi, tatizo linaanza upya kwa sababu huyu aliyekuja hajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine; mfumo wa maafisa ardhi kwenye nchi hii. Kuna Mbunge mmoja amezungumza hapa asubuhi, maafisa ardhi wa halmashauri zetu wanawajibika Wizarani lakini yupo Ofisi ya Mkurugenzi. Mambo haya mlibadilisha mwaka 2020, lengo lilikuwa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutatua migogoro, afisa ardhi wa halmashauri ya mji hawajibiki kwa Mkurugenzi, anawajibika Wizarani. Haiwezekani hawa watu wazima tu. Je, wanawajibika TAMISEMI au Wizara ya Ardhi iwe na *mandatory* yake au wawe na mamlaka yao kama ilivyo *TANESCO*, kama ilivyo *EWURA* na mamlaka nyingine. Ndio maana kuna *contradiction* hata kwenu wenyewe kwa wenyewe, kwa sababu ya hii mifumo mliyoitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine amelizungumzia mtu mmoja, Mheshimiwa mmoja hapa, mambo ya uwekezaji haya. Hivi aliyetudanganya kwamba mwekezaji ni mtu *special* wa kuhurumiwa ni nani? Kwa sababu nchi hii wananchi wakilalamika, aah! Kuna mwekezaji, kuna mwekezaji. Hakuna mwekezaji (ninaweza nikatumia neno gumu), hakuna mwekezaji mjinga kwenye dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji yeyote akija, ameshapiga hesabu zake ameziweka mfukoni ila sisi sasa tunaona amekuja kutuokoa.

Katika watu wanaonyanyasa wananchi kwenye nchi hii, wananchi wa maeneo husika ni wawekezaji mnaotuletea na wanakuja na full document. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahitaji kushirikishwa, ukimshirikisha hana shida. Anakuja mwekezaji awe wa madini, awe sijui wa nini, anakuja ana-*full document* kijiji hakina taarifa. Ila wanasema kuna mwekezaji amekuja, wakati sheria ya uwekezaji inataka wenyeji washirikishwe namba moja lakini namba mbili inataka wenyeji kama kuna ajira kwenye huo uwekezaji ndio wawe wa kwanza kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kukutaarifu kwamba, Njombe ni miongoni mwa maeneo ambayo wawekezaji wanawanyanyasa wananchi na ninashukuru Mungu kuna siku uli-*address* kwa *data* vizuri sana hapa. Tuna mwekezaji huyu anaitwa *BL*, wamekuwa wakiandamana wananchi kila siku, Mheshimiwa alishaelezea vizuri sana, kwa sababu yupo kwenye jimbo lake Njombe mjini. Amekuwa akinyanyasa wafanyakazi sana lakini Mheshimiwa Samia, mwaka jana alivyokuja alimpa ahueni ...

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba uchukue hela *CRDB* sisi Serikali tunakudhamini, amechukua zile pesa, amepeleka kwenye makampuni yake mengine ya Kenya na Uganda...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, unaongelea Njombe lakini ngoja kwanza kuna taarifa pale, ninamuona Mheshimiwa Naibu Waziri, amesimama.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 78(1) ambayo inaongelea kuhusu utaratibu. Ningependa kujua Kanuni ya 74(1) inasema, bila kuathiri mashariti ya Ibara ya 100 ya Katiba, yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, ukienda (k) inasema Mbunge, hatatumia lugha ya kuudhi inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sigrada, wakati anazungumza ametumia maneno ambayo yanadhalilisha wawekezaji na anasema, hakuna watu wanaoongoza kwa kunyanyasa raia kama wawekezaji. Lugha hii ni ya kuudhi, ni lugha ambayo inadhalilisha wawekezaji wanaokuja kuwekeza fedha nyingi katika nchi yetu ya Tanzania lakini kama haitoshi inaweka rehani nguvu kubwa anazotumia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuvutia wawekezaji kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini Mheshimiwa Mbunge anayezungumza anavunja utaratibu wa Bunge wa kutunza staha na kulinda watu

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongezee ...

MWENYEKITI: Tunaenda na mmoja mmoja kwanza.

Mheshimiwa Sigrada, kuna maneno kwamba ...

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hawa ndio tunao watafuta, hawa ndiyo wapo nyuma ya wawekezaji, ndio maana wawekezaji wanakuwaga na viburi sana. Hakuna lugha ya kuudhi niliyotumia, nimeongea uhalisia lakini pili, mimi nilishaambiwa humu sijitambui. Kwa hiyo fanya kama hayo maneno ameongea mtu asiyejitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea ...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Maneno kwamba. Mheshimiwa Sigrada polepole.

Maneno kwamba, "wananyanyasa wananchi" maana yake kimsingi unatakiwa uje na ushahidi hapa. Sasa kwa vile huwezi kutoa ushahidi ni bora ukayatoa.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ninao na ni Njombe ambapo *BL* amefukuza wafanyakazi wote walioandamana mwezi uliopita kudai mishahara yao na barua ninazo, kwa hiyo *simple* tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada!

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, anatakiwa kuleta ushahidi huyo.

MWENYEKITI: Ninaomba twende polepole. Yeye anaongea na kiti sasa hivi, msimchanganye Mheshimiwa Sigrada. Maneno kwamba, "wawekezaji wananyanyasa wananchi" maana yake hakuna muda wa kuuleta huo ushahidi hapa. Kwa hiyo ni bora ukayaondoa, kwa wakati muafaka ukaleta hoja yako kuhusiana na jambo hilo.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi dhambi nilizonazo zinatosha. Siwezi nikabadilisha lugha kwa sababu ninaamini kweli wananyanyasa, sasa niseme uwongo? Hii ndiyo lugha sahihi, wanawafukuza, hawawalipi mishahara, watu wanaandamana kila siku. Hilo tutumie lugha gani, kwamba wanawapenda au? Kunyanyasa nayo imekuwa ni *debate?*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kwa mujibu wa Kanuni zetu hautakiwi kubishana na Kiti. Hutakiwi kubishana na Kiti, aidha utoe hayo maneno au usiendelee kuchangia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Baba yangu, Mlezi wangu kwa heshima yako ninayaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, bahati mbaya muda wako na wenyewe umeisha, malizia kwa ku ....

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekunde moja.

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashauri Wizara, hebu wachunguze huu mfumo wa mabaraza ya ardhi ya Kata, mfumo wa ofisi za vijiji na mfumo wa Baraza la Ardhi Wilaya. Mfano, Njombe tuna Mahakama moja Mkoa mzima, Hakimu huyu azunguke nchi nzima, kama imewashinda hiyo *formula* rudisheni kwenye Mahakama za kawaida, kesi za ardhi zianzie Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Sigrada, Mbunge wa Viti Maalum Njombe. Nilimwita Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, atafuatia.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaomba nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Katika kuunga mkono hotuba hii nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri, uchukue kalamu na karatasi kwa sababu ninataka nikuulize na ninatarajia Mungu akipenda kesho ukihitimisha hotuba yako uweze kuniambia juu ya suala linalohusu urasimishaji wa makazi katika kata tisa jimboni kwangu Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikutajie hizo Kata na ndiyo maana nilikuwa ninahitaji uziandike ili uweze ukawauliza wataalamu wako wamefikia wapi katika suala zima la kupima

maeneo ambayo ni *squatters* sugu katika Mji wa Kinondoni, mji ambao tunasema Kinondoni ndiyo Dar es Salaam. Kinondoni yenyewe kuna Kata inaitwa Kinondoni, Tandale, Mwananyamala, Makumbusho, Kigogo, Magomeni, Ndugumbi, Mzimuni na Kijitonyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 wakati nikiwa Diwani katika Kata ya Hananasif, tulifanya zoezi la kurasimisha Kata, Kata ile ikapimwa, wananchi wa pale wakapewa hati na wananchi wenyewe walichangia hata gharama za upimaji. Sasa naona ugumu uko wapi kwa sababu wananchi wako tayari hata mkiwahusisha katika kulipia baadhi ya gharama, wako tayari mji wao ukapimwa ili uweze ukapangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuupanga mkawazidishia uwezo wa kiuchumi wananchi wale wa Kinondoni. Hivyo nitatarajia Mungu akipenda kesho wakati ukihitimisha Mheshimiwa Waziri na nakuamini sana kwa uwezo wako, utakuja na majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikisoma madhumuni na sababu ya Sheria ya Ardhi Namba Nne ya mwaka 1999, nataka nisome mawili. Moja ya kuundwa kwa sheria ile ni kuwezesha ardhi itumike kiuchumi na pakaelezwa uhitaji wa kupanga, kumilikisha vilevile katika masuala ya mabadiliko ya matumizi. Sheria ilikuwa inalenga moja ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, moja ya maeneo ni kupunguza migogoro, sasa hali ikoje Mheshimiwa Waziri? Sheria hii ambayo imetungwa mwaka 1999 leo hii ina miaka 27. Wakati ikitungwa na mpaka leo, marekebisho yamefanyika zaidi ya mara 40 au na zaidi, katika kuliangalia suala la sheria yenyewe ije itumike kwa yale niliyokuambia, utakuta kwamba wakati sheria inatungwa, watu katika nchi hii walikuwa karibu milioni 30 na zaidi mpaka 1999, miaka 27 baadaye leo tuko watu wanaofikia zaidi ya watu milioni 70 na mahitaji yamekuwa yakiongezeka, mahitaji ya watu kumiliki ardhi, mahitaji ya usuluhisho wa migogoro, mahitaji yanayohusiana na *processes* zilizo ndefu kupunguzwa kwa maana ya urasimu migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Kinondoni alikuwa amekuja kwenye ziara fulani, katika moja ya mikutano tuliofanya pale llala, nafikiri 80% ya malalamiko yalihusu masuala ya ardhi. Hii maana yake migogoro imeendelea kukua wakati sheria ilitaka migogoro ipungue, hata sasa hivi najua mnafanya kliniki kila mahali pale inapobidi, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu kliniki zile zinaweza mkajikuta mnataka dispensari au hospitali za ardhi kwa sababu migogoro haipungui na ndiyo kwanza inaongezeka. Sasa nikiangalia hii sheria na mahitaji ya sasa hivi, naona kwamba kasi ya maendeleo ni kubwa sana kuliko uwezo wa sheria yenyewe. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, hebu kaeni na wataalam, fanyeni *review*. Hivi kweli sheria hii inaweza ikahimili Tanzania ya sasa, Tanzania ya kidijiti? Wakati sheria ikiundwa, masuala ya kidijiti yalikuwa hayapo, sasa hivi kuna matumizi makubwa ya kidijiti. Matumizi ambayo yanaweza yakaondoa *double allocation*, matumizi yanaweza kusaidia hata upangaji wa miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri hebu kaeni na wataalam muangalie na mjiulize kwamba kweli sheria hii inakidhi mahitaji ya Tanzania ya sasa? Nimependa sana mtazamo wa Wizara kwamba inataka kwenda kuboresha Sinza iwe mahali pazuri. Mimi nataka nikuambie Mheshimiwa Waziri, Dar es Salaam nzima inahitaji kufanyiwa chini ya mpango uliouzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam sasa hivi kuna maeneo yamechakaa. Maeneo yamechakaa wakati pale ndipo penye mapato makubwa ya Serikali, hebu Serikali iangalieni, na nilikuja na wazo moja kwamba Dar es Salaam yote ilivyo, iwe viwanda ya makazi au biashara lakini leo ukiangalia kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi, mahitaji ya kubadilisha matumizi ya ardhi imekuwa ni kero kubwa mno, inachukua muda mrefu sana kufanya mabadiliko ya ardhi ili ufanye biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami hii inanitia wasiwasi kwamba biashara zote tunaziona Dar es Salaam, hivi kweli wale wamepata idhini ya kubadilisha matumizi ya ardhi? Tunaikosesha Serikali mapato. Ombi langu, hebu sasa Serikali inaona ugumu gani kuitangaza Dar es Salaam kama ni eneo la makazi na biashara ili

hitaji la mabadiliko ya matumizi ya ardhi likaondolewa na kuondoa urasimu ili nchi yetu ikaweza kupiga hatua zaidi katika masuala ya kibiashara. Kwa sababu sasa hivi mahitaji ya fedha ni makubwa na watu wanazo, tunataka kuwekeza lakini urasimu umekuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umiliki wa ardhi na kutoa hati unaisaidia Serikali kupata mapato, lakini tuchukulie pale Dar es Salaam, kuna wakati wa sensa ya mwaka 2022 ya watu na makazi, wanasema kuna kaya milioni moja na laki tano na kwamba inakisiwa kati ya kaya hizo kwa maana ya nyumba na makazi, 20% ndio yenye hati. Hizi takwimu sina uhakika nazo, pengine Mheshimiwa Waziri unaweza ukaja na takwimu zinazoonesha nyumba zilizopo Dar es Salaam kama hizi takwimu mnazo na ni asilimia ngapi ya nyumba zile zina hati na ngapi zinalipa pango na ngapi hazilipi ili tuweze tukajua kwamba kuna mapato ya Serikali yanayopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi na hasa suala la upangaji wa miji ni muhimu sana katika kipindi chetu hiki. Kwa hali hiyo ukiangalia kwamba mahitaji ya upangaji wa ardhi kwa ukubwa wake ni uchumi pekee yake na nchi yetu haijapimwa yote, ingependeza katika moja ya mambo ambayo utakuja kumalizia hotuba yako utuambie Serikali inajipangaje kuhakikisha nchi yetu inapimwa kwa maana ya yale ma-*group* ya matumizi ya ardhi. Maeneo gani ya kilimo, maeneo gani ya viwanda, maeneo gani ya nyumba za kuishi na kadhalika na kadhalika ili nchi yetu hii iweze ikafanya vizuri masuala ya mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam tunazo *squatters* nyingi kwa sababu tulizembea katika masuala mazima ya upangaji wa miji. Huo ndiyo ukweli na ukweli lazima tuukabili, hatuna muda wa kusubiri, lazima sasa Serikali irekebishe na naamini hata ukienda miji mingine, miji mikubwa mingine ya Tanzania, hali ipo hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapo Ilala ambapo ndio Jiji kwa maana ya Jiji la Ilala kwa maana ya pale Dar es Salaam, bado kuna *squatters* kila unapozunguka *squatters* zipo, inawezekana vipi Tanzania ya leo miaka sitini na ushee ya uhuru

tunaendelea kuwa na *squatters?* Maeneo ambayo hayaisaidii Serikali kuweza kupata mapato zaidi, haisaidii wananchi wetu kuweza kujikwamua kiuchumi kwa sababu ukiwa na hati, maana yake unaweza kwenda ukakopa ukajikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wengi hawana hizo, wana leseni za makazi, benki haitoi mikopo kwa leseni za makazi. Wasaidieni Watanzania na hasa sisi Kinondoni tuko tayari mfanye *pilot project* kwamba Kinondoni ipimwe, wapate hati, halafu muone wananchi wa Tanzania wanavyoweza kupata maendeleo makubwa ya kiuchumi na tukaondokana na umaskini, halafu maeneo mengine yafuate, sisi tuko tayari kuonyesha barabara ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itampendeza Mheshimiwa Waziri baada ya vikao vya Bunge, twende tukatembee Kinondoni aone Kinondoni inavyochangamka na jinsi gani utasaidia maeneo mengine nayo yachangamke kiuchumi ili wananchi wa Tanzania waweze kufaidi maendeleo ya Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kulihutubia Taifa hili na naunga mkono hoja, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao tuwatambue ndani ya Ukumbi wa Bunge.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni waliopo ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Dkt. Juma Zuber Homera, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria, ambao ni Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, tuwaone, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliolitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 103 na walimu wawili kutoka Chuo cha Sayansi

na Teknolojia *(MUST)* kutoka Jijini Mbeya, tuwaone, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 49 wa Chuo cha St. John's kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa kuwa usajili wa mbio za Wakili Marathon 2026 zenye kaulimbiu ya kusogelea huduma za msaada wa kisheria karibu zaidi na Mtanzania, usajili huo unaendelea kwenye viwanja vya Bunge kwenye banda la Gezabo lililopo nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Mbio zinatarajiwa kufanyika siku ya Jumapili Tarehe 31 Mei, 2026 Jijini Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbushwa na mshauriwa kushiriki mbio hizo, mnahimizwa kushiriki mbio hizo muhimu sana kwa sababu hasa ya nia ya mbio hizo ya kusogeza huduma za msaada wa kisheria karibu na wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji ninamwita sasa Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae. Inaonekana kama hayupo, tunakwenda kwa mchangiaji anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Ali Khalil Mirza.

MHE. ALI KHALIL MIRZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima na kuweza kufanikisha shughuli yetu hii tunayoifanya leo jioni. Pia nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo makubwa anayotufanyia nchini kwetu ikiwemo sekta ya ardhi na kama ilivyosomwa leo kwenye bajeti pia ni kuongeza bajeti ya Wizara hii ya Ardhi. Zaidi kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunachangia Wizara ya Ardhi, sekta ya ardhi ni Wizara yenye umuhimu aina yake kwa vile yote tunayoyapanga, yote tunayoyazungumza, *vision* zetu, *mission* zetu vitu vyote vinakaa juu ya ardhi. Kwa hivyo, lazima sisi katika

michango yetu tujielekeze kutizama namna gani tunaweza tukaisaidia sekta hii ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi imeumbwa mara moja na Mwenyezi Mungu na toka ilivyoumbwa iko vilevile lakini inazidi kuwa ndogo na inazidi kuwa umuhimu na watu wanaongezeka na matumizi yanaongezeka na ndio maana leo inazalisha kile tunachokiita migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati unazungumza migogoro lazima tujue chanzo cha migogoro hii. Wizara inataka kusaidiwa kwa sababu suala la ardhi ni mtambuka, sote kwa njia moja au nyingine tunawajibika katika kuisaidia Wizara ya Ardhi kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitizama *population* yetu Tanzania, mwaka 2012 tulikuwa milioni 44. Leo tuko milioni karibu 70 na tutapofika mwaka 2050 tutakuwa zaidi ya watu milioni 115. Hali kadhalika hata ukuaji wetu ulikuwa asilimia 2.9 na leo tunakuwa kwa asilimia 3.2. Haya yote yanaonesha kwamba mahitaji ya ardhi yanaendelea kukua, hata hivyo takwimu za leo zinaonesha kwamba takriban watu 30% -32% wameshahamia mijini. Hali hiyo inapelekea *pressure* kubwa ya ardhi zaidi mijini na miji yote mikubwa Dodoma, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza imekuwa kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu ardhi inahitajiwa na wakazi, leo pia tuna tatizo lingine la ukuaji wa magari, sote hapa tuna magari, takwimu zinaonesha gari zilizo *registered* ni zaidi ya 4.5. Sasa hapa nini kinatokea? Kinachotokea ni kwamba ardhi ni ileile, umuhimu wake unazidi lakini inagombaniwa na kila mtu kwa sababu kila mtu anataka nafasi ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika ripoti yake ya mwaka jana imesema kwamba kumekuwa kuna migogoro elfu kumi na moja mia nane na sitini, hii ina maana gani? Ina maana kwamba kila migogoro inapokua, Wizara inalemewa na inatumia muda wake mwingi wa ku-*solve* migogoro kuliko kukaa kufikiri vipi inaweza kuleta maendeleo na hilo ni jambo muhimu. Kwa hivyo kwa upande wa Wizara kufuatia na *budget speech* aliyoisoma

Mheshimiwa Waziri inaonesha kwamba Wizara inajitahidi, inao mwelekeo mzuri na inajua vipi itakavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini cha kufanya? Ardhi tunaita ni *asset*, lakini ikiwa ardhi ile itaendelea kuwa na migogoro inaweza kugeuza *asset* na ikawa *liability* na sisi tunapaswa sasa hivi kuitumia ardhi zaidi katika mwelekeo wa uchumi, yaani *economics of land* na siyo ile *land use* ya kawaida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ninavyoona katika kuelekea huko na kwa vile dira zetu zote zinaonesha kwamba tunataka kukua, 2030 tufikie ukuaji wa asilimia saba kutoka asilimia 5.7 na 2050 tufikie kwenye uchumi wa trilioni moja, yale yote tuliyoyapanga yanawezekana lakini kuna mambo lazima tuanze kuyashughulikia kwa uhalisia wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri mambo manne mpaka matano ni muhimu. Kwanza suala la upangaji wa ardhi, *land use planning*, hilo ndio kipaumbele cha mwanzo. Kinachofuata ni kumtambua na kumthibitisha yule mwenye haki ya matumizi ya ardhi ile ili kuondoa migogoro kabla hata haijatokea. Kisha kuendelea kuipima ardhi na kutoa hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapokwenda katika kutoa hati au wenyewe wanaita *titling*, hiyo umuhimu wake ni kwamba kwanza inazalisha watu watakuwa na usalama wa umiliki, yaani *security of land* na hapo ndio inafanya kila mtu ajihisi kwamba ile ardhi anaweza kuitumia, akakaa nayo na anakuwa na uhalisia wake na *security* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ardhi ile inaweza kuchukulia mikopo na hapo ndilo suala lote la ardhi kuunganisha na kupunguza umaskini linapokuja. Ardhi inapoweza kuchukuliwa mikopo ina maana wananchi wanaweza kujiendeleza kipato, kiuchumi na kimaendeleo. Tatu, inapunguza ile migogoro ya ardhi wanavyoita migogoro au *land conflicts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni vizuri kuanza kuongeza *speed* ya kupanga, kupima na kutoa. Hakuna njia nyingine, hakuna mbadala mwingine na hakuna *shortcut* juu ya hilo. Hapa

kinachotokezea zaidi kwamba lile wimbi la uvamizi, wimbi la ukuaji ni kubwa kuliko uwezo wa wizara. Kwa hiyo wizara hii inastahili kusaidiwa, inastahili kupata bajeti kubwa, wataalamu ili tuweze kuwahi sasa hivi kwa sababu kila siku zinapokwenda na miaka inavyokwenda ndio tatizo linazidi kuwa gumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naunga mkono bajeti hii mia juu ya mia na naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako na nimwite sasa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nami nafasi niweze kusema machache kwa niaba ya Watanzania wenzangu wa Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba mimi tangu nazaliwa, nimekua, nimeikuta ardhi ya Tanzania ni hii hii ambayo mpaka leo nami nimetotoa ardhi yetu ni hii hii haijawahi kuongezeka kipande cha ardhi kutoka sehemu yoyote! Maana yake ni kwamba watu tunaongezeka, ardhi yetu haiongezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo yenye dhamana ya kuamua shughuli zetu, mipango yetu, mikakati yetu na mambo yetu yote ya kila siku. Wao ndiyo wenye hatima na ardhi yetu tuliyonayo.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

TAARIFA

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Ninapenda kumpa taarifa tu Ndugu yangu anayechangia Mheshimiwa Mbunge kuwa, binadamu hatotoi,

anayetotoa ni ndege, binadamu huwa anazaa au anajifungua. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitwa Kunti, Mbunge wa Jimbo la Chemba na Mheshimiwa Sigrada ni Mbunge wako wa Viti Maalum, Mkoa wa Njombe. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Samahani, Mheshimiwa Kunti.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea ni kweli binadamu hatotoi. Sasa sijui anazaa au anajifungua Kaka yangu atanisaidia.*(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Ardhi ni Wizara muhimu sana lakini kwa jicho la pili, Wizara hii ndiyo chanzo cha migogoro na matatizo ya ardhi ndani ya Taifa hili. Wizara hii, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi wanayo wao, miradi ya namna bora ya kupanga, kupima na kumilikisha iko kwao. Wizara hii ndiyo ina taasisi kwa ajili ya kuweza kuendeleza makazi ndani ya Taifa letu iko kwao *NHC*, lakini tukiangalia Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, hivi wako wapi? Wanafanya nini? Wapi na saa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya Chemba mwaka 2024 mwezi wa Septemba, tuliwaandikia barua tukiwaomba tuna vijiji 11 ambavyo vina kero na mateso ya migogoro. Hata tu kutujibu barua kwamba wamepokea, hawajawahi tangu 2024. Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi kujibu tu barua, achana kwamba sasa huna uwezo, kusema tu tunashukuru tumepokea tutashughulikia, wao haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa chombo cha namna hii, watu wa namna hii, yaani tunamalizaje migogoro? Migogoro inaishaje kwa staili hii kama huwezi kujibu barua iliyokufika ofisini kwako? Mheshimiwa Waziri, tunakuomba na mimi hii barua nakuomba waambie wataalam wako wakutafutie hiyo barua wakupe. Mimi leo siitoi ninayo, ila nakuomba waitafute hiyo barua utuambie barua yetu tuliyoiandika mwaka 2024 ya kupima vijiji 11; Vijiji vya Handa, Lahoda, Ndoroboni, Isini, Kelemakuu, Rofati, Tumbakose,

Moto, Gonga pamoja na Probanguma, ni lini mtatujibu hiyo barua na ni lini majibu hayo yakija, ni lini mtakwenda kutusaidia? Kwa sababu hivyo vijiji vina migogoro watu wanauawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili, kwenye migogoro hiyo hiyo, watu wetu wanasaga na kumaliza viatu kwa ajili ya kwenda kwenye Wizara ya Ardhi kutafuta suluhu, jambo hilo limejionesha dhahiri shahiri hadharani kwenye ziara za Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo pekee na kero pekee inayotikisa leo nchi yetu ni migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila anakokanyaga Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukiambiwa kero watu wana mafaili na mafaili wamerundika, wanamletea Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikawa najaribu kutafakari, hivi Wizara ya Ardhi, Waziri na timu yake wanajisikiaje? Wanaona fahari gani Waziri Mkuu kuteseka kila siku, kwenye kila Wilaya, kila Halmashauri watu wanahangaika na migogoro ya ardhi? Wao wanajisikiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli hawana cha kufanya? Hivi ni kweli Wizara ya Ardhi, tumeamua kwamba Waziri Mkuu ndiyo akatatue migogoro ya ardhi na wao wapo? Ndiyo kazi aliyochaguliwa Mheshimiwa Waziri Mkuu? Sasa, kama Waziri Mkuu anaweza kutatua hiyo migogoro, kwa nini tuna Wizara ya Ardhi? Kwa nini tusiifute ili abaki Waziri Mkuu amalize migogoro yote tuliyonayo? Yaani wao wapo kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna mgogoro, watu wangu wametembea, Bunge lililopita iliundwa timu ya Mawaziri Nane, timu ya Mawaziri Nane, wakaunda timu ndogo ya wataalamu wameenda kati ya mgogoro wa *WMA* Makame pamoja na watu wa kwangu Mrijo lakini pamoja na watu wengine wa Kiteto. Mheshimiwa Waziri watu hawa wamekuja ofisini kwako zaidi ya mara moja, nimekufuata kwenye kiti chako, ukaniambia Mheshimiwa Mbunge sawa ninalishughulikia, kweli sisi tunaratibu na ukanipa matumaini kwamba nitamtuma Naibu Waziri wangu akirudi yuko safarini, sijaona hata hiyo dalili ya kumtuma huyo Naibu Waziri wako. Sijaiona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakuja kila leo mmebakisha kwenda kusema... tuambieni Mheshimiwa Waziri shida ni nini? Timu imefanya kazi imemaliza, inaripoti mezani lakini ni nini la kusema hiyo ripoti? Waambieni Watanzania kinachojiri, mimi watu wangu wanatamani kusikia kauli ya Serikali kwamba, yale mashamba mnawapa ama hamuwapi. ni hilo tu! Nendeni mkawaambie, karekebisheni hiyo migogoro, katatuweni, waacheni watu wawe huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunawatesa watu kwenye kitu ambacho hakiwezekani? Sema hakiwezekani hakuna atakayekunyonga, badala ya kuendelea kuwapotezea muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunapoteza rasilimali fedha kidogo walizonazo, huku tunawanyang'anya mashamba yao, halafu huku ninyi mnaendelea kuwanyonya, wanalipa nauli kila siku, kuwafuata ofisini. Wenzetu mna *V8*, mna magari nini, mafuta mnajaziwa na Serikali, wale wanachukua chao kidogo walichonacho, ambapo hata hayo mashamba mmeshanyang'anya hawana mahali pa kwenda hata kulima!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akija naomba aniambie huo mgogoro unakwisha lini? Unakwenda lini kuwaambia wananchi wa Wilaya ya Kiteto pamoja na Chemba, suala la mgogoro wao huo wa hayo mashamba, pamoja na hifadhi, ninyi ndiyo mlikuwa mnaratibu huo mgogoro, lini mnakwenda kutoa tamko la huo mgogoro kuisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la tatu, *NHC* walikuja kuchukua viwanja Chemba tangu mwaka 2015, nia ya kuchukua viwanja pale ni kwa ajili ya kujenga nyumba za bei rahisi kwa ajili ya watumishi na watu wengine. Tunavyoongea ni mwaka wa 11 mwananchi wa kawaida leo akichukua kiwanja asipokiendeleza mnamnyang'anya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi Wizara ya Ardhi mmechukua viwanja Chemba, mpaka leo hamjathubutu kufanya jambo lolote, mkija mniambie *NHC*, vile viwanja mlivyochukua Chemba mwaka 2015 mnakuja kuviendeleza au hamviendelezi? Kama hamviendelezi tuambieni tuwauzie watu wengine, wako

wanaohitaji kama ninyi hamtaki kuja kutuhudumia Wana-Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la nne, Chemba ni Wilaya mpya, hivi ninavyoongea nina Afisa Ardhi ambaye anakaimu mwaka wa pili. Sina Afisa Mipango wala sina Mthamini Wilaya. Watu wetu leo, tembo wanaharibu mazao, tukihitaji Mthamini inabidi mkulima amtafute Mthamini kutoka Dodoma, amlipie gharama zote ndiyo aende akafanye utathmini. Mifugo imeingia kwenye shamba la mkulima, ama kuna jambo lolote tunahitaji kufanya uthamini ni lazima mwananchi anayetaka hiyo huduma, twende tumtafute ndiyo aje atuhudumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Chemba tunarudi nyuma, Mheshimiwa Waziri nikuombe hali kadhalika tusaidie, tunaomba Mthamini wa Wilaya, tunaomba yule Afisa Ardhi aliyeko pale kama hafai, muondoeni tuleteeni Afisa Ardhi mwenye mamlaka kamili aliyethibitishwa. Pia, tunaomba Afisa Mipango Miji, Chemba tunakwenda kuwa Manispaa, tunahitaji kupata Afisa Mipango Miji, tupange mji wetu wa Chemba, tuachane na *squatter* ambazo wanaongelea akina Mheshimiwa Tarimba za huko Dar es Salaam. Sisi Chemba tunataka kuwa *smart*, hatutaki kuendelea kuwa na *squatters,* tuleteeni Afisa Mipango Miji tupange mji wetu vizuri, watu waishi vizuri bila kuwa na migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ninapokwenda kumalizia, tunao mradi ule wa KKK tuliosema. Mheshimiwa Waziri na timu yako nikuombe, Mji wa Chemba unakua sana, tunaomba hizi Halmashauri ambazo mmeziwezesha, twendeni sasa kwenye Halmashauri zile nyingine ambazo hamziwezeshi. Sisi Chemba tuko tayari kuwalipa, tupeni fedha tuambieni mnataka nini kutoka kwetu, tupatieni fedha twende tukatengeneze mazingira rafiki ya kuweka miundombinu mizuri kwa ajili ya watu wetu na makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala zima la Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Chemba, hali kadhalika hatuna Mwenyekiti huyo. Mheshimiwa Waziri, tunahitaji, watu wangu wanapata taabu sana, wakimaliza Mabaraza ya

Kata wanatakiwa kutoka Chemba ama kutoka Kata nyingine zote waende Kondoa ama waje Dodoma. Kwa hiyo, tunaomba Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi ili wananchi wangu waweze kuhudumiwa kwenye Makao Makuu yao ya Wilaya, badala ya kuendelea kupoteza gharama na muda mrefu wa kusafiri kwa ajili ya kutafuta hiyo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninakushukuru, ahsante sana kwa muda wako. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi hiki cha jioni cha uchangiaji. Sasa nitaahirisha Kikao hiki cha Bunge mpaka kesho Ijumaa, tarehe 29 Mei, 2026 saa tatu asubuhi.

(Saa 12.48 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 29 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)